# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

### Kikao Cha Nne – Tarehe 30 Agosti, 2013

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, Kikao cha Nne cha Mkutano wetu wa 12 kinaanza.

Katibu tuendelee?

### MASWALI NA MAJIBU

Na. 39

**Hospitali ya Misheni ya Kibara Kuwa Hospitali Teule**

**MHE. ESTHER A. BULAYA (K.n.y. MHE. KANGI A. LUGOLA)** aliuliza:-

Je, kuna sababu gani kwa Serikali, kutoifanya Hospitali ya Misheni ya Kibara, kuwa Hospitali Teule?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA *(TAMISEMI)*** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mwibara liko katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda. Halmashauri hii ina Hospitali mbili zinazomilikiwa na Mashirika ya Dini, yaani Hospitali ya Bunda inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania *(KKKT)* na Hospitali ya Kibara inayomilikiwa na Kanisa Katoliki. Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, haina Hospitali ya Wilaya inayomilikiwa na Serikali na kwa kuzingatia hilo mwaka 1992 iliamuliwa kuwa Hospitali ya Bunda inayomilikiwa na *KKKT* iwe Hospitali Teule ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa naibu Spika, wananchi wa eneo la Kibara katika Jimbo la Mwibara ambao wanafikia idadi ya watu 121,000 hutembea umbali wa Kilomita 60 kufuata huduma za afya katika Hospitali Teule ya Bunda. Hospitali ya Misheni iliyopo katika Makao Makuu ya Kata ya Kibara, hakuna Kituo cha Afya kinachomilikiwa na Serikali wala Sekta Binafsi. Kituo cha Afya cha karibu kipo katika Kata ya

Kasahunga umbali wa kilometa 11 kutoka yalipo Makao Makuu ya Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda inaweza kuingia *"Service Agreement"* na Hospitali ya Misheni ya Kibara ili kuweza kutoa huduma kwa kiwango kinacholingana na Hospitali Teule. Utaratibu unaotakiwa kufuatwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kupitisha maombi hayo katika Vikao vya Kisheria kama vile Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Mkoa *(RCC)* na baadaye kuwasilisha maombi hayo kwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ambaye kwa kupitia Wataalamu wake watajiridhisha na kutoa kibali kama watakavyoona inafaa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa sababu, maombi ya Wana-Kibara sio kuingia *"Service Agreement Contract"* kwa sababu, haitabadilisha mazingira ya kutoa huduma ya afya kama ambavyo yako kwa sasa hivi. Wao wanachotaka hii iwe Hospitali Teule, wapate huduma ambazo Serikali, wanapeleka kwenye Hospitali ya *DDH* kama dawa kutoka *MSD,* vifaa tiba pamoja na kuwalipa mishahara wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wafanyakazi pale wanapata tabu na hata wafanyakazi 11 Serikali, imewachukua na imewapeleka katika vituo vingine vya afya na kuendelea kuleta usumbufu katika Hospitali hiyo ya Kibara.

Je, ni lini Serikali, itaona umuhimu wa kuibadilisha Hospitali hii na kuwa Hospitali Teule? Swali langu la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Kidogo nimeshangaa Mheshimiwa kusema Wilaya ya Bunda haina Hospitali ya Wilaya, wakati Kituo cha Afya cha Manyamanyama, Wizara imeamua iwe Hospitali ya Wilaya ya Bunda na hivi ninavyoongea tayari kibao kimewekwa pale, lakini mpaka sasa hivi bado hospitali ile inapata mgawo kama Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni lini Serikali, itahakikisha Kituo cha Afya cha Manyamanyama, ambayo ni Hospitali ya Wilaya, wanaanza kupata mgawo rasmi wa vifaa tiba na dawa kama Hospitali ya Wilaya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA *(TAMISEMI)*:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Esther Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba sana Mbunge, anisikilize vizuri. Najua *concerns* zake hapa, anaeleza kwamba, hizi huduma hazipatikani; mimi namweleza utaratibu unaotakiwa kutumika ili huduma hizo ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani hapa Mheshimiwa Bulaya, mimi siwezi kukuza jambo lolote unalozungumza

hapa. *The bottom line is,* bila kufuata utaratibu tunaousema hapa kama Serikali, hii habari yote ninayozungumza hapa nitakuwa ninasema uwongo Mheshimiwa kwamba, tutakwensda kuingia pale. Maana yake ni nini, hiki kinachozungumzwa hapa tunazungumza habari ya Hospitali Teule; Hospitali Teule maana yake ni kwamba, utakwenda kufanya Mkataba na Kanisa katoliki. Maana yake ni kwamba, utasema hivi huduma zote za ki-serikali ambazo zinatolewa katika ile Halmashauri zihame zipelekwe katika Hospitali ile ya Katoliki pale; maana yake ni pamoja na kupeleka ruzuku pale. Maana yake ni pamoja na kupeleka watumishi pale. Maana yake ni kupeleka na hivi vyote ambavyo Mheshimiwa amevizungumza hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekiri hapa. Nataka niwaambie tumekesha, mimi saa sita usiku ndio nalala kwa ajili ya kutafuta ukweli wa jambo hili. Tujue jinsi ya kuwasaidia wananchi wa Mwibara, ambao wanasota mle. Mimi namwomba Mheshimiwa, atuelewe tunaposema hapa hatutaweza kuingia katika jambo hili mpaka wafuate utaratibu huu tunaousema; Halmashauri ya Wilaya ya Bunda inatakiwa ikae kwa sababu, ina *Budget Implications* zake hapa. Mimi nataka nimwahidi Mheshimiwa Esther Bulaya, nimwambie kwamba, nitashirikiana na yeye kuhakikisha kwamba, wananchi hawa wanapata hicho wanachotaka kupata hapa, lakini kwa kufuata utaratibu huu tunaosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili. Anazungumza habari ya Hospitali ya Mayamaya; iko hapa tumeizungumza na tumeitaja hapa. Ngoja nikutajie vitu ambavyo vimeshafanyika hapa, tumeweka upanuzi wa jengo la *OPD,*

tumeweka jengo jipya la Utawala limeshajengwa, tumeweka jengo la upasuaji na wodi nne – wanawake, watoto, wanaume na wazazi. Majengo haya yote yanafanya kazi. Kazi ambazo hazijafanyika ni jengo la utakasaji, *mortuary,* njia za kutembelea na uzio.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukishayamaliza mambo haya yote, kama tulivyosema kwenye utaratibu huu, hapa hakuna ugomvi mzee wangu. Mimi nasema utaratibu unavyotakiwa. Atatoka hapa Mheshimiwa Mwinyi pamoja na Mheshimiwa Seif, watume watu wao waende mpaka kule wakakague yale majengo, waseme naam, hii tunaridhika kwamba, inafaa kuwa Hospitali ya Wilaya. Huo ndio utaratibu. Baada ya hapo hakuna ugomvi, sisi Ofisi ya Waziri Mkuu tutafuata yale yote yaliyoshauriwa katika swali hili.

Na. 40

**Utafiti wa Makaa ya Mawe Magamba**

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE (K.n.y. MHE. GODFREY W. ZAMBI)** aliuliza:-

(a) Je, utafiti huu utakamilika lini?

(b) Je, wananchi wa Isansa na Mbozi kwa ujumla, wategemee nini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, inatambua kuwepo kwa madini aina ya makaa ya mawe katika Wilaya ya Mbozi. Kutokana na utafiti wa kijiolojia uliofanywa na Wakala wa Jiolojia Tanzania, yaani *Geological Survey of Tanzania (GST),* Wilaya ya Mbozi inayo Jiolojia yenye mfumo wa miamba ijulijkanayo kama *Karoo.*

Mfumo huu una aina ya madini ya makaa ya mawe. Miamba hii ina uwezekano mkubwa wa kuwa na mashapo ya kutosha ya madini ya makaa ya mawe yanayoweza kuchimbwa kibiashara.

Kwa sasa kampuni ya Kitanzania ya *Magamba Coal Ltd.,* imekamilisha utafiti kwa hatua ya awali iliyoiwezesha kampuni hiyo kuomba leseni ya kuchimba makaa ya mawe ikiwa imeambatanisha Hati ya Tathmini ya Uharibifu wa Mazingira. Taratibu za kutoa leseni ya uchimbaji, zinakamilishwa. Aidha, hata baada ya leseni kutolewa kazi ya utafiti itaendelea ili kuongeza uhai wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Sera ya Madini ya Mwaka 2009, Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na Kanuni zake, Serikali, imeendelea kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, ili walete mitaji kuwekeza katika sekta ya madini, ikiwemo eneo la Magamba Wilayani Mbozi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, inawahakikishia wananchi wa Isansa na Mbozi kuwa, inasimamia kwa karibu uwekezaji katika eneo la Magamba na kuhakikisha kwamba, Taifa na Watanzania kwa ujumla wananufaika ipasavyo.

Aidha, wananchi wa Isansa na Mbozi, wategemee kuwa, mgodi wa makaa ya mawe utakapoanzishwa wataweza kujipatia ajira, ushuru wa Halmashauri pamoja na mapato yatokanayo na utoaji wa huduma zinazohitajika migodini.

Sambamba na manufaa hayo na kama ilivyo kwenye migodi mingine, vijiji vinavyouzunguka mgodi huu vitanufaika na huduma za jamii zitolewazo na mwekezaji kwa utaratibu wa *Corporate Social Responsibility (CSR).*

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Serikali imejitahidi sana kufanya tafiti nyingi zinazohusu madini katika maeneo mengi, yakiwemo maeneo ya safu za Milima ya *Livingstone* inayosambaa kutoka Wilaya ya Kyela, Makete, Rungwe, Ludewa na sasa mpaka huko Wilaya ya Nyasa. Lakini matokeo ya tafiti hizo hayajawekwa wazi kwa wananchi, ili waweze kujiandaa nao kifikra na kimipangilio, ili waweze kuanza kuchimba madini hayo.

Je, ni lini sasa Serikali, itasambaza matokeo ya tafiti hizo kwa wananchi wote hapa Tanzania, ili kufahamu ni madini aina gani, kiasi gani, yaliyoko katika maeneo hayo yaliyofanyiwa utafiti?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hilda Ngoye, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, ziko tafiti mbalimbali zinazofanyika nchini kwenye sekta ya madini. Na kwamba, baada ya tafiti hizo kukamilika ndipo utaratibu wa leseni na uzalishaji huanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge hapa anataka kujua ni lini tafiti hizi zitakuwa zikiwekwa wazi kwa wananchi; tunao utaratibu na kazi nzuri inayofanywa na Shirika letu la Wakala wa Utafiti linalojulikana kama *Geological Survey of Tanzania (GST),* ambao wana tafiti za awali za nchi nzima.

Niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge, wale wanaopenda kujua taarifa za kijiolojia za maeneo wanayotoka wafike *GST,* ili waweze kupatiwa hizo tafiti za awali. Lakini tafiti za kina ili uweze kwenda kwenye uzalishaji zinakuwa ni mali ya yule anayefanya utafiti ingawa ni haki ya wananchi kwa sababu na wao ni wadau kufahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalichukua wazo hili tuone namna bora ambayo inaweza ikafanyika, ili kuweza

kuwapa Taarifa hizi za utafiti hata wadau wengine, wakiwemo wananchi na Viongozi wanaotoka katika maeneo hayo.

Na. 41

## Sera ya Madini ya Mwaka 1997

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI** aliuliza:-

Moja ya mikakati ya Sera ya Madini ya Mwaka 1997 ni kuhakikisha wachimbaji wadogo wanapata uwezo wa kukopa katika taasisi za fedha:-

(a) Je, wachimbaji wadogo wa almasi wanaozunguka mgodi wa Mwadui na *New Almasi* wamewezeshwa vipi, ili na wao waweze kuwa wachimbaji wakubwa?

(b) Je, ni Wataalamu wangapi wa fedha hasa waliobobea katika sekta ya madini wanashirikiana na asasi zinazofanya kazi na wachimbaji wadogo, ili kupata mitaji?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Mhoja Kasulumbayi, lenye sehemu *(a)* na *(b),* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Madini ya mwaka 1997 ilifutwa baada ya kutungwa kwa Sera ya Madini ya Mwaka 2009 kwa lengo la kukabiliana na changamoto zilizotokana na utekelezaji wa Sera hiyo, hususan kuhakikisha kuwa Sekta ya Madini inachangia ipasavyo katika pato la Taifa.

Pamoja na masuala mengine yaliyomo kwenye Sera ya Madini ya Mwaka 2009, suala la kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini nchini ili shughuli zao ziweze kuwa na tija na kuongeza mchango katika pato la Taifa, limesisitizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kasulumbayi, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha utekelezaji wa Sera ya Madini ya Mwaka 1997, pamoja na hatua muhimu zilizochukuliwa na Serikali, kuwawezesha wachimbaji wadogo wa almasi wanaozunguka mgodi wa Mwadui na *New Almasi,* ni kuwarasimisha kwa kuwapatia maeneo ya uchimbaji mdogo ili waweze kuyamimiliki Kisheria.

Jambo hili lilifanyika mwaka 2004 ambapo eneo la Maganzo, lenye ukubwa wa takribani kilometa za mraba 137.43 lilitengwa kwa wachimbaji wadogo na kupimwa viwanja zaidi ya 1,000 ambavyo viligawiwa kwa wachimbaji wadogo wa madini ya almasi. Wachimbaji hao waliendelea kupata huduma za ugani kutoka Ofisi ya Madini ya Kanda ya Kati Magharibi, iliyoko mjini Shinyanga.

Aidha, Serikali, imeanzisha mpango wa kutenga fedha kwa ajili ya mfuko wa kuendeleza shughuli za uchimbaji mdogo nchini. Mpango huu unatarajiwa kuwa endelevu ili wachimbaji wengi waweze kunufaika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu haina takwimu za idadi ya Wataalamu wa Fedha waliobobea katika Sekta ya ya Madini ambao wapo nje ya ajira ya utumishi wa umma, wanaoshirikiana na asasi zinazofanya kazi na wachimbaji wadogo kwa lengo la kuwapatia mtaji wakutosha wa kuwasaidia wachimbaji wadogo kwa ufanisi zaidi, Wizara yangu imewaelekeza Wataalamu wa Madini wa Wizara na Taasisi zake kushirikiana na wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Mamlaka ya Ufundi *(VETA),* Shirika la Viwanda Vidogo *(SIDO)* na Benki ya Rasilimali ya Tanzania *(TIB).*

Kwa kutumia ushirikiano huu na wenye taaluma katika Nyanja mbalimbali, ikiwemo Wataalamu wa fedha, tunaweza kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazowakabili wachimbaji wadogo nchini kwa lengo la kuufanya uchimbaji mdogo kuwa endelevu na wenye manufaa kwa Taifa.

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa maelezo yake imedai kwamba, imeshalirasimisha eneo la kilometa za mraba 137.43.

Je, kama kweli hali iko hivyo, ni kwa nini kila kukicha wachimbaji wadogo wa eneo hilo huwa kila wakati wanakamatwa na wengine hata kuuliwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Katika eneo la *New Almasi,* ambalo lilisharejeshwa Serikalini tangu tarehe 31 Mei, 1965 eneo hilo kwa sasa anayelimiliki ni nani? Kwa sababu, vijana wetu ambao ni wachimbaji wadogo wanaendelea kuuliwa na kukamatwa kila kukicha. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasulumbayi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kama zimetengwa hizo kilomita 137.43 katika eneo husika bado wachimbaji wadogo wanahangaika kutafuta maeneo ya uchimbaji. Jibu hapa ni kwamba wachimbaji wadogo hawa hakuna *control* yaani huwezi ukasema hawa ndiyo wametosha. Kwa hiyo, kila kukicha wanaongezeka. Kwa hiyo, hata hii itaendelea kuwa ni changamoto kwa sababu maeneo yana kiasi chake lakini wachimbaji hawa wanaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo juhudi ambayo Serikali tunafanya katika Wizara ya Nishati na Madini ni kwamba tunajua changamoto hiyo itaendelea na tunajua wataendelea kuzaliwa wachimbaji wadogo wengi na sisi tutaendelea kuwa tunaendelea kutafuta maeneo kadiri tunavyoweza kuyapata ili kuweza kuwagawia.

Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo litakuwa endelevu, Mheshimiwa ningeomba ukubaliane tu kwamba pale

wanapokuwa wanaongezeka basi unatuona tunaweza kuona namna gani tufanye na kwa maana hiyo sasa hata swali lake la pili kwamba kuna eneo ambalo tangu mwaka 1995 liko chini ya Serikali ngoja tukae tuone kama na hilo nalo kwa sababu namna ya uendelezaji wa hii migodi lazima tuone pia tunaiendeleza kwa faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia lazima tuone ni aina gani ya teknolojia ambayo inapaswa kutumika katika kuendesha huo mgodi.

Mahali pengine ukimpeleka mchimbaji mdogo hakika unaona kabisa hana mtaji wa kuweza kuchimba. Vinginevyo nichukue tu hili wazo lako la kuona tunaweza tukafanya nini, siyo tu katika eneo hilo ulilolitaja, lakini pia na maeneo mengine ili tuendelee kupambana na hii changamoto ya wachimbaji wadogo ambao wanaongezeka kila kukicha.

Na. 42

## Aina za Kodi na Ushuru Tanzania

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Je, Tanzania ina aina ngapi za kodi na ushuru?

(b) Je, ni watu wangapi wanategemewa kulipa kodi na wangapi hawalipi kwa kuzingatia idadi ya watu milioni 43.9 Tanzania Bara?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania inatoza kodi na ushuru za aina mbili, kodi zinazosimamiwa na Serikali kuu na zile kodi ambazo zinasimamiwa na Serikali za mitaa. Serikali kuu inatoza kodi na ushuru katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza kodi ya mapato kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya kodi ya mapato kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya kodi ya Mapato Sura ya 332, kodi ya ongezeko la thamani kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la thamani sura ya 148, Ushuru wa Bidhaa kama ilivyoainishwa kwenye sheria ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004 na marekebisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kodi nyingine ambazo zinakusanywa na Serikali Kuu ni kodi ya ushuru wa magari, kodi ya ushuru wa viwanja vya ndege, ushuru wa Bandari pamoja na tozo ya Maendeleo ya Ufundi na Elimu.

Kwa upande wa Serikali za Mitaa, kutoza ada mbalimbali kwa mujibu Sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato ili mtu aweze kulipa kodi ni lazima awe na kipato. Kipato hicho kinapatikana kwa njia ya kufanya biashara au kufanya kazi na kupata ujira.

Vile vile kwa mujibu wa Sheria ya mapato siyo Wafanyabiashara wote wanatakiwa kulipa kodi kulingana na mabadiliko ya Sheria yaliyopitishwa na Bunge mwaka 2012/2013 mfanyabiashara ambaye anapata kipato cha zaidi ya shilingi milioni nne kwa mwaka ndiye anayestahili kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili mfanyabiashara aweze kulipa kodi ni lazima apate usajiri wa mlipa kodi kutoka mamlaka ya mapato hadi kufikia tarehe 31 mwezi wa saba mwaka 2013 idadi ya walipa kodi waliosajiliwa ni kama ifuatavyo:-

Ulipaji wa Kodi ya Mapato ambao wenye *TIN Number* ni 1,199,942, ulipaji wa kodi la ongezeko la thamanni ya *VAT* ni 21,659, idadi hii haijumuishi wafanyakazi wanaokatwa kodi moja kwa moja kutoka kwa waajiri wao yaani kama wafanyakazi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mabadiliko ya Sheria ya Kodi ya Mapato ni wafanyakazi wanaopata mshahara wa zaidi ya shilingi 170,000/= kwa mwezi ndiyo ambao wanastahili kulipa kodi. Aidha Mamlaka ya Mapato

ina jumla ya waajiri 92,510 ambao wanawasilisha kodi za watumishi wao *(PAYE).*

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na baada ya hayo nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya Serikali yanategemea kodi za wananchi wake idadi ambayo imeonyeshwa ndani ya majibu haya ni ndogo sana hailingani na wafanyabiashara ambao wana kipato cha zaidi ya shilingi milioni nne.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha kwamba wale wote ambao wana kipato cha Shilingi milioni nne na zaidi wanajisajiri na kulipa kodi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli idadi bado ni ndogo sana ukilinganisha na hali halisi ya mapato ya Tanzania pamoja na maendeleo lakini kuna jitihada mbalimbali ambazo tunaendelea kuzifanya ni pamoja na kuwasajili wale wote ambao wanafanyabiashara ili nao waweze kuwa wanalipa kodi.

Lakini *initiative* inayoendelea ya kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wote wenye haya mapato nao wanaingia ama wanunua vifaa hivyo vya *Electronic Fiscal*

*Devices* ambazo nazo zitasaidia wao kuweza kujua mapato yao lakini vile vile Serikali kupata mapato mengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mpango ambao unaendelea wa *Cooperate Plan* ya Mamlaka ya Mapato pamoja na kazi nyingine ni pamoja na kuhakikisha kwamba tunakwenda sasa *deep down* kuweza kuhakikisha wafanyabiashara wote ambao wanastahili kulipa kodi wanalipa kodi hii ni pamoja na ku-*strengthen capacity* ya watumishi wetu wa *TRA* kuweza kuhakikisha kwamba wanakwenda na wanaweza kufanya *analysis* ya wafanyabiashara ambao wanastahili sasa kulipa kodi ili Serikali ipate kodi stahiki kama inavyotarajiwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri kwamba kodi ni jambo la msingi na linaleta tija kwa Taifa letu. Lakini takwimu zinaonyesha kwamba majengo yote ya Chama cha Mapinduzi (CCM) pamoja na Viwanja vya mpira ambavyo vilichukuliwa bila ridhaa ya wananchi vingi havilipiwi kodi.

Hii ni pamoja na Ofisi za Chama cha Mapiduzi Iringa, vibanda wanavyouzia choma moto, pale Iringa Mjini na maeneo kadha wa kadha. Kodi ambayo ni ya *Property Tax.*

Je, hii ni sera ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwamba iwe inaweza kukusanya kodi wakati yenyewe haitozwi kodi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Msigwa kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna sera hiyo ya Chama cha Mapinduzi ya kuwa isilipe kodi sisi ni Serikali ambayo tunaongozwa na Serikali ambayo iko chini ya Chama cha Mapinduzi kwamba tunataka kuhakikisha kila mtu analipa kodi. Kwa hiyo, hayo majengo umeyataja tu wewe kwa sababu ya *interest* zako.

Lakini kuna majengo mengi ambayo tayari hayalipi kodi kwa maana hiyo katika mkakati wetu wa kuhakikisha kwamba sasa *Property Pax* inalipwa ni pamoja na majengo hayo. Kwa hiyo, hatuwezi ku-*discriminate t*u kwa sababu tu ya Chama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Serikali, Serikali ya Chama cha Mapinduzi na tunahakikisha kwamba tunataka kukusanya kodi kwa ajili ya kupata maendeleo ya Taifa hili. Kwa hiyo, Mchungaji Msigwa hata nyumba yako kama ipo tukiwa tunaingia katika hii *mass evaluation* ambayo tunakwenda nayo sasa na wewe tutahakikisha kuwa na wewe unalipa kodi.

Na. 43

**Uhuishaji wa Viwango vya Pensheni**

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA** aliuliza:-

Dhumuni la kuwalipa wastaafu pensheni ni kuwawezesha waishi maisha yanayokaribiana na yale ya utumishi wao na kwamba mifuko ya Hifadhi ya Jamii hutakiwa kuhuisha viwango vya Pensheni, (*indexation)* kulingana na kupanda kwa gharama za maisha na mfumuko wa bei.

Je, *PPF* walihuisha *(indexation)* viwango vya pensheni kwa wanachama wao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi, swali namba 43 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mifuko ya pensheni duniani ipo ya aina kuu mbili ile ya kuchangia na ile ambayo siyo ya kuchangia. Mifuko ya kuchangia hulipa mafao ya wanachama wake kulingana na hali na uwezo wa mfuko husika na kwa kuzingatia maelekezo ya mtaalamu/ mthamini wa pensheni yaani *actuary valuator.*

Mifuko isiyo ya kuchangia haizingatii utaratibu huu wa kitaalamu kwa kuwa hutegemea Bajeti za kila mwaka kwa Serikali husika kulipa mafao ya wanachama wake na kwa hivyo ni rahisi kwao pia kuhuisha pensheni kulingana na gharama za maisha tofauti na mifuko ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, *PPF* ni mfuko wa kuchangia ambao mafao ya wanachama wake wakati wowote yanategemea sana hali halisi ya kifedha ya mfuko kutokana na michango pamoja na uwekezaji. Fursa za uhakika za uwekezaji hapa nchini ni finyu na mara nyingi kinachopatikana hakiendani na mfumuko wa bei na kupanda kwa gharama za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafao ya pensheni yanayolipwa na mfuko huu yamethaminiwa tangu awali na hivyo mwanachama anapoanza uanachama yaani *defined benefit* hivyo hayana budi kulipwa kisheria. Mtu pekee ambaye anaweza kubainisha na kuelezea afya au hali ya kifedha ni mdhamini wa mfuko baada ya kufanya tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya tathmini kufanyika na kubaini ziada au pungufu katika dhima na mali za mfuko bodi ya wadhamini hushauriwa kuchukua hatua ya ama kuongeza viwango vya pensheni au kupunguza viwango vya kuchangia.

Mfuko wa *PPF* uliboresha pensheni mnamo mwezi Mei 2010 na hadi sasa kima cha chini cha Pensheni kinacholipwa na PPF ni 50,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi msimamizi na mdhibiti wa mifuko ya hifadhi ya jamii nchini kwa kushirikiana na na mifuko husika wanafanya mchakato wa kuangalia uwezekano wa kuhuisha viwango vya pensheni yaani *indexation* kwa kuzingatia uwezo wa mifuko pamoja na gharama za maisha.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe masikitiko yangu kwamba majibu haya ya Mheshimiwa Naibu Waziri yanakatisha tamaa wastaafu waliofanya kazi nzuri na hiki kima cha chini anachosema kimeongezwa ni kwa sababu ya Sheria ambayo inasema kima cha chini cha pensheni kiwe Sh. 50,000/= siyo *discretion* ya mfuko kama inavyofanya mifuko mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali kwa kuwa NSSF mfuko mwingine wa hifadhi wamefanya *indexation* yaani wamehuisha viwango vyao mara sita toka mwaka 2000 na mara ya mwisho wamefanya mwaka 2012 kwa kumpatia kila mtu aliyekuwa kwenye *payroll* ya kupata pensheni 52%.

Kila penshenia aliyekuwa kwenye *payroll* amepata 52% ya kima chake kile na mpaka sasa kima cha chini cha *NSSF* ni shilingi 80, 000/- kama hawa wameweza na mazingira yanayosemwa ni haya haya ya Tanzania ni kwa nini PPF wanawakandamiza wastaafu kwa kutokufanya zoezi hili la *indexation?*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa mujibu wa Sheria ya *Social Security Regulatory Authority* ambayo tumeipitisha hapa huwa naikumbuka *Part four* kifungu namba 32 kinamtaka huyo *Regulator* kuhakikisha kwamba mifuko hii ya hifadhi inafanya zoezi la *indexation* kila mara kulingana na hali ya kupanda kwa maisha.

Hivi Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hii *Social Security Regulatory Authority* imeshindwa kutimiza majukumu yake kwa kutokutekeleza Sheria ambayo ipo tumeipitisha hapa ya kuhakikisha kwamba *PPF* na mifuko mingine wanahuisha viwango vya wastaafu ili kusudi wastaafu nao waone kwamba wametumikia nchi hii kwa salama na amani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mbunge wa Singida magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba *PPF* wanawakandamiza wastaafu kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba *indexation* inaendana na kupata faida kwa mfuko wenyewe.

Sasa nilieleza kwamba kwa sasa hivi *SSRA* kwa kushirikiana na mifuko yote sasa inafanya *actuary evaluation* na kwa taarifa ni kwamba sasa hivi *actuary evaluation* tayari ripoti iko tayari na imeshapelekwa katika *Cabinet Secretariat* kwa ajili ya sasa kuingizwa katika Baraza la Mawaziri na kuridhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine ripoti hiyo itaangalia ni namna gani sasa tunaweza tukafanya *indexation* kwa mifuko yote ili sasa kuweka uwiano sawa kwa wastaafu ambao wanapata pensheni

zao katika mifuko mbalimbali. Hii itaondokana na ile sisi tuko *PPF* tunapata kidogo wengine wako *NSSF* wanapata nyingi na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili ni zoezi ambalo litakamilika hivi karibuni na kama nilivyosema tayari ripoti ipo kwa *Cabinet Secretariat* kwa ajili ya kuridhiwa kutokana na mapendekezo ambayo yametolewa.

Lakini kama alivyosema kwamba hiyo *valuation* inafanywa kwa kushirikiana pamoja na *SSRA* kwa hiyo *SSRA* nayo inatimiza wajibu wake kama vile ambavyo imeelezwa kwenye Sheria kwa kuhakikisha kwamba *actuary evaluation* inafanywa na mafao pamoja na faida inayopatikana inakuwa sawa katika mifuko yote.

Kwa hiyo *SSRA* kwa mpango huu kwamba inahakikisha kwamba inafuata hiyo Sheria ambayo imetajwa katika sheria, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Halima Mdee swali fupi sana la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kati ya wastaafu ambao wanaishi katika mazingira duni sana na ya hovyo ni wastaafu wa Jeshi ambao tunawaita Jeshi la akiba lakini vile vile kumekuwa kuna malalamiko sana kutoka kwa wanajeshi wastaafu kwamba kumekuwa na ubaguzi kati ya wanajeshi ambao walistaafu kabla ya 2007 na baada ya 2007.

Sasa Serikali hapa Bungeni imekuwa ikitoa ahadi nyingi sana kwa Waziri wa Ulinzi lakini vile vile kwa Waziri wa Fedha kuhusiana na kurekebisha hizi pensheni kiduchu za Wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka kupata kauli ya Serikali baada ya hizi ahadi nyingi sana na porojo nyingi sana. Ni lini Wanajeshi hawa waliostaafu pensheni zao zitafanyiwa marekebisho, ili japo ziendane na mazingira halisi ya uchumi wa Tanzania? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima James Mdee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli kilio hiki cha wastaafu wa jeshi kimekuwa ni kikubwa sana kwa sababu tu tulifanya marekebisho hapa kwa hiyo naomba tu nilichukue hili suala na kwenda kulifanyia kazi zaidi ili tujue *how much* hawa wanajeshi wetu tumeweza kuwapatia kile kilio kiduchu ambacho walikuwa wanakidai. Kwa hiyo, namshukuru sana kwa swali lake na nalichukua tutakwenda kulifanyia kazi kama inavyostahiki. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa naibu Waziri wa Fedha kwa jibu muhimu sana la busara maana yake Mheshimiwa Halima alituchonganisha. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo sasa tunaelekea huko Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, simwoni badala yake Mheshimiwa Rita Mlaki, atamwulizia swali lake.

Na. 44

**Vyombo vya Habari Kuhakikisha Amani ya Nchi**

**MHE. RITA M. MLAKI (K.n.y. MHE. ZARINA S. MADABIDA)** aliuliza:-

Vyombo vya habari vinachangia sana utulivu na amani ya nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuhakikisha kuwa vyombo hivyo haviharibu amani na utulivu wan chi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mbunge wa viti maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli vyombo vya habari ni mdau muhimu katika kuimarisha amani na utulivu wan chi yetu. Katika kuhakikisha kwamba vyombo vya habari vinatimiza dhima hii, Serikali imeendelea kuvitaka vyombo vya habari kufanya kazi kwa kuzingatia weledi na maadili ya kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha Serikali inakamilisha Sheria ya kusimamia vyombo vya habari itakayobainisha

wajibu wa wanahabari na vyombo vya habari kufanya kazi kwa kuzingatia weledi, maadili na misingi ya taaluma ya uandishi wa habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itahakikisha vyombo vya habari havishiriki kubomoa au kuhatarisha amani na utulivu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa waandishi wa habari, wahariri na wamiliki wa vyombo vya habari kuzingatia weledi na taaluma ili kujiepusha na habari zitakazopelekea uvunjifu wa amani nchini.

**MHE. RITA M. MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Je, Serikali inaweza kutuambia imechukua hatua gani pale ambapo imeona vyombo vya habari vimevunja maadili au vimepotosha amani kwa kiwango fulani?

(b) Serikali inaweza ikatuambia imekutana mara ngapi na vyombo ambavyo vinasimamia Waandishi wa Habari kama *MOAT,* Jukwaa la Wahariri, Baraza na kadhalika ili kujadili pale ambako inaona kuna upotoshaji wa habari au pale ambako unaona kuna malalamiko ya wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema

katika majibu yangu ya msingi ni kwamba, Serikali itahakikisha kwamba, vyombo vya habari haviwezi vikabomoa au kuhatarisha amani ya nchi yetu. Katika hili, nataka kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba, tumekuwa tukichukua hatua; kwa mfano, ilipothibitika kwamba, Vituo vya Redio Imani ya Morogoro, Kwa Neema na Gazeti la Mwanahalisi, vilitoa habari ambazo zingeweza kuhatarisha amani, tulichukua hatua za kuvifungia na hatimaye kuhakikisha wanarejea katika hali ambayo Serikali inataka.

La pili, ni kwamba, Serikali imeendelea kufanya kazi kwa karibu sana na hata mchakato wa kupata sheria ya kusimamia vyombo vya habari, tunafanya kazi kwa karibu sana na Vyombo vya *MOAT*, Baraza la Habari na Jukwaa la Wahariri. Lengo ni kuhakikisha tunakuwa na sheria nzuri na tunafanya kazi kwa pamoja ili kulinda amani na utulivu wa nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Swali la nyongeza, tupate kutoka kwa Mwandishi wa Habari, Mheshimiwa Nkamia!

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo tu la nyongeza.

Katika Bunge lililopita, Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, iliahidi kuleta Muswada wa Sheria ya Vyombo vya Habari katika Bunge hili ili kuondoa adha inayowapata Waandishi wa Habari hasa wanaofanya kazi katika Vyombo vya Habari vya Binafsi ambao wanafanya kazi kwenye mazingira magumu; hawana ajira na mara nyingi wamekuwa wakitumiwa

kuilalamikia Serikali wakati wao wenyewe wanaishi katika mazingira magumu sana. Je, ni lini Serikali italeta Muswada huo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juma Nkamia, kama ifuatavyo:-

Kwamba ni lini Serikali italeta Muswada wa Sheria wa Kusimamia Vyombo vya Habari hapa Bungeni; kweli hiyo ndiyo ahadi ya Serikali na ndani ya Serikali tumeshafanya kazi hiyo kubwa, tayari Mwanasheria wa Serikali ameshakamilisha rasimu ya awali na itapelekwa Baraza la Mawaziri na wakati wowote tukipangiwa, tutawasilisha Sheria hiyo hapa Bungeni.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru. Bado tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, swali la Mheshimiwa Vincent Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa niaba ya Watanzania wote wanaochukia kulazimishwa na Mbio za Mwenge, naomba swali langu lipatiwe majibu.

**NAIBU SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Amos Makalla, Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo!

Na. 45

## Bajeti na Faida ya Mbio za Mwenge Nchini

**MHE. VINCENT J. NYERERE** aliuliza:-

Falsafa ya Mbio za Mwenge ilikuwa ni kuwamulika wahujumu uchumi na wala rushwa Serikalini na hivi sasa rushwa na ufisadi vimekithiri sana licha ya Mbio za Mwenge kuendelea:-

(a) Je, nini faida ya Mbio za Mwenge kwa sasa?

(b) Je, Bajeti ya Mbio za Mwenge kwa mwaka ni kiasi gani?

(c) Je, matumizi ya fedha za Mbio za Mwenge hufanyiwa ukaguzi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, faida zinazopatikana kutokana na Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa sasa ni kama ifuatavyo:-

(i) Mbio za Mwenge wa Uhuru zilianzishwa kwa falsafa ya kuhamasisha Ukombozi wa Taifa na Bara zima la Afrika kama alivyosema Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alipowasha Mwenge wa Uhuru kwa mara ya kwanza na nukuu: "Sisi tunataka kuwasha Mwenge na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro, umulike ndani na nje ya mipaka yetu, ulete tumaini pale ambapo hakuna matumaini, upendo pale ambapo pamejaa chuki na heshima pale palipo na dharau." *(Makofi)*

(ii) Mwenge wa Uhuru umeendelea kuwa tunu ya Taifa letu na chombo pekee nchini kinachohamasisha na kuhimiza mshikamano, umoja wa kitaifa, uzalendo, uadilifu, kukuza moyo wa kujitolea na kuendelea kuenzi Uhuru wetu na kuhimiza harakati za ukombozi wa Bara la Afrika. *(Makofi)*

(iii) Mbio za Mwenge wa Uhuru zimeendelea kuwahamasisha Wananchi nchini kubuni, kuchangia na kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kwa mfano, mwaka 2012/2013 jumla ya Miradi ya maendeleo 273, yenye thamani ya Sh. 158,833,117,855/= ilizinduliwa na mingine kuwekwa jiwe la msingi nchini kote. Aidha, kupitia mbio hizo, Wananchi walichangia kwa hiari. Narudia; walichangia kwa hiari Sh. 11,500,846,850/= kwa ajili ya kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya zao.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara yangu imetenga shilingi milioni 450 kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, kwa ajili ya shughuli za Mwenge wa Uhuru. Fedha hizi hutumika kugharimia gharama za kuchapisha ujumbe wa Mwenge na mafunzo ya Wakimbiza Mwenge

Kitaifa, posho za Wakimbiza Mwenge, gharama za matangazo, wiki ya vijana na ushiriki wa Wizara katika Sherehe za Uzinduzi na Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya fedha za mbio za Mwenge wa Uhuru hufuata utaratibu wa matumizi ya fedha za Serikali zinazopitishwa na Bunge lako Tukufu na hukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG).*

*(Hapa Wabunge wengi walisimama kutaka kuuliza maswali ya nyongeza)*

**NAIBU SPIKA:** Duh, hii ni hatari kubwa! Mheshimiwa Vincent Nyerere, swali la nyongeza! *(Kicheko)*

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

(i) Hivi karibuni Mbio za Mwenge zilipopita Musoma Mjini walilazimisha kuchukua magari ya Halmashauri yakiwemo magari ya wagonjwa na huduma zikasimama, wakaeneza chuki badala ya upendo kama alivyosema Naibu Waziri. Naibu Meya alipojaribu kuzuia, aliitwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama na kupewa vitisho, ukawa Mwenge umeeneza chuki. Nini kauli ya Serikali?

(ii) Kwa kuwa Wananchi wa Musoma Mjini hawapendi kulazimishwa kuchanga fedha kwenye Mbio za Mwenge na wameniambia mwaka kesho hawatachanga.

Je, Serikali haioni busara sasa kukimbiza Mwenge katika maeneo ya watu ambao wako kuchanga na wakaacha Musoma Mjini kwa sababu hawatachanga? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Vincent Nyerere, kama ifuatavyo:-

Kwanza, Wizara yangu haijapata taarifa katika Wilaya ya Musoma Mjini, kama hayo mambo yalitokea. Nataka niseme kwamba, utaratibu upo katika Wilaya, lakini sisi tumelipokea tutalifanyia kazi jambo hilo.

La pili, ningefurahi sana, kwa sababu Mheshimiwa Vincent ni sehemu ya familia ya Mwalimu ambaye ndiyo alikuwa na falsafa hii, angeendelea kuuenzi Mwenge huu na angekuwa kinara wa kuhamasisha. Sisi tunasema kwamba, tutaendelea kuenzi kauli ya Baba wa Taifa na Mwenge utaendelea kukimbizwa nchi nzima na Wananchi ambao wako tayari, waendelee kuchangia na michango hii ni ya hiari siyo ya lazima na ni kwa maendeleo ya Wilaya zao. *(Makofi)*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza kuhusiana na Mwenge wa Uhuru. Muktadha wa kuanzisha Mbio za Mwenge wa Uhuru maana yake ilikuwa ni kujenga uzalendo, kumulika wezi, mafisadi, wala rushwa na kujenga moyo wa kujitolea kwa Wananchi.

Sasa kwa miaka ya karibuni na wakati tunafahamu kwamba, kila mwaka Mwenge unakimbizwa, yametokea matukio mabaya kama ya wizi wa pesa, *EPA,* matukio ya *RICHMOND*, ujangiri, wizi wa Meno ya Tembo, rushwa, ufisadi, uchakachuzi wa pesa za miradi ya maendeleo, madawa ya kulevya na mambo mengine. Sasa, ningependa kujua, kwa sababu kila mwaka Mwenge wa Uhuru unakimbizwa; hivi wakati haya matukio yanatokea Mwenge ulikuwa unamulika wapi haukuwepo ili uweze kuyaona haya matukio? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nassari kama ifuatavyo:-

Kwanza, aliwahi kusema kwamba, Mwenge ukafungiwe na usije huku Arumeru. Nashukuru kwamba, Mwenge unaendelea kukimbizwa na utafika Arumeru. Nataka niseme kwamba, matukio haya yanaendelea lakini angekuwa mfuatiliaji, kila mara Mwenge una kaulimbiu yake na kaulimbiu ipo ya kupiga vita madawa ya kulevya, kukomesha rushwa na haya yamekuwa yakienezwa. Sisi wote ni Watanzania na matukio haya yanafanywa na Watanzania, tushirikiane kwa pamoja kutokomeza haya yote ambayo ameyasema. *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Waziri haoni kwamba, Serikali inapata gharama kubwa kwa kila Wilaya kwa Viongozi wa Wilaya

nzima siku Mwenge unapokuja na siku unapoondoka, hufunga maofisi kwa siku mbili na wanalala siku ya siku tatu baada ya kukesha kwenye Mwenge kwa gharama kubwa. Serikali inasimamisha kazi kila Wilaya kwa siku tatu; hawaoni kwamba wanaingizia Serikali gharama; nchi maskini kama hii na faida za Mwenge zimepitwa na wakati? ... *(Hapa mic ilizimika)* *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Nilifikiri napata nafuu kumbe ndiyo ...! Mheshimiwa Makalla, majibu! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Keissy, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye pasipo mashaka yoyote kwamba, shughuli za Mwenge zinapoingia, basi wakati mwingine husababisha ratiba za shughuli zingine kuathirika. Pamoja na hilo, faida zinazotokana na Mwenge ni kubwa zaidi kuliko shughuli ambazo zinaweza zikasimama na kwa maana hiyo, Serikali inaona faida kubwa na Miradi mingi inayozinduliwa ni kwa manufaa ya Wananchi na Serikali itaendelea na utaratibu huu wa kukimbiza Mwenge nchi nzima ili Wananchi waendelee kujiletea maendeleo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Makalla, kwa majibu mazuri sana. Majibu ya nyongeza toka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuchika!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, kwanza, napenda nimpongeze Naibu Waziri, kwa majibu mazuri sana aliyoyatoa. Muda wetu ni mdogo, nisingependa kutoa historia ya Mbio za Mwenge jinsi ulivyoanza, maneno ya Baba wa Taifa; sisi watu wa Tanganyika tunapenda kuwasha Mwenge na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro, ufanye yale mambo yaliyoelezwa. *(Makofi)*

Umekimbizwa ndani ya usimamizi wa Chama, lakini baada ya kuingia Mfumo wa Vyama Vingi na kwa kutambua kwamba, shughuli za Mbio za Mwenge zinanufaisha Watanzania wote, shughuli za Mwenge tukazihamisha kutoka kwenye Chama zikaenda Serikalini. Mimi nataka niseme kwa ufahari kabisa, kama kuna chombo kinatoa elimu kwa Watanzania nchi hii hakuna kama Mwenge kwa sababu Mwenge wa Uhuru unapita kila Wilaya kuelimisha habari ya madawa ya kulevya, kuelimisha Magonjwa ya UKIMWI ...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizomea)*

**MBUNGE FULANI:** Unaeneza UKIMWI!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Lakini pia kuzindua Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Kwa hiyo, nataka nimalizie kwa kusema kwamba, hoja kwamba Watanzania wanauchukia Mwenge wa Uhuru, hoja hiyo haina ukweli wowote. Nilikuwa natoa darasa, kwa hiyo, wale wanaozomea ni tabia yao acha waendelee, lakini Watanzania wanaopenda Mwenge wananisikia huko vijijini.

**NAIBU SPIKA:** *Order, order.* Wizara ya Maji, swali linalofuata.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Nataka nimalizie kwa kusema kwamba, Mbio za Mwenge zitaendelea kama kawaida.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jenista Mhagama!

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

Na. 46

**Tatizo la Maji Peramiho**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Katika bajeti ya mwaka 2013/2014, Bunge liliidhinisha nyongeza ya Tsh.184.5 bilioni kwa ajili ya Miradi ya Maji hasa Vijijini:-

(a) Je, ni kiasi gani kimepelekwa katika Jimbo la Peramiho ukiacha fedha zilizopelekwa katika bajeti zilizopita?

(b) Je, ni Miradi mingapi katika Jimbo la Peramiho itafikiwa na fedha hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Miradi ya Maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea katika Vijiji vya Lilondo, Maposeni, Maweso, Masigira, Liweta, Mkongotema, Magingo, Liula, Likuyufusi, Morogoro, Muungano - Zomba, Lugagara, Lundusi, Peramiho A na Peramiho 'B'.

Ujenzi wa miundombinu ya maji unaendelea katika Vijiji vya Masigira na Liweta, ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2013 na katika Vijiji vya Mkongotema na Madingo unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2013. Tathmini kwa ajili ya kupata mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya maji imefanyika katika Kijiji cha Maweso. Zabuni ya kupata wakandarasi wa ujenzi wa miundombini ya maji, zimetangazwa kwa Vijiji vya Lilondo, Liula, Likuyufusi, Lugagara, Muungano - Zomba, Maposeni, Morogoro, Lundusi, Peramiho A na Peramiho 'B'.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Songea katika mwaka 2013/2014, imetengewa kiasi cha shilingi 589,642,150 kupitia Mfuko wa Pamoja *(Basket Fund).* Sambamba na fedha hizo, kiasi cha Sh. 364,322,621/= kimetengwa, ikiwa ni mgao baada ya ongezeko la fedha za ndani kiasi cha shilingi bilioni 184.5 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maji Vijijini.

Vijiji vyote vinavyotekeleza Miradi kupitia Programu hii, vipo katika Jimbo la Peramiho lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea. Hivyo, fedha zilizotengwa kupitia Mfuko wa Pamoja na za nyongeza, zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa Miradi ya Maweso, Liula, Likuyufusi, Lilondo na Mradi wa Luyelela, unaojumuisha Vijiji vya Lugagara, Muungano -

Zomba, Maposeni, Morogoro, Lundusi, Peramiho A na Peramiho B.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili makubwa sana ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Kijiji cha Likuyufusi na Kijiji cha Masigira, vijiji hivi viwili viko Manispaa ya Songea na haviko katika Halmashauri ya Wilaya kwa maana ya Jimbo la Peramiho na viko katika Jimbo la Songea Mjini. Je, Serikali sasa iko tayari kuviondoa vijiji hivyo viwili ambavyo vinapoteza nafasi ya Vijiji vya Peramiho katika Mradi na badala yake kuviingiza Vijiji vya Parangu na Vijiji vya Mpandangindo na Kata ya Mtyangimbole ili kuhakikisha nafasi hizo za Vijiji vya Jimbo la Peramiho vinaendelea kupata nafasi sawa katika mgao huu wa fedha za maji?

(ii) Kwa kuwa Wananchi ninaowawakilisha na niliowaombea maji kwa muda mrefu wa Vijiji vya Lugagara, Muungano - Zomba, Maposeni, Morogoro, Lundusi, Peramiho A, Peramiho 'B', Maweso na Liula, wanayo heshima na furaha kubwa kwa kuona Serikali yao sikivu imeongeza bajeti kubwa ya maji na sasa wanakwenda kupata maji. Je, Mheshimiwa Waziri mwenyewe yuko tayari sasa kuambatana na mimi kwenda kupokea shukrani za Wananchi wa Jimbo la Peramiho kwa niaba ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutatua tatizo hili kubwa la maji?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nijibu maswali mawili

ya nyongeza ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho.

Kwanza, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa jibu zuri sana. Napenda pia nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kufuatilia kwa makini utekelezaji wa Miradi ya Maji katika Jimbo lake hapa Bungeni na kule Wizarani na usimamizi mzuri wa ujenzi wa Miradi ya Maji katika Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea mabadiliko aliyoyapendekeza na sisi Serikali hatuna tatizo na jambo hilo. Kupitia Bunge lako, ninamwagiza Mhandisi wa Maji kule Peramiho, atayarishe Vijiji hivyo vya Parangu na Mtangimbole ili viweze kutekelezwa katika kipindi cha pili cha Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niko tayari kutembelea Jimbo la Peramiho na kufuatana na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kuhamasisha utekelezaji wa Miradi hii na kufungua ile ambayo iko tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, nianze kuishukuru Wizara ya Maji kwa kazi nzuri wanayofanya, Mungu awabariki sana. Pia, namshukuru Mheshimiwa Sabodo, kwa kutuchimbia visima kule kwenye Jimbo langu.

Mwaka 2012, Wizara ya Maji ilinitengea shilingi milioni 60 ili kumalizia Mradi wa Maji kule Bungu kutoka Sakale, hadi

leo hii Wizara imetoa shilingi milioni 20 tu. Je, shilingi milioni 40 zilizobakia zitatolewa lini ili Mradi ukamilike? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ngonyani, kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda kumshukuru sana kwa kuendelea kukumbusha ndani ya Bunge na nje ya Bunge; ni kweli Serikali iliahidi kutoa shilingi milioni 60 kwa ajili ya Mradi wa Bungu na tumeshatoa shilingi milioni 20. Nataka nimhakikishie kuwa, shilingi milioni 40 zilizobaki tutazitoa ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Miradi ya Maji katika sehemu tulizoahidi. Tuna ziara kule kwenye vile visima mjini na zitatekelezwa ili Wananchi wapate maji.

Na. 47

**Hitaji la Chuo cha Ufundi Rukwa**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Mkoa wa Rukwa hauna Chuo cha Ufundi hata kimoja:-

Je, ni lini Serikali itajenga Vyuo hivyo kila Wilaya katika Mkoa wa Rukwa kama lilivyo lengo la Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla Mikoa ya Rukwa na Katavi kugawanywa, Chuo cha *VETA* cha Mpanda kilikuwa katika Mkoa wa Rukwa. Hivi sasa Chuo hicho kipo katika Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Mikoa, Serikali inafanya majadiliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(African Development Bank - AFDB),* kuangalia uwezekano wa kupata mkopo nafuu wa kiasi cha Dola za Kimarekani shilingi milioni 57, ambazo pamoja na shughuli nyingine, zitatumika pia katika ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Mikoa ya Geita, ambayo ni Mikoa mipya, Simiyu, Njombe na Rukwa, ambayo haina Vyuo vya Mikoa kabisa. Aidha, katika Bajeti ya Maendeleo 2013/2014, Serikali imetenga fedha za nje kiasi cha Shilingi bilioni kumi kwa shughuli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa Vyuo vya Wilaya, napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wilaya yake ya Nkasi na Sumbawanga Vijijini, ziko kwenye awamu ya pili ya ujenzi wa Vyuo vya Wilaya ambao unahusisha Wilaya 16 nchini. Ujenzi wa awamu ya pili utafanyika baada ya ujenzi wa awamu ya kwanza kukamilika kutegemeana na upatikanaji wa fedha. Aidha, Wilaya hizo zina vyuo binafsi ambavyo vinatoa mafunzo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa, katika kuona umuhimu wa kutoa elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi, mwezi Januari, 2013, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Chala kilichoko katika Wilaya ya Nkasi, kimeanza kutoa mafunzo kwa wanachuo 50 katika fani ya useremala na ujenzi, sanjari na mafunzo ya maendeleo ya jamii, chini ya usimamizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kama Serikali ilivyoahidi kuvitumia baadhi ya Vyuo hivyo vya Maendeleo ya Wananchi kutoa mafunzo ya ufundi stadi.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninalo swali moja dogo la nyongeza.

Pamoja na uchambuzi wa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri, nilichobaini mimi ni ukosefu wa fedha, ambao utatuzi wake unategemea ufadhili, jambo ambalo hatuna uhakika sana na upatikanaji wa hizo fedha. Ili Vijana wa Mkoa wa Rukwa wapate mafunzo ya ufundi kwa haraka kwa nini tusitumie majengo yaliyojengwa na wakandarasi wa barabara katika kambi zao pindi mradi ule utakapokuwa umekamilika, ambayo yapo katika Kijiji cha Mparamawe kule Nkasi Kaskazini, katika Kijiji cha Kianda Sumbawanga Vijijini, katika Kijiji cha Matai, Makao Makuu ya Wilaya ya Kalambo, katika Mji wa Sumbawanga Kijiji cha Kanondo na maeneo mengine katika Mikoa mingine? Je, kwa nini majengo hayo yasitumike ili kuharakisha zoezi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Ignas Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mbunge, kwa kutuambia kuna majengo ambayo wakandarasi baada ya kumaliza kazi ya ujenzi wa barabara ya lami kutoka Tunduma kwenda Mikoa ya Rukwa na Katavi, kwamba, wapo. Kama Mkoa kwa kutumia *RCC* ya Mkoa, watakubaliana na hao wanaojenga barabara kwamba wanaweza wakakabidhi Mkoa na Mkoa wakakabidhi Wizara ya Elimu kwa Mamlaka ya *VETA,* sisi tuko tayari kutumia majengo hayo, ndiyo maana nakushukuru sana kwa kunipa uwazi huo.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, fanyeni hizo juhudi mtuandikie andiko pale Wizarani, sisi tuko tayari kabisa kuanza kutafuta karakana na kuweka Chuo cha Ufundi Stadi *(VETA)* katika maeneo hayo.

Na. 48

**Kuajiri Wataalam wa Nje Kwenye Vyuo Nchini**

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA (K.n.y. MHE. SARA M. ALLY)** aliuliza:-

Gharama za kuwasomesha wanafunzi vyuo vya nje ni kubwa sana ukilinganisha na vyuo vya ndani. Je, kwa nini Serikali isianzishe utaratibu wa kuajiri kwenye vyuo vyetu Wataalam kutoka nje ya nchi ili wanafunzi wengi wafaidike na utaalam huo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, gharama za kuwasomesha wanafunzi Vyuo Vikuu vya nje ni kubwa sana ukilinganisha na vyuo vya ndani. Kwa mfano, mwanafunzi wa Udaktari anayesoma katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili *(MUHAS),* analipiwa kiasi cha Sh. 2,959,545/= kwa mwaka kwa ajili ya ada, vitabu, chakula, malazi, mafunzo kwa vitendo na mahitaji mengine ya Kitivo, wakati mwanafunzi anayesoma nchini Cuba kwa kozi hiyo hiyo hulipiwa jumla ya *USD* 8,364 ambazo ni sawa na Sh. 13,800,000/= kwa mwaka; ambapo Sh. 8,910,000/= ni kwa ajili ya matumizi binafsi na shilingi 4,950,000 ni kwa ajili ya nauli ya kwenda na kurudi mwanzo na mwisho wa masomo.

Vilevile Mhadhiri anayesomeshwa nchini Ujerumani kupitia Mpango wa *Deutcher Akademischer Austausch Dienst – DAAD,* kwa Shahada ya Uzamivu *(Ph.D.)* kwenye Elimu, hulipiwa na Serikali *USD* 12,121, sawa na Sh. 20,000,000/= kwa ajili ya chakula, malazi na matumizi binafsi na usafiri tu kwa yeye na familia yake. Aidha, ada na mahitaji mengine hulipwa na Serikali ya Ujerumani kama msaada, wakati Mhadhiri anayesoma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hapa Tanzania katika kozi hiyo hiyo ya

*Ph.D.,* analipiwa kiasi cha Shilingi milioni 15 kwa mwaka kwa ajili ya ada, vitabu, chakula na malazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo Vikuu vya Umma vimekuwa vikiajiri Wahadhiri wa Nje kwa nia ya kukabiliana na uhaba wa Wataalam Wanataaluma na pia kwa ajili ya kubadilishana uzoefu. Aidha, Serikali huwapeleka wanafunzi nje ya nchi kwa masomo ili vijana wetu wapate taaluma ambazo katika vyuo vyetu kozi hizo zinadahili wanafunzi wachache sana. Pia, kwa ajili ya kuwapa fursa ya kupata maarifa, stadi, ujuzi na uzoefu katika mawanda mapana toka nchi nyingine ambazo tuna mikataba nao ya mashirikiano.

Vyuo Vikuu vya Umma nchini vimeajiri Wahadhiri toka nje ya nchi kama ifuatavyo: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeajiri Wahadhiri 15; Chuo Kikuu cha Dodoma 45; Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi Shirikishi Muhimbili wawili; Chuo Kikuu cha Mzumbe saba; Chuo Kikuu cha Ardhi mmoja na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania *(Open University)* wahadhiri sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto ya uhaba ya wanataaluma, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali, ikiwemo kusomesha wanataaluma 80 kila mwaka katika ngazi za Uzamili na Uzamivu, ndani na nje ya nchi, kupitia ruzuku ya Serikali na vilevile kutoa mikopo kwa wanataaluma wanaotaka kujiendeleza kimasomo. Kwa sasa wanataaluma 183 wanasoma kwa kukopeshwa na Bodi ya Mikopo, kusomesha wanataaluma 20 kila mwaka chini ya ufadhili wa Serikali ya Ujerumani na Tanzania na kusomesha

wanataaluma 378 kwa Shahada za Uzamivu na Shahada za Uzamili chini ya Ufadhili wa Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, unaodhaminiwa na Benki ya Dunia - *Science, Technology and Higher Education Project (STHEP).*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi nilizoziainisha, bado kuna changamoto ya Vyuo Vikuu Binafsi ambavyo kutokana na uchanga wao, Vyuo hivyo vinalazimika kuajiri wahadhiri kutoka Vyuo Vikuu vya Umma, hasa wahadhiri wanaostaafu katika kutekeleza majukumu yao ya kitaaluma, kwani kwao ni gharama nafuu kuwatumia Wahadhiri wa ndani kuliko wa kutoka nje ya nchi.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naipongeza sana Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, kwa jitihada kubwa ya mageuzi inayoyafanya katika Sekta hii ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Wizara ya Afya imekuwa ikifanya mageuzi makubwa sana ya kuanzisha vitengo mbalimbali vya tiba, ambavyo nchini kwetu vimekuwa havipatikani kwa muda mrefu. Je, kwa nini Wizara hii isiandae mazingira mwafaka yatakayowezesha wale wataalam ambao tunawapeleka nje ya nchi waweze kupata taaluma hizo hapa hapa nchini kama mageuzi yaliyofanywa na Wizara ya Afya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru kwa kutupa ufahamu huo, kwamba, Wizara ya Afya inaandaa kozi mbalimbali kwa ajili ya kuzianzisha hapa nchini. Naomba tuchukue ushauri huo tukaufanyie kazi tuone kama linawezekana tuweze kuendelea na kozi hizo.

Na. 49

**Ujenzi wa Barabara ya Serengeti – Mto wa Mbu**

**MHE. KAIKA S. TELELE (K.n.y. MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE)** aliuliza:-

Maandalizi ya ujenzi wa barabara ya kutoka Serengeti –Makutano – Natta – Mugumu – Loliondo hadi Mto wa Mbu km 452 yamekamilika:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa fidia wale wote walioguswa na ujenzi wa barabara hiyo kabla ya kuanza kujengwa kama sheria inavyoelekeza?

(b) Je, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa rasmi?

(c) Kama Serikali ilivyoahidi Bungeni kujenga kipande cha km 41 kutoka Mugumu hadi Lango la Fort Ikoma; je, ni lini ujenzi huo utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali lililoulizwa na Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, Mbunge

wa Serengeti, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wanaostahili watalipwa fidia zao kabla mkandarasi hajaanza kazi. Uthamini wa mali umekwishafanyika na uhakiki wa uthamini huo ndiyo unaendelea, ambapo baada ya kukamilisha taratibu hizo, Wananchi wanaostahili kulipwa fidia kwa mujibu wa sheria watalipwa?

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Makutano – Natta, kilometa 50, tayari ameanza maandalizi ya kuanza kazi *(mobilization),* ikiwa ni pamoja na kupeleka mtambo eneo la mradi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeamua kujenga Barabara ya Makutano - Natta - Mgumu na Loliondo - Mto wa Mbu kwa kiwango cha lami. Hivyo, kwa sasa ujenzi wa barabara hii hautahusisha sehemu ya Mugumu - Fort Ikoma, kilometa 46.5. Ujenzi wa sehemu ya Mugumu - Fort Ikoma kwa kiwango cha lami utaingizwa katika mipango ya baadaye ya Serikali.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema sana ya Serikali ya Tanzania ya kuamua kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ili kuwaondolea Wananchi wa maeneo hayo adha ya usafiri:-

(i) Je, Serikali ina taarifa kwamba imeshitakiwa Mahakamani katika Mahakama ya Bunge la Afrika Mashariki kupinga ujenzi wa barabara hii na imefanywa na wanaharakati kutoka Jamhuri ya Kenya?

(ii) Kama hivyo ndivyo, ujenzi wa barabara hii sasa utasimama kwa kipindi chote ambacho kesi ipo Mahakamani? Naomba majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Telele, kama ifuatavyo:-

Kwanza, niseme tu kwamba, Serikali haina taarifa kuhusu kushitakiwa na Mahakama ya Afrika Mashariki. Kama hilo suala lipo, tungekuwa tumeshajulishwa, lakini silifahamu. Kama tumeshitakiwa, sisi tuna mpango wetu wa kujenga, ambao tumeshaamua na kazi hizo tayari tumeshaanza. Sielewi kama inawezekana kuendelea na kazi ambayo tayari tumeshaianza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuvumiliane kwa sababu muda umebaki mdogo sana, ninawaona lakini tuvumiliane. Swali la Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi.

Na. 50

**Kuzipandisha Hadhi Barabara Wilayani Rungwe**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA** aliuliza:-

Barabara za Ndembela, Kagwina, Kapugi, Itete, Kalalo hadi Kyimo na ile ya Kyimbila, Isajilo, Mibula, Bugoba hadi Ushirika ni muhimu sana kwa uchumi wa eneo hilo Wilayani Rungwe na kutokana na bajeti ndogo ya Halmashauri kuwa

mzigo mkubwa katika kuwezesha barabara hizo kupitika nyakati za masika:-

Je, Serikali inasemaje kuhusu kuzipandisha daraja barabara hizo mbili ili zihudumiwe na Mkoa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. David H. Mwakusya, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu na vigezo vinavyotakiwa katika kupanga barabara katika madaraja stahiki, vimeainishwa katika Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na kanuni zake za mwaka 2009. Taratibu hizo ni pamoja na kupitisha maombi hayo kwenye Bodi za Barabara za Mikoa husika. Bodi ya Barabara ya Mkoa ikiridhia kuwa barabara zinazoombewa kupandishwa daraja zinakidhi vigezo vilivyowekwa, itawasilisha maombi hayo Wizara ya Ujenzi kwa hatua zaidi. Hivyo, nashauri maombi hayo yawasilishwe rasmi kwa kuzingata utaratibu uliowekwa kisheria ili yawezwe kufanyiwa kazi na Wizara yangu.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, namshukuru Naibu Waziri, kwa kunipa maelekezo, nitayafanyia kazi. Vilevile ningependa niipongeze Serikali kwa kazi nzuri inayofanya katika ujenzi wa barabara hapa nchini. Mafanikio haya huwezi

kutenganisha na utendaji wa Mheshimiwa Magufuli, ambaye naye nampa hongera ingawa hanisikii sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema kwamba, kwa kumbukumbu zangu, Waziri mwenye dhamana ya barabara hajawahi kutembelea Wilaya ya Rungwe, ambayo ni moja ya sehemu ya kazi yake. Nilitaka kumwuliza Mheshimiwa Magufuli kwamba, atakuwa tayari, siyo lazima aongozane na mimi, lakini aitembelee Wilaya ya Rungwe akaone adha ya barabara kama tunavyolalamika humu ajue nini kinajiri kule? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Prof. Mwakyusa, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nazipokea pongezi ambazo amezitoa kwa kazi ambazo zinaendelea nchi nzima. Kuhusu kutembelea Wilaya ya Rungwe, naomba nimuahidi tu kwamba, Waziri au Naibu Waziri, atatembelea Wilaya hiyo na kuangalia Miradi na namna ya kuboresha barabara zetu.

**NAIBU SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo litaulizwa na Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, kwa niaba yake Mheshimiwa Dokta Haji Mponda.

Na. 51

## Zoezi la Vitambulisho vya Uraia

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA (K.n.y. MHE. ABDUL R. MTEKETA)** aliuliza:-

Tanzania iko katika mchakato wa kutoa vitambulisho kwa raia wake wote na Wilaya ya Kilombero ilichaguliwa kuwa ya kwanza na kuwa mfano kwa Wilaya nyingine zote:-

(a) Je, ni lini vitambulisho hivyo vitagawiwa kwa Wananchi hao?

(b) Pamoja na zoezi hilo kufanikiwa; je, ni kitu gani kimekosekana hadi leo Wananchi kutojua kinachoendelea?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mbunge wa Kilombero lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA),* ina jukumu la kutengeneza mfumo wa utambuzi na usajili wa watu waishio nchini wenye umri wa miaka 18 na kuendelea, kuwapatia Vitambulisho vya Taifa kwa mujibu wa hadhi zao.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ilifanya zoezi la usajili wa jaribio *(Pilot Project),* katika Wilaya ya Kilombero, Mkoani Morogoro, mnamo Mwezi Februari, 2012. Katika zoezi hilo, Wananchi 220,000 walijaza fomu za maombi, ambapo maombi hayo yalifuata utaratibu wa kupitishwa katika Kamati za Ulinzi na

Usalama za Kata ili kuhakiki na kuridhia uraia wa waombaji. Baada ya kuhakiki maombi hayo, yamekwishaingizwa katika mfumo wa kompyuta wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa. Hatua inayofuata ni uchukuaji wa alama za vidole, picha pamoja na saini za kielektroniki *(Biometric)* na hatimaye kutoa Vitambulisho kwa Wananchi hao.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge, ni kweli zoezi hili lilifanikiwa katika hatua za awali. Hata hivyo, zoezi hili limechelewa kutokana na kuchelewa kupata vifaa muhimu kwa ajili ya uchukuaji wa picha na alama za vidole.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kupitia Bunge lako Tukufu, kuwafahamisha Watanzania wote kuwa, lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa, zoezi la utambuzi na usajili wa watu wote wanaoishi nchini na hatimaye kuwapatia Vitambulisho vya Taifa, linakamilika ifikapa mwaka 2015.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa zoezi hili katika Wilaya ya Kilombero lilifanyika kwa njia ya majaribio *(Pilot Testing),* ambapo walikuwa wanajaribu vifaa vya kufanyia kazi, wafanyakazi wenyewe na mfumo mzima wa utendaji wa hiyo kazi. Je, Serikali haioni kwamba siyo sahihi kutumia matokeo haya kuwapa Vitambulisho hivyo muhimu sana kwa Watanzania hawa?

(ii) Kwa kuwa zoezi hili lilifanyika kwa njia ya majaribio na limeacha kuwahusisha watu wengi sana wakiwemo ndugu zangu, wanafamilia yangu, hawakuhesabiwa kabisa, hawakuhusishwa kabisa kuchukuliwa Vitambulisho hivyo. Sasa, je, Serikali hawaoni kwamba ni vyema irudie tena upya zoezi hili ili iwatendee haki Wananchi hawa wa Kilombero ambao wengi wameachwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Haji Mponda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu ya msingi, ni kwamba, kweli Kilombero ilichukuliwa kama *Pilot Project*. Nataka tu nimhakikishie kwamba, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inafanya kazi kwa weledi mkubwa na tutahakikisha kwamba, Watanzania wote wenye sifa ikiwemo hata hao ambao hawajapata nafasi hiyo, basi zoezi hili linafanyika kwa uzuri zaidi na kuhakikisha kwamba, kila Mtanzania anapata kitambulisho. Kasoro alizozitaja kama zipo, Wizara itashughulikia kuzirekebisha.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu lilikuwa hilo namba mbili, kwa sababu Wananchi wa Kilombero walikuwa wanalalamika, wengi hawajaandikishwa na walikuwa hawajapewa Vitambulisho vyenyewe; kwa hiyo, walikuwa na sintofahamu. Ahsante.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa ukiacha miji ya mipakani, hata katika Jiji la Dar es Salaam na miji mingine, kuna wageni wengi sana; na kwa kuwa wako wageni wengi sana ambao wameshajipenyeza Tanzania kwa muda mrefu na wengine hata kumiliki pasipoti na wakati siyo Watanzania:-

Je, Mamlaka hii itatumia kigezo gani ili Vitambulisho vya Taifa wavipate Watanzania halisi na wageni waweze kutambulika wasipate Vitambulisho hivyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba, wapo wahamiaji ndani ya nchi yetu, lakini nataka nimhakikishie tu, zoezi hili linaendeshwa kitaalam zaidi kuona kwamba, linachukua alama kwa usahihi kabisa kupata Vitambulisho vya Watanzania wenye sifa ya kuwa na Vitambulisho hivyo. *NIDA* itahakikisha inazingatia wasiwasi wako kuona kwamba, wageni wasio na sifa hawapati Vitambulisho na Watanzania wanapata Vitambulisho hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Nashukuru tumemaliza *session* ya maswali ya leo asubuhi na nitaomba sana ushirikiano wenu, kwa sababu baada ya muda si mrefu, tutaanza kuishughulikia Sheria ya Umwagiliaji

kwa kupitia Kamati ya Bunge Zima. Nitawaomba sana Waheshimiwa Wabunge muwepo ili tushirikiane katika kuchambua Muswada huo.

Kuhusu wageni waliofika Bungeni ni pamoja na Wanafunzi 100 kutoka Shule ya Sekondari ya Kikuyu Dodoma. Pale mlipo, karibuni sana watoto wetu. Tunafurahi sana mnapokuja kututembelea, pamoja na Walimu pia; karibuni sana Wanafunzi wa Kikuyu.

Tuna Kiongozi wa Watanzania wanaoishi Uingereza (*Diaspora*), Bwana Haruna Mbeyu na wenzake saba, ambao wamekuja kututembelea na kujifunza masuala ya Bunge. Ndugu Haruna na wenzako! Karibuni sana Watanzania mnaoishi kule Uingereza, kwenye Bunge lenu la hapa nyumbani. *(Makofi)*

Wapo Madiwani kumi kutoka Geita Mjini, ambao wamefika Bungeni kwa lengo la kujifunza. Waheshimiwa Madiwani kutoka Geita Mjini, karibuni sana mjifunze. *(Makofi)*

Matangazo mengine ya kazi; Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane Msekwa B, saa saba mchana.

Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane katika Ukumbi Namba 227, Ghorofa ya Pili, saa saba mchana.

Mheshimiwa John P. Lwanji, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa saba mchana katika Ukumbi Namba 231, Ghorofa ya Pili.

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Nimewaona Wabunge wawili; Mheshimiwa Kombo na Mheshimiwa Hamad Rashid.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba mwongozo wako, Kanuni ya 68(7), katika mambo yaliyotokea hivi karibuni juu ya suala la Mwenge.

Mheshimiwa Mkuchika, alipokuwa akielezea, alikuwa anazungumza kwamba, Mwenge ulikuwa umetakiwa utembezwe Tanganyika; lakini sasa unafika mpaka Zanzibar, sijui kwa sababu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Mheshimiwa Mkuchika ametueleza kuwa, Mwenge sasa unaratibiwa na Serikali na kwa sababu unaratibiwa na Serikali na bajeti yake inatoka Serikalini, lakini bado Mwenge unakimbizwa na watu ambao wanatoka katika Vyama vya Siasa. Sasa sijui inakuwaje na umetolewa kwenye siasa! Naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba busara zako na mwongozo wako kwamba, hili suala la Mwenge na muktadha wake mzima, siyo jambo baya ila sasa kumekuwa na malalako na

manung'uniko ya hapa na pale. Kwa kuwa kwa muda mrefu toka Mwenge utembezwe hakujafanywa tathmini ya kina kuona mabaya na mazuri ili uboreshwe uende vizuri zaidi ili muktadha uweze kukamilika.

Je, Kiti chako hakioni ni busara sasa Serikali kwa kushirikina na Kamati Maalum ya Bunge kufanya utafiti wa kina kujua *pros and cons* za Mwenge na kutoa mwongozo mzuri wa utekelezaji wa Sera hii?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimesimama kuomba mwongozo wako kufuatia hoja iliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wawili hapo ya Historia ya Mwenge wa Uhuru, ambayo ni alama muhimu ya Taifa letu, kwa wale wanaojua historia. Mara tu baada ya Uhuru wa Nchi yetu, Mwalimu alieleza kwamba, sisi tunataka kuwasha Mwenge na kuweka juu ya Mlima Kilimanjaro ili ulete tumaini pale ambapo hapana tumaini na heshima pale ambapo hapana heshima na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyuma yako hapo kuna Nembo ya Taifa, kwenye Nembo ya Taifa hapo ya Uhuru na Umoja kama unavyowaona bibi na bwana, pale kuna alama muhimu sana ya Mwenge wa Uhuru, alama muhimu ya Taifa letu. *(Makofi)*

Kwa kuwa imejitokeza kwamba, kuna uelewa mdogo wa Watanzania juu ya historia ya nchi yetu na historia ya ukombozi wa Taifa letu, kwa kiwango kwamba hata baadhi ya Watanzania wengine wameweza kupenya na kuingia Bungeni ilhali hawajui historia ya nchi yao, kana kwamba

wamechupia; je, Kiti chako kitakuwa tayari kutoa elimu kwa wale ambao wana uelewa mdogo juu ya historia ya ukombozi wetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Miongozo ilikuwa ni hiyo mitatu, inatosha kwa leo. Nitatoa nafasi kwa Mheshimiwa Mkuchika tu, pale mahali ambapo ameguswa aweze kufafanua, mengine tutayashughulikia baadaye.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, nitoe ufafanuzi kwa ndugu yangu Mheshimiwa Kombo na kwa wale ambao hamumfahamu vizuri Mheshimiwa Kombo, alipokuwa *Afro Shirazi Party Youth League* na mimi nikiwa *TANU Youth League*, tulikuwa tunakimbiza pamoja Mwenge. Kwa hiyo, haya aliyouliza labda ametaka tu nifafanue ili watu wengine wapate kuelewa. *(Makofi/Kicheko)*

Moja, nataka niseme, mimi nilikuwa namnukuu Mwalimu, maneno yale Mwalimu aliyasema kabla ya Muungano. Kwa hiyo, asingeliweza kusema sisi watu wa Tanzania, alisema sisi watu wa Tanganyika mwaka 1961.

Nini kimetokea baada ya pale? Kilichotokea baada ya pele, mwaka 1964 nchi zetu zikaungana tukawa na Mwenge ambao unakimbizwa na Vijana wa *Afro Shirazi Party Youth League* na wa *TANU Youth League.* Huyo Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, tumekimbiza naye Mwenge. Kwa hiyo, nataka kusema hilo kwamba, nililolisema sijakosea. *(Makofi)*

Jambo la pili, ametaka kujua kwa nini Mwenge sasa wanaoukimbiza wanatoka katika Vyama. Nataka niseme kwamba, hili jambo siyo kweli; tunawapataje wakimbizaji Mwenge, wanapendekezwa na Ofisi za Wakuu wa Mikoa, wanapeleka kwenye Wizara inayohusika wanateuliwa na wanapoteuliwa wala hakuna kadi ya Chama gani, wala Chama gani, wanapendekezwa na Serikali za Mikoa. Kwa hiyo, naomba sote tuungane, ndugu yangu Mheshimiwa Kombo, tuendelee kukimbiza Mwenge, kuelimisha Wananchi kama tulivyokuwa tunafanya wakati wa *TANU* na *Afro Shirazi Party.*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Machali; nini tena rafiki yangu?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 47, niliombe Bunge lako tujadili hoja hii. Kwa kuwa hasa ikizingatiwa kwamba, Mwenge ulikwa unaonekana ni wa Chama kimoja, lakini baada ya kuwa tumeingia kwenye Mfumo wa Vyama Vingi, Mwenge ulionekana sasa umekuja kukabidhiwa Serikalini halafu zile rasilimali kama ofisi na viwanja bado vimeendelea kumilikiwa na chama kimoja.

Sasa kwa sababu ya hii *contradiction* na hasa tukiheshimu mawazo ambayo yametolewa na Mheshimiwa Hamad Rashid, naomba kutoa hoja yangu ili tuahirishe shughuli za Bunge zilizoko mbele yetu na tuweze kujadili suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. Waheshimiwa Wabunge, naomba mniunge mkono. (*Kicheko*)

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Jambo hilo tutalitazama kwa uzito wake wakati mwingine. Katibu tunaendelea!

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji wa Mwaka 2013 *(The National Irrigation Bill, 2013)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa Sheria ya Umwagiliaji kutaweka msukumo na mazingira ya kilimo cha umwagiliaji kuwa mazuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada umeeleza mambo mengi, lakini nafikiri suala la kutunza na kuvuna maji ya mvua katika mabwawa lingezingatiwa. Mvua zinaponyesha kwa wingi maji yanapotea wakati yangeweza kutumika kwa ajili ya umwagiliaji. Ni dhahiri mito mingi inakauka wakati wa kiangazi ingawa mvua inaweza ikawa imenyesha sana kwa mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Sheria hii pia iangalie namna ya kujenga mabwawa makubwa katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kukusanya maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa jitihada zake za makusudi katika Sekta hii ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda kuongelea suala moja tu la Kilimo cha Zabibu Mkoa wa Dodoma. Dodoma ni mahala pekee ambapo panaweza kuokoa Taifa letu na kuagizwa kinywaji cha *Wine.* Siyo hilo tu, Dodoma ndipo hapo hapo panapoweza kutupatia fedha za kigeni kutokana na kinywaji cha *wine*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji *(drip irrigation),* kinazalisha zabibu bora. Namsihi Mheshimiwa Waziri asimame imara (Serikali), kufanya maamuzi ya makusudi ya kuiangalia miundombinu ya umwagiliaji wa Kilimo cha Zabibu Dodoma. Nitoe masikitiko yangu, kwani Serikali haijaonesha kujali Zao la Kilimo cha Zabibu Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake, azungumzie miundombinu ya kilimo cha zabibu Dodoma. Wizara yake itasaidia vipi Taifa hili nikimaanisha kuboresha miundombinu katika kilimo cha zabibu Dodoma.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema, naunga mkono hoja.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Naipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada wa Sheria ya Umwagiliaji. Sheria hii itasaidia wakulima wetu, Watanzania wanategemea kilimo cha mvua, tukizingatia mvua hunyesha mara moja kwa mwaka ambapo kilimo cha mahindi hutegemea sana maji ya mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mabwawa mengi, mito mingi na maziwa makubwa. Hii itakuwa ni ukombozi mkubwa kwa Watanzania. Neno tuna uhaba wa chakula ni aibu kwa Taifa letu, kwa sababu kila kitu tunacho, kinachotakiwa ni ubunifu katika Sekta hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba, tuwe na *center* za kutolea semina kwa wakulima wetu katika masomo ya umwagiliaji. Pili, Madiwani waelimishwe mradi au mpango mzima wa umwagiliaji. Tatu, Wabunge wote tuungane na kushirikiana na Serikali ili kuhakikisha Kilimo cha Umwagiliaji kinawakomboa wakulima wetu. Nne, Mipango ya umwagiliaji iwekwe kwenye mpango mzima wa Kitaifa na Bajeti ya Kilimo iongezwe kwa kila mwaka wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono Muswada huu ambao kwa kiasi kikubwa, umelenga namna ya kuendeleza kilimo chetu kupitia umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni nchi yetu imekumbwa na tatizo kubwa la kutokuwa na mvua za kuaminika za vuli na masika. Hali hii inatokana na mabadiliko ya hali ya hewa duniani. Kutokana na mabadiliko hayo, nchi yetu imekuwa ikikumbwa na balaa la njaa mara kwa mara katika baadhi ya Mikoa, Wilaya, Kata au Vijiji vyetu. Hali hii imesababisha Taifa kutafuta chakula kwa waathirika hao nje ya nchi yetu. Kuanzishwa kwa Sheria hii inayotaka kuwepo au kuundwa Tume iakayosimamia suala la umwagiliaji hapa nchini, itasaidia sana kuimarisha hali ya chakula nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuanzishwa kwa Tume hiyo, kuna mambo ya msingi ambayo yanatakiwa kusimamiwa ipasavyo ili kuhakikisha umwagiliaji unafanyika. Miongoni mwa mambo hayo ni kuwepo kwa mkakati imara wa kuhifadhi vyanzo vya maji. Hivi sasa maeneo mengi ambayo yalikuwa vyanzo vya umwagiliaji yamekauka; mfano, katika Bonde la Mto Rufiji na hasa maeneo yaliyo ndani ya Wilaya ya Rufiji, vyanzo vingi vya maji vimekauka. Hali hii imesababishwa na uingizaji mkubwa wa mifugo (ng'ombe), hapo mwaka 2007 na kukausha mabwawa makubwa manane, yaliyokuwa na uwezo wa kuhifadhi mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, uharibifu huo wa vyanzo vya maji katika Bonde hili la Mto Rufiji sasa umeingia kwenye Mto Rufiji wenyewe. Makundi makubwa ya ng'ombe yapo kandokando ya Mto Rufiji na kunywa maji ndani ya Mto huu. Hali hiyo imesababisha kina cha maji katika Mto huo kupungua sana na sehemu nyingine

kukauka kabisa. Ni vizuri Serikali ikaingilia kati kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, kuondoa mifugo hii ili ile ardhi chepechepe ndani ya Bonde hili irudi katika hali yake ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu iliyoanzishwa miaka ya nyuma. Mara baada ya kupitishwa Sheria hii, ni vizuri kwa Tume kukagua Miradi yote ya Umwagiliaji iliyopo kabla ya kuanzisha Miradi mipya. Hivi sasa hasa katika Wilaya ya Rufiji, kuna Miradi mikubwa miwili ya Nyamweke, ambayo imegharimu zaidi ya Shilingi bilioni moja na bado haujakamilika kwa sasa umesimama na Mradi wa Segeni – Ikwiriri pia umesimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuiomba Tume mara baada ya kuanzishwa, kubaini maeneo mapya ya umwagiliaji kwa kushirikiana na Wananchi wenyeji wa maeneo hayo. Jimbo la Kibiti ambalo lina mabonde makubwa sana, hadi sasa halina hata shamba moja la umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni Wataalam wa Umwagiliaji. Uanzishwaji wa Tume hii uende sambamba na kuandaa Wataalam ambao watasimamia umwagiliaji katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Umwagiliaji ni kukuza kilimo kwa kujitosheleza kwa chakula. Nchi yetu inavyo vyanzo vingi

vya maji ambavyo vinaweza kuelekezwa kwenye umwagiliaji. Hivi sasa uzalishaji mwingi wa kilimo unategemea mvua. Serikali kwa kuja na Sheria hii, mimi naiunga mkono na kwa maana hiyo, Serikali itatenga ardhi ya kutosha kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali isimamie vizuri Sheria hii ili kuweza kuzuia migogoro yoyote isitokee. Migogoro hiyo hutokea wakati wakulima wanapoona mashamba yao yanavamiwa na wafugaji, kwa sababu ardhi imekuwa chanzo cha msuguano. Serikali ina kazi kubwa ya kuleta jamii pamoja ili waweze kushirikiana vizuri katika hatua zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema kwamba, naunga mkono kuwepo kwa Sheria hii na Serikali iharakishe ili iweze kufanya kazi.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu nami naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, tunatakiwa tutatue tatizo la uharibifu wa mazingira ambalo linaonekana halijasimamiwa vizuri na hasa katika ngazi za chini kama Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yote yanayofaa katika umwagiliaji yaainishwe kwa kutaja maeneo yaliyopo, kwa kutaja Mikoa, Wilaya, Kata hadi Vijiji, kwa kuyalinda kwa mujibu wa Sheria na kuyatambua kwa kujua umiliki wake ili kuzuia kupora kwa maeneo hayo. Serikali ihakikishe

inajitosheleza katika suala zima la wataalam ili kuhakikisha wanatosheleza hadi kufikia ngazi za vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matatizo makubwa ya fedha kiasi kwamba, Serikali imeshindwa kumalizia au kuendeleza Miradi ambayo tayari ilikwishaainishwa. Je, fedha za kukabiliana na Mfuko huu zitapatikana kutoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pembejeo kama mbolea, mbegu na madawa, hadi sasa Serikali imeshindwa kabisa kukidhi utoshelezi katika mfumo wa pembejeo. Tutafute mbinu za kukidhi hili la pembejeo, tukifaulu ndipo tuendelee na mifumo mingine, kwani bado tuna tatizo kubwa na suala hili bado halijaleta tija kabisa. Nashauri tupambane na hili kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatakiwa, kwanza, ijishughulishe na utoaji wa elimu kwa jamii kutambua dhana nzima ya umwagiliaji kwa kutambua faida na hasara. Katika jambo hili, mara nyingi tunaanzisha mambo mengi ambayo mwisho wake haituletei tija kutokana na uelewa mdogo wa Wananchi wetu. Hivyo, tujikite sana katika kutoa elimu kwa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukihimiza wakulima wetu juu ya kilimo, lakini baada ya mwitikio mzuri wa wakulima wanapoitikia, wanarudishwa nyuma kwa kukosa soko na hatimaye wakulima kupata hasara na kukata tamaa na kubaki maskini. Hivyo, Serikali itatue kwanza shida ya soko la mazao kwa Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo tulilonalo kwa nchi yetu ni usimamizi wa Sheria. Tumekuwa mabingwa wa kutunga sheria, shida ni usimamizi wa sheria; je, katika hili Serikali imajipanga vipi?

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii ni mwafaka na imekuja kwa kuchelewa. Kwa kutambua kuwa kilimo ndiyo mwajiri wa Watanzania zaidi ya asilimia 75 na kuwa kilimo ni mchangiaji mkubwa wa Pato la Taifa, lakini tegemeo kubwa kuingiza fedha za kigeni nchini. Sheria hii iharakishwe pamoja na kanuni zake ili Tanzania iweze kujitegemea kwa chakula na kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Sheria hii ni kukabiliana na changamoto tunazoziona au kupambana nazo katika kilimo cha umwagiliaji. Miradi mingi ya umwagiliaji imekuwa ikisuasua kutokana na kukosa Maafisa Umwagiliaji ambao wako kwenye Kanda na hawatoshi kutoa huduma katika maeneo mengi kila sehemu nchini. Sheria inalenga kuondoa changamoto ya ukosefu wa wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, rasilimali fedha imekuwa changamoto kubwa katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Nchi kama China, Malaysia; zimepiga hatua kubwa katika kilimo kwa matumizi bora ya kilimo hiki. Dunia ya leo inatambua kilimo cha uhakika ni kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji kinahitaji vyanzo vya maji na mabonde yenye rutuba. Maeneo haya yabainishwe kwa lengo halisi la uendelezaji azma hii na siyo kitapeli tapeli katika uwekezaji wake kama inavyojitokeza

kwenye Miradi ya Kilimo kwa watu waliomilikishwa ardhi kwa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitishwa Sheria hii, natumaini yale maeneo ya umwagiliaji yaliyokwama, yanaweza kuanza kuleta matunda katika maeneo mbalimbali hata kwenye Jimbo langu la Nkasi Kusini, kama vile mabonde yaliyoko Kate, Namansi na Bonde la Lwaufi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha umwagiliaji ni ukombozi wa Watanzania walioko mijini na vijijini. Hata hivyo, kuwepo Sheria na kupitishwa na Bunge ni jambo moja na utekelezaji wa Sheria hii ni jambo lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili mara nyingi linapitisha Sheria, lakini utekelezaji wake hauonekani. Ningelipenda nielewe kama kutakuwa na udhibiti wa kuvuna maji ya mvua yatakayoweza kutumiwa kwa umwagiliaji kwa muda wote, ili Sheria hii ionekane ina meno katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Tanzania tumeshindwa kulinda vyanzo vya maji tulivyonavyo kutokana na sababu zifuatazo:-

Wafugaji wengi wanaathiri maeneo ya vyanzo vya maji, lakini vilevile Wakulima kadiri wanavyolima kwa kuviingia kwenye vyanzo, kunaathiri vyanzo hivyo. Zaidi, suala la ukataji miti inayosaidia uwepo wa vyanzo vya maji,

jambo ambalo linakausha maji na kusababisha uwepo wa jangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu mkubwa juu ya uundwaji wa Tume ya Umwagiliaji wa Maji wa Mikoa na Wilaya ni kukosekana kwa uadilifu wa kuziendeleza kwa kuzipa uwezo Ofisi za Kilimo za Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa Maafisa wa Kilimo wa Wilaya na Mikoa tumeshindwa kuwawezesha kukuza shughuli za kilimo kwa kuwapatia uwezo wa kifedha na uwezo wa usafiri, tutawezaje kuunda Tume nyingine ambazo zitashughulikia umwagiliaji? Hawa ni wa Taasisi gani katika Wizara ya Kilimo na wale ni wa Taasisi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume hii ya Umwagiliaji itapata wapi vitendea kazi na fedha zitatoka wapi na wale Maafisa wa Kilimo wa Wilaya na Mikoa kwa nini tunawadumaza kuwabakisha maofisini, jambo ambalo limeikosesha tija nchini kwa muda mrefu?

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza waandaaji wa Muswada na naipongeza Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ieleweke kabisa kuwa, ukulima bila uwezo wa umwagiliaji ni sawa na utaratibu wa kucheza kamali kwa kuwa mvua hasa nyakati hizi za mabadiliko makubwa katika mwenendo wa hali ya hewa, inaweza isinyeshe inavyotakiwa. Hivyo, ili kuwa na uhakika wa usalama wa chakula, umwagiliaji ni lazima. Kwa hiyo, uundwaji wa Sheria hii ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchakato wote ni muhimu mamlaka juu ya ardhi ambayo wanayo Wananchi kupitia Serikali zao za Vijiji, Kata na Halmashauri zisiondolewe au kupunguzwa, pamoja na mamlaka juu ya vyanzo vyao vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuishauri Serikali kwamba, kuna umuhimu wa *Commission* hii kukaa mahali pamoja na siyo kuhamahama katika Wizara tofauti. Kama ilivyokuwa Idara hii, itasaidia sana ufanisi wa shughuli mbalimbali zinazoratibiwa na Tume hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mahusiano ya Sheria ya Umwagiliaji na Sheria nyingine zinazohusu matumizi ya maji, chini ya Wizara ya Maji ili kuepuka *conflict of laws*. Kama mtu anamiliki kisima kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya maji, lakini atakapotaka kutumia maji hayo kwa ajili ya umwagiliaji, je, ni sheria ipi itatumika? Hivyo kuna haja sheria hizi ziwe *harmonized* katika utekelezaji wake. Pia ni vyema Sheria ya Umwagiliaji iendane na Sheria ya Mazingira kwa kuwa *issue* ya Mazingira ni suala mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ni lazima Muswada huu uweke lengo la kuwafaidisha wakulima wadogo na isiwe ni kwa wawekezaji wakubwa tu, hii haitawatendea haki wakulima wadogo.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Sheria hii; ukombozi mkubwa kuokoa nchi dhidi ya tishio kubwa duniani litokanalo na mabadiliko makubwa ya tabia nchi kilimo chetu ambacho huchangia sehemu kubwa zaidi katika pato la Taifa kitaimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo hicho (cha umwagiliaji) kiwe endelevu na kitoe tija inayotarajiwa na hata zaidi. Yafuatayo yazingatiwe:-

(a) Kasi ya kuzalisha wataalam wazalendo iongezeke.

(b) Miradi inayoendelea itumike kama maeneo ya ufundishaji *(training grounds).*

(c) Wawekezaji walazimishwe kupokea wataalam wanafunzi kwa ajili ya mafunzo *(Technology Transfer).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wahandisi Washauri, Wakandarasi na kadhalika; Sheria iweke wazi kusisitiza juu ya ulazima wa kutumia Wataalam na Makandarasi waliosajiliwa na vyombo husika chini ya Sheria za nchi: Wahandisi - *Engineers Registration Board (ERB),* Wakandarasi - *Contractors Registration Board (CRB)* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitaji hili liwe la lazima kwa vyombo vyote vya nchini na vya nje ya nchi.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na nchi yetu kutegemea kilimo kwa zaidi ya asilimia 70, hivyo kilimo bado ni uti wa mgongo kwa

maendeleo yetu. Kikubwa zaidi nchi yetu kama ilivyo duniani, inakabiliwa na tatizo kubwa sana la mabadiliko ya tabia nchi. Hivyo, ukame umekuwa tishio kubwa sana kwa kilimo chetu. Kilimo cha kutegemea mvua, kimepitwa na wakati na hakina tija tena. Ni kwa mantiki hii, nchi yetu yenye eneo kubwa la umwagiliaji hekta 29.4 milioni, ni muhimu litumike kwa kilimo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ni kwa bahati mbaya sana miundombinu ya umwagiliaji bado ni mibovu sana, kwani maji mengi hususani ya mvua yanapotea bila kuvunwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na eneo kubwa la umwagiliaji la hekta 29.4 milioni, bado ni hekta 450,362 tu zinazomwagiliwa sawa na asilimia 1.5 tu. Hii ni hatari sana kwa mustakabali wa nchi hii. Hivyo, inasikitisha kuona Serikali inazidi kuunda Taasisi ambazo kimsingi zinazidisha matumizi kwa walipa kodi na hivyo utendaji kwa maana ya umwagiliaji unakuwa hafifu. Naomba Wizara (Serikali) itueleze Tume hii itasaidiaje umwagiliaji kama miundombinu hapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba Tume hii ihakikishe kuwa wana wataalam na fedha ili kweli kilimo hicho kifanikiwe, kwani Watanzania zaidi ya asilimia 70 wanategemea kilimo na pia tuna bahati ya kuwa na vyanzo vingi vya maji.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuanzisha Sheria hiyo kwani hali ya tabia nchi imebadilika na sasa kuna

ukame uliokithiri nchini sehemu kubwa ya shughuli za kilimo hutegemea kilimo cha umwagiliaji, kuendeleza kilimo hicho kutapunguza njaa nchini, mvua sasa hazipo umwagiliaji pekee ndiyo njia ya kuendeleza kilimo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa angalizo pia kuwa endapo Sheria hiyo itapita, tunaomba Ofisi za Wataalam wa shughuli za umwagiliaji ziwepo Wilayani ambako kuna watu wanaotegemea kilimo cha umwagiliaji na siyo tu katika Ofisi za Kanda. Pia wasisahau Kanda ya Kusini ambako kuna mabonde mengi, ambako unaweza kutumia kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji lakini hayatumiki ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuunga mkono hoja hii iliyopo mbele yetu. Pia napenda kuipongeza Wizara na Waziri husika kwa kuleta Muswada huu muhimu sana kwa wananchi wa Tanzania na Taifa zima, kuleta matumaini kwa maisha bora kwa kila Mtanzania. Mpango huu ulikuwa umechelewa sana kuletwa Bungeni. Hata hivyo, ni mpango endelevu kwa Taifa, hatujachelewa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, baada ya kuipitisha Sheria hii, isimamiwe vilivyo ili kukidhi malengo na mahitaji kwa wananchi wetu ili kuleta imani kwa uongozi na Viongozi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri wa Kilimo, Watendaji wake na Kamati kwa kuleta wazo na hatimaye Sheria ya Umwagiliaji ya 2013 hapa Bungeni kwa ajili ya kuchangia na hatimaye kuiunga mkono Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii imeletwa Bungeni kwa kuchelewa. Sheria hii ya muhimu, ingekuwa imeletwa hapa mapema ili Wananchi waweze kupata ukombozi kwa kuinua uchumi wao kupitia kilimo ambacho ndiyo uti wa mgongo na ndiyo tegemeo la Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia au kutumia umwagiliaji wa kisasa, uzalishaji wa mazao kama mahindi, ngano, pamba, kahawa, maharage na kadhalika, utaongezeka sana. Tatizo la njaa nchini ambalo limekuwa likijitokeza mara kwa mara kwa baadhi ya mikoa hapa nchini litakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa umezungukwa na vyanzo vya maji mengi ya maziwa na mito mingi kama Ziwa Tanganyika, Ziwa Rukwa, Mito ya Kalambo, Luiche, Lwanji, Kate na mabwawa kama Pwela na kadhalika. Kutokana na vyanzo hivyo, wakulima wangelima kwa mzunguko wote wa mwaka (masika na kiangazi).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo vyanzo nilivyovitaja hapo juu, Wizara ifanye juhudi kuvitumia vyanzo hivyo kwa umwagiliaji wa matone au wa aina yoyote ile ili mradi kiwango cha uzalishaji mazao kiwe bora na

kiongezeke maradufu ili mikoa mingine iweze kunufaika na mazao yauzwe ndani na nje ili wana Rukwa waweze kuinua uchumi wao *(GDP Per Household),* lakini nao waweze kubaki na chakula cha kutosha hata watakapokuwa wameuza mazao yao kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalizo, katika yote Serikali iziachie Halmashauri za Vijiji au Mikutano Mikuu ya Vijiji kuamua juu ya ardhi zao katika kuuza au kukodisha ardhi kwa wawekezaji wa ndani na nje kwa ajili ya Kilimo cha Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai yangu kuwa mpango kabambe huu ambao ni ukombozi wa Watanzania utakapoanza basi Sheria hii isimamiwe ipasavyo. Utekelezaji ufanywe kwa umakini na uadilifu kwa uwajibikaji mkuu ili uweze kuleta matokeo makubwa na ya haraka *(Big Results Now).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Muswada huu wa kuwa na Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri vyombo vitakavyoundwa baada ya kupitishwa kwa Muswada huu muhimu vitambue na vibaini maeneo yanayokabiliwa na ukame mkubwa kama vile Ukanda wa Kati kwa maana ya Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Tabora. Mikoa hii

inahitaji kupelekewa maji ya Ziwa Victoria kama ilivyofanyika kwa Mikoa ya Mwanza na Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka husika ziangalie uwezekano pia wa kujenga mabwawa makubwa ya kuhifadhi maji ya kutosha nyakati za masika kwa ajili ya Kilimo na Mifugo. Maeneo haya ya Ukanda wa Kati hayana mito ya kutosha, ingawa mvua za muda mfupi humwaga na kutawanya maji mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni huo na naomba kuwasilisha.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wengi waishio vijijini na hasa wanaojishughulisha na kilimo, wameshindwa kuendesha shughuli za kilimo chenye tija kutokana na kutegemea mvua za msimu ambazo kwa hivi sasa kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, zimekuwa zikinyesha bila uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Watanzania wengi wanaoishi katika maeneo mazuri ambayo kilimo cha umwagiliaji kingeweza kuwa cha faida kubwa na hivyo kuzalisha zaidi ya wanavyofanya sasa. Serikali ingeweza kupitia Wizara husika kuandaa vibwagizo vya kuelimisha wakulima kwa njia ya *Radio* kwani kwa vyovyote Watanzania au Kaya nyingi zinamiliki *Radio*. Elimu ingetolewa kuhusu kilimo cha umwagiliaji na hivyo wakulima wangeondokana na kilimo cha kusubiri mvua za msimu na hivyo kujikomboa kutokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutunga Sheria peke yake haionekani ni kwa faida ya wakulima wazawa. Sheria hii inaweza kuonekana ni kwa ajili ya kuwavutia na kuwalinda wawekezaji zaidi. Mipango ielekezwe kwa Watanzania zaidi na hasa hii inayohusu ardhi na kilimo. Watanzania wengi wameweza kuendesha vizuri shughuli za kilimo bila hata ya Sheria kuwekwa, cha msingi ni elimu itolewe kuhusu matumizi mazuri ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu inaeleweka kwamba ni jukumu la *Local Government Reform Programme* kuangalia uundwaji wa Idara za Kiutendaji ndani ya Halmashauri zinazosimamiwa na Baraza la Madiwani na siyo kama inavyopendekezwa kwamba liwe jukumu la Waziri wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema katika kuzungumzia kilimo cha umwagiliaji, Serikali ikamwangalia mkulima mdogo atafaidikaje badala ya kumwacha aendelee kuwa maskini na badala yake Sheria inamfikiria mwekezaji tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Christopher Chiza; Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Kighoma Malima; Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa Muswada huu. Ni ukweli usiopingika kuwa Sheria hii itasaidia sana kuongeza uzalishaji kupitia kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawapongeza Wajumbe wa Kamati ya Kilimo chini ya uongozi wa Mheshimiwa Profesa Msolwa, kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuboresha Muswada huu kwa maslahi ya wakulima wa Tanzania. Ni matumaini yangu kwamba, ukipitishwa na Bunge, utafanya kazi nzuri sana ya nchi yetu kuondokana na janga la njaa wakati nchi yetu inapokumbwa na ukame, wakulima watalima kilimo cha umwagiliaji ambacho hakina kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuweka kipaumbele cha Kilimo Kwanza, bado kuna maeneo makubwa ya ardhi ambayo yanahitaji kutumika kwa kilimo hasa cha umwagiliaji. Hivyo, ni imani yangu kuwa tukiridhia Bunge zima kuundwa kwa Tume ya Umwagiliaji, itasaidia sana Tume hii kujikita kwa jukumu moja tu na ufanisi wake utakuwa wa kiwango cha juu. Kwanza Tume hii itaanza na kazi ya kuainisha mabonde yote yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Vile vile baada ya kuainisha utekelezaji wake utakuwa mwepesi na wenye kiwango cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mikoa yenye ukame mfano Singida na Dodoma haitaweza kuondokana na janga la njaa kama hawatajikita kwenye kilimo cha umwagiliaji ambacho kitasaidia kulima wakati wote hata kiangazi, endapo maji ya mvua yatatunzwa kwa kutengeneza mabwawa na skimu za umwagiliaji kwenye mabonde mbalimbali; mfano, Mkoa wa Singida - Tarafa za Nkonko na Kintinku na Tarafa zake. Pia Vijiji vya Kilimatinde, Itigi na Manyoni yenyewe hata Wilaya ya Iramba, Kata za Mtoa, Shelui, Ntwike, Tulia na maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimalizie kwa kuunga mkono kwa asilimia mia moja kuundwa kwa Tume ya Umwagiliaji kupitia Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji wa Mwaka 2013.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii kwani malighafi kuu ya kilimo ni maji na ili maji yatumike vizuri, ni muhimu kuweka miundombinu ya umwagiliaji. Kwa hiyo, Muswada huu una lengo zuri la kuleta tija katika kilimo ambacho kinategemewa na asilimia 75 ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, ninao ushauri ufuatao:-

(a) Ujenzi wa mabwawa. Changamoto kubwa ya Tume ya Umwagiliaji ni kupewa fedha za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na hasa mabwawa ili kukinga *(harvest)* na kuhifadhi maji wakati wa kipindi cha mvua. Hivi sasa maji mengi yanatoroka kwenda baharini. Hivyo, kazi ya ujenzi wa mabwawa makubwa kwa kilimo kikubwa na mabwawa madogo kwa kilimo kidogo cha mboga mboga ni muhimu ikafanyika.

Maeneo ya Mikoa ya Kanda ya Kati yana ardhi nzuri, lakini ni maeneo kame na hivyo hupata shida ya njaa kila mwaka. Kilimo cha umwagiliaji kitaondoa tatizo hili na kuinua uchumi wa wananchi.

(b) Uratibu na ushirikishaji. Ili Tume ya Umwagiliaji itekeleze majukumu yake vizuri ya kuratibu shughuli za

umwagiliaji, ni lazima ipate ushirikiano wa Wizara za Kilimo, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Maji, Wizara ya Fedha na Wizara ya TAMISEMI na ikibidi Wizara hizo zibadilishe Sheria zao ili kuweza kutambua uwepo wa Tume hii na pia sheria hizo ziwezeshe Tume kufanya kazi bila vikwazo. Aidha, Tume lazima iwashirikishe wadau katika kila hatua ya kila mradi. Wadau wa Tume ni wawekezaji na pia wakulima wadogowadogo huko vijijini wapatao asilimia 75 ya Watanzania wote.

(c) Uelimishaji na uhamasihaji. Kwa kuwa lengo la sheria hii na mpango huo wa umwagiliaji, ni kuwakomboa Watanzania kupitia kilimo cha umwagiliaji basi ni muhimu Watanzania waelimishwe na wahamasishwe kuunga mkono.

Napongeza hatua ya sheria hii kutafsiriwa kwa Kiswahili (*good practice)* na hatua hii itasaidia wananchi wengi kuisoma na kuielewa na kushiriki katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema kwamba naunga mkono hoja hii.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Mhandisi Christopher Chiza, Naibu Waziri, Mheshimiwa Adam Malima, Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara wote kwa kuandaa na kuwasilisha Muswada wa Sheria hii muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa dhati hoja hii lakini nashauri yafuatayo:-

(a) Ibara ya 18 irekebishwe ili izingatie mamlaka aliyonayo Waziri wa Ardhi chini ya Sheria ya Ardhi, Na. 4 ya 1999, ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kuwasilisha mapendekezo ya utwaaji ardhi kwa Rais.

(b) Ibara ya 30 (2), nakubali kuwa wakulima wote walio katika eneo la mpango watakiwe kuzingatia kanuni au sheria ndogo. Nashauri kuwa wasilazimike kujiunga na Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji kwani kufanya hivyo ni kukiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977 inayotoa uhuru kwa mtu kujiunga na chama anachopenda.

(c) Ibara ya 35, ufafanuzi utolewe juu ya ardhi itakayogawanywa na Chama cha Umwagiliaji inatoka wapi. Je, chama hicho kinapata wapi mamlaka ya kugawa ardhi nje ya taratibu zilizoelezwa kwenye Sheria za Ardhi Na. 4 na 5 za mwaka 1999?

(d) Ibara ya 40(2), nashauri kuwa jukumu la kukusanya ada za umwagiliaji zifanywe na chombo kimoja, yaani Tume na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kuwa Wakala.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii ili nichangie Muswada huu wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii ni nzuri sana ikiwa itafuatwa na kutekelezwa ipasavyo lakini ninakuwa na wasiwasi kwa sababu Sera ya Kilimo Kwanza tu imeshindwa kutekelezwa ipasavyo na imebakia kuwa kama Wimbo kwa Taifa hili. Mpaka sasa Mikoa mingi ambayo ina sifa ya kuzalisha chakula na kuondoa balaa la njaa lakini ndiyo imekuwa ikikumbwa na njaa. Yote hiyo ni kwa sababu ya kutosimamia ipasavyo kwa sababu mpaka sasa Watanzania wengi bado wanatumia jembe la mkono na ukosefu wa pembejeo. Pia hutolewa kwa ubaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tufanikiwe na ili mradi huu wa umwagiliaji ufanikiwe basi ni vema Sheria hii iboreshwe na kuzingatia kwanza mgawanyo mzuri wa ardhi bila uonevu. Rushwa ipigwe vita katika usimamizi wa mradi huu kulingana na rasilimali watu ambao ni muhimu katika mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii isimamie vilevile makundi ya wafugaji na wakulima ili kila kundi lithamini kundi lingine ili kuondoa migogoro ambayo hutokea ya uharibifu wa miradi ya kundi lingine ili maendeleo yaonekane katika sekta zote. Kundi la wakulima wadogowadogo likithaminiwa basi tunaweza kufika mahali pazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mgawanyo wa ardhi uzingatiwe sana kwa wazawa wote wa nchi hii, tofauti na ilivyo sasa hivi ambapo maeneo mengi mazuri wamepewa wawekezaji na wazawa kunyang'anywa na vijana wengi kukosa kabisa maeneo ya ardhi. Huko ni kukaribisha

umaskini mkubwa. Hivyo sheria hii izingatie sana suala la rasilimali watu kwanza ndio tutafanikiwa na tutaendelea.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kutuletea Muswada huu. Nawapongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kutuletea Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji imekuja kwa wakati mwafaka sana hasa kipindi hiki ambacho kuna mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha ukame. Hivyo, kupitia sheria hii, tutakuwa na nafasi nzuri ya kutekeleza shughuli za umwagiliaji. Naomba kuunga mkono hoja hii ili utekelezaji uanze mara moja kupitia sheria hii. Kanda ya Ziwa kupitia Bonde la Ziwa Victoria, Wananchi wataweza kunufaika na kuwa na kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali kubwa nililokuwa nalo ni juu ya utekelezaji wa sheria hii lakini kupitia Muswada huu, tayari Tume Maalum itaanzishwa kwa ajili ya kusimamia shughuli zote za umwagiliaji. Niiombe Serikali ihakikishe kwamba Tume hii inawezeshwa kifedha ili utekelezaji wa majukumu yake uweze kufanikiwa maana bila fedha, uanzishwaji wa Tume hii itakuwa bure kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine muhimu linalohitajika kuangaliwa ni suala zima la ardhi, nikimaanisha namna ya kupata ardhi kwa ajili ya kutengwa kwa shughuli za umwagiliaji. Lazima suala hili liangaliwe kwa makini sana. Mimi nina uzoefu wa migogoro mingi ya ardhi baina ya wananchi na wawekezaji katika sekta ya madini. Ili

kuepusha migogoro, ni vema kuanzia sasa sheria inapotungwa, tuweke utaratibu mzuri utakaoondoa mianya ya kusababisha migogoro. Ikiwezekana kuwepo na ushirikishwaji wa wananchi wenyewe katika maamuzi juu ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja nikiamini kwamba sheria hii ni mkombozi kwa wananchi walio wengi, maana zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania tunategemea kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naipongeza Serikali pamoja na kuchelewa kwake, kwani Sera ilikuwa mwaka 2009 hadi leo 2013 ndiyo Sheria inakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, rasilimali ambayo mgawanyo wake katika dunia, *earth's water – fresh water 3%,* bahari 97%, *fresh water – ground water 30.1%, ice water 68.7%, fresh surface water – lakes 87%, rivers 2%* na *swamps 11%.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Tume ikaweka bayana maji yatakayotumika ni ya aina gani na yaliyopo wapi, kwani upungufu wa maji duniani ni moja ya changamoto hasa ukitilia maanani juu ya matatizo ya tabia ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa nchi yetu ina rasilimali kubwa ya ardhi, lakini kutokana na maendeleo ya viwanda na ongezeko la watu, ni dhahiri

Muswada ulitakiwa utoe majukumu kwa Tume kuainisha maeneo ya umwagiliaji ambayo yataipa chakula nchi kwa kipindi cha miaka angalau 50 ijayo. Hivyo, siyo suala la kumwagilia kila mahali, bali ni maeneo gani, mazao gani na kwa Mikoa na Wilaya zipi na zizalishe nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Miswada mingi ambayo imepitishwa na Bunge hili hasa inayoanzisha Tume, haielezei *financial implications* katika utekelezaji wa Muswada huu. Hivyo Tume inaweza kuanzishwa lakini utekelezaji wake unakuwa mgumu na mafanikio ni madogo. *Sections* 3 – 6, ni vyema ikaongezwa Wizara ya Nishati na Madini ambayo ina umiliki wa ardhi sehemu kubwa ya nchi, lakini pia ni watumiaji wakubwa wa maji hayo hayo tunayotaka kuyatumia kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejitahidi kuanzisha Taasisi nyingi kwa dhana ya kuboresha na kutoa huduma bora, lakini kwa kuwa Sheria zetu nyingi haziweki muda wa mwombaji wa huduma kupata majibu, inakuwa vigumu kwa uboreshaji wa utoaji huduma. Hivyo, nashauri Tume ipewe muda wa utoaji wa huduma kwa watu wanaohitaji huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *section 13 (4) (a)* hakuna haja ya kuwa na *Regional Irrigation Officer,* ni *misuse of resources.*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeomba kuchangia Muswada huu baada ya kuona kuwa ndugu zetu Wapinzani wanapotosha Watanzania kwa kuchanganya baina ya vitu vitatu:-

(1) Nini maana ya Sheria?

(2) Nini umwagiliaji na manufaa kwa nchi yetu?

(3) Nini maana ya Sheria ya Umwagiliaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachojadili hapa ni Sheria itakayosimamia umwagiliaji ili tuweze kuharakisha mafanikio ya Kilimo cha Umwagiliaji katika nchi yetu. Sheria haina itikadi, ndiyo maana hata Mheshimiwa Mbowe akiandamana kwenye barabara zetu, akikiuka Sheria, anachukuliwa hatua. Akipitiliza Mikutano yake, anachukuliwa hatua, Sheria ni Sheria, hazipaswi kuwa na itikadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, umwagiliaji upo hapa nchini hata sasa. Muswada huu hauendi kuanzisha, bali unakwenda kusimamia vizuri ili kuweza kuwawajibisha watendaji ambao siyo lazima wawe wafuasi wa Chama cha Mapinduzi. Kinachopingwa ni kipi hapa na kwa masilahi ya nani, kama siyo kuwapotosha Watanzania ambao wanatutegemea sote tuwaboreshee maisha na kuwaondolea umaskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoonekana kwenye mawazo ya Wapinzani waliochangia hasa Mheshimiwa Kafulila na Mheshimiwa Mkosamali ni mawazo ya kutapatapa na yame-*paralize* kwa kushindwa kuelewa tofauti ya mambo matatu niliyotaja hapo juu. Tusiwapotoshe Wananchi kwa masilahi binafsi.

Utakapojumuisha Mheshimiwa Waziri, uelezee vizuri kuwa Serikali yetu haitapitapi kwa kuleta Muswada huu, bali wenyewe ndio wanaopotosha wananchi kwa mawazo yao potofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii nzuri sana kwa asilimia mia moja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana kuja kwa Muswada huu. Naomba kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 17 na 18, vifanyiwe marekebisho kwa kuhusisha maamuzi ya Mikutano ya Vijiji kabla ya kutumia ardhi za Vijiji.

Vile vile nashauri kwamba uteuzi uwe makini bila kuleta upendeleo ili kupata watu wenye uwezo wa kufanya kazi za umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, uteuzi wa Wajumbe wa Tume pia uhusishe angalau Mkulima mmoja wa kawaida wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri, moja kwa moja. Mheshimiwa Malima, yeye ataongea kwa muda wa dakika 30 na baadaye atafuata Mheshimiwa Waziri, kwa muda wa dakika 45. Mheshimiwa Malima, tafadhali!

Waheshimiwa Wabunge, mnaokwenda kwenye Chai na kadhalika naomba msiende mbali mrudi tushirikiane kupitia hii Sheria.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, *Subhanahu Wataala aza wajaa,* kwa kunijalia afya na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge Tukufu, niweze kuchangia katika hoja hii muhimu sana kwa mustakabali wa Taifa letu.

Naomba pia nitumie fursa hii, niwashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kwenye mchakato mzima wa kuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako. Naomba kwa maana hiyo, nimshukuru sana Mheshimiwa Chiza, Waziri wangu wa Kilimo, Chakula na Ushirika; Bi. Sophia Kaduma, Katibu Mkuu wangu, nimpe pongezi kwa kuteuliwa juzi kuthibitishwa katika nafasi hiyo; na Watendaji wangu wote ndani ya Wizara katika ngazi mbalimbali, ambao wamewezesha Muswada huu kuletwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba pia niwashukuru Wabunge wote.

Muswada huu na umuhimu wake kwa nchi hii na namna ambavyo Wabunge wameuchangia, naomba niwashukuru sana kwa maoni yao yote, waliopinga na waliounga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, upana wa umuhimu wa Mradi huu kwa maisha ya Watanzania hauna mjadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tuna Watanzania milioni 47, tunakadiriwa kwamba, kwa utaratibu huu wa uzalishaji tunaweza tukawa na Watanzania milioni 60 ifikapo ndani ya miaka 10 au 12. Kwa hiyo, hasa tukichukulia kwamba, wanasema *most important concerns of our time* ni *water security*, *food and nutrition security* na *energy security.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili sisi tunasema kanzu ya Ijumaa inafuliwa Jumatano, Alhamisi inapigwa pasi, unaweka akiba isije ikanyesha mvua ukakosa kanzu ya kuvaa Ijumaa. Kwa hiyo, shughuli hii tunayoifanya hapa ni kuanza kutengeneza utaratibu na mikakati ya kuangalia namna ambavyo tutajielekeza kwenye usalama wa chakula wa nchi hii.

Tutakapokuwa na Watanzania milioni 60 miaka hiyo kumi ijayo na hatuna namna ya kufanya hivyo isipokuwa kuangalia masuala ya tija kwenye uzalishaji wa chakula. Aidha, hatuna namna ya kufanya hivyo kama hatujielekezi kwenye mfumo wa uzalishaji wa chakula unaozingatia changamoto za siku za sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba michango yote iliyowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge, mimi ninaamini, hata kwa wale waliopinga lakini walilenga kupanua mjadala huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila niseme tu kwamba, kuna *principles of Parliamentary Opposition,* mimi naamini kwamba kwa namna yoyote ile lazima katika masuala kama haya tuwe na *common ground, common interest and common good.* Huu Muswada ni wa *common good.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wale waliosema Muswada huu usiingie Bungeni, urejeshwe. Nachelea kufikiria kwamba inawezekana hata siku moja tutakapokuja kusema kwamba sasa tunaleta Muswada wa kuongeza adhabu kali kwa watu wanaoleta madhara kwa watoto, akinamama na walemavu, mtasema kwa sababu umetoka CCM, tunaukataa. Mimi nadhani *we have principles of Parliamentary common good* ambazo lazima zitawaliwe na *Parliamentary Democracy* na siyo *Parliamentary ludicrous*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo, ninaomba niseme tu kwamba, wakati Mheshimiwa Felix Mkosamali anachangia, nilikumbuka mwaka 1985 nikiwa mwanafunzi wa mwaka wa pili *University of Havana,* tulikuwa tunaanza mjadala huu wa *perestroika* na *glasnost.* Akasimama mwanafunzi mwenzagu mmoja akamkashifu sana Michael Gorbachev. Nimejaribu kukumbuka ile kauli aliyoisema yule Mwalimu wetu aliyekuwa anaitwa Profesa Juan Carlos nadhani Medina, tulikuwa tunamwita Machi, alisema hivi:-

*“El futuro de este pais esta en las manos de ustedes la juventud...no podemos crear la cultura de celebrar lo ridiculo sobre lo estupido...” (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anasema hatma na maisha ya mbele ya nchi hii, yamo mikononi mwenu ninyi vijana. Tusijenge tamaduni ya kushabikia upuuzi na ujinga. Yaani mtu anasema tu jambo lakini kwa sababu mimi, wanasema, *"Juventud communista"*, mimi ni umoja wa vijana wa Chama wa Kikomonisti basi ninasema kwamba huyu Gorbachev, hapana. Anasema ninyi hatima yenu ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa, yamo mikononi mwenu. Tusijenge tabia ya kushabikia mambo ambayo hayana maslahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemwona Mheshimiwa Felix Mkosamali kaondoka lakini nilitaka nimwambie kwamba, kuna kauli moja alitumia ya kumshambulia Waziri wangu Mheshimiwa Chiza, kuhusu ujuzi, uzoefu na uwezo wake lakini ninamwambia hatua utamaduni huo. Wakati Mheshimiwa Felix Mkosamali anazaliwa mwaka 1986, Mheshimiwa Chiza tayari alikuwa *Engineer* wa miaka mingi katika masuala ya umwagiliaji. Kwa hiyo, basi, sitaki kuheshimu ujuzi niheshimu umri tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, Muswada huu unalenga kuboresha usimamizi wa umwagiliaji. Waheshimiwa Wabunge wameuchangia kwa upana wake. Kuna wengine wamegusia masuala ya mbolea, kuna wengine wamezungumzia masuala ya mbegu na wameleta kwenye Muswada wa Umwagiliaji. Ni sawa kabisa kwa sababu kwenye uchangiaji ule walikuwa wanasema pamoja na kuboresha miundombinu au kuboresha usimamizi kwenye umwagiliaji, ni lazima umwagiliaji huo uendane na maboresho katika maeneo mengine ya kilimo cha Tanzania. Naomba niseme siyo tu

kwenye hilo lakini pia kwenye masuala ya utafiti na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie kwa ujumla *the general aspect,* masuala mapana tu ya Muswada huu na tumekubaliana kwamba Mheshimiwa Waziri katika zile dakika zake 45 atakapokuja kuhitimisha, atawatambua Wabunge wote lakini pia tutajaribu kujibu hoja mojamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli. Jambo moja ambalo Waheshimwia Wabunge wote, waliopinga na waliokubali, wameweka tahadhari sana kwenye usimamizi wa umwagiliaji. Naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge waukubali Muswada huu maana unakotokea, naomba nitoe mfano mmoja tu.

Nimekwenda Wilaya ya Bahi kugagua miradi ya umwagiliaji. Katika Wilaya hiyo, kuna miradi ya umwagiliaji mizuri sana pale lakini kuanzia pale ambapo miradi ya umwagiliaji ipo na ofisi za Halmashauri, hapazidi kilomita mbili (2). Nimekwenda pale, nawauliza wanachama wa zile skimu, hivi wasimamizi wa mradi huu walikuja lini? Wanasema sisi tuna mwaka hatujawaona, hata kilomita mbili ofisi zao hazifiki. Sasa Muswada huu unataka kujenga misingi ya haki na uwajibikaji katika miradi ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mradi wa umwagiliaji wenye hela ndogo, *any way you look at it.* Ukichukua ile miradi ya umwagiliaji ambayo tunasema ya asili, iliyoanza tangu mwanadamu alipojifunza kupanda mbegu, maana

wataalam wanasema binadamu alipoanza kujifunza kupanda mbegu, kitu cha pili alichotengeneza ni ndoo ili kuweza kumwagilia. Hasa ukiondoka kwenye zile *format* za *traditional irrigation,* unakuja kwenye *spray irrigation and then* unakuja kwenye *technology* ya sasa ambayo tunasema ni *drip irrigation,* zote hizi zina taratibu zake za usimamizi. Sheria hii imelenga tupate ufanisi mkubwa zaidi kwa miradi yetu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge iliyojielekeza kwenye kuhakikisha kwamba hata kama tukianzisha Tume ya Umwagiliaji, tunapanda kutoka kwenye Idara ya Umwagiliaji tunakwenda kwenye Tume ili kudhibiti zaidi usimamizi wa sekta hii muhimu. Usimamizi huo lazima uwe na tahadhari ya kwamba sasa tunaondokana na zile *practice* za zamani. Ukiangalia vifungu vya mradi ule kwenye maeneo yote, Muswada huu umejielekeza huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja za uwekezaji ambazo zimetoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Naomba niseme tu kwamba, katika muda wote ambao sisi tumejikita kufanyakazi na Muswada huu, Muswada huu haulengi kujikita kwenye masuala ya uwekezaji ndani ya kilimo, hapana! Muswada huu, unalenga masuala ya umwagiliaji kwa upana wake. Kutakuwa na uwekezaji ndani ya umwagiliaji, naam, lazima uwepo kwa sababu miradi ya umwagiliaji inachukua fedha nyingi, za umma na za watu binafsi lakini athari zake pia ni pana. Kwa hiyo, kwa sababu kuna fedha za umma, kuna fedha za watu binafsi, tumesema hivi, kuendeleza miradi ya umwagiliaji, tunataka tuitazame kwa upana wake. Kwa hiyo, sheria hii

imezungumzia haya na watu wa sekta binafsi, anzisheni miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumesema, ukiangalia pale kwenye *Chapter* Six, inasema '*Management of Irrigations Schemes',* inazungumzia *categorically* kwamba miradi hii itakuwa na utaratibu wa kuisimamia ambao utakuwa ni *uniform.* Ukiwa wewe mwekezaji mkubwa, ukiwa mwekezaji mdogo, lazima ufuate zile taratibu ambazo zinafanya miradi ya umwagiliaji kuwa ndelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la uwekezaji ndani ya hii Sheria ya Umwagiliaji, naomba tutazame kwamba suala la uwekezaji halizungumziwi kwenye kuwezesha uwekezaji, hapana, linazungumziwa kwenye kuhakikisha kwamba uwekezaji ule unakuwa na ufanisi ambao unawezesha umwagiliaji uwe endelevu kwa sisi na huko mbele tunakokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine limezungumzwa la utwaaji *(acquisition).* Nilikuwa najaribu kuangalia, kwa sababu tulikuwa tunaangalia kama Muswada wenyewe ulivyoandikwa kwa Kiingereza na tafsiri yake kwa Kiswahili, kama zimeweka msisitizo kwenye utwaaji. Nimegundua kwamba pale kwenye kutangaza haya maeneo, kwa sababu inaonekana kifungu kinachofuata cha 18, ni suala la utwaaji, panaonekana pana mgogoro pale lakini niseme tu kwamba hii *aspect* ya utwaaji wa maeneo kwa ajili ya *irrigation,* haina maana kwamba ukitangaza eneo basi umelitwaa, hapana! Tunachosema ni kwamba ukitangaza eneo kuwa eneo la umwagiliaji, kuna misingi ya kilimo bora au misingi ya

usimamizi ambayo inabidi idhibitiwe pale ili eneo lile liweze kuwa linandelea kumwagilia kwa miaka 30 au 40 inayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachojua ni kwamba kuna miradi mingine ya umwagiliaji ambayo tunaiona na ninyi wengi mkiwa kama Waheshimiwa Wabunge mnajua kwamba Serikali imewekeza hela kwenye miradi mingine ya umwagiliaji ambayo mpaka sasa haina mchango mkubwa kwa yale malengo yaliyokusudiwa. Sasa, *what went wrong,* nini kilichokuwa na matatizo, labda ni usimamizi lakini tunajua pia kwamba labda pana ubadhirifu kwenye ile miradi, pana mambo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe mfano tu, kuna mradi mmoja nilikwenda na Mheshimiwa Omary Baduwel hapohapo Bahi. Mheshimiwa Omary Baduwel, alitoa kwenye pesa zake za Jimbo kama Sh.1,500,000/= akatibu tatizo ambalo wataalam walikuwa wamelikadiria Sh. 8,000,000/=. Hiyo Sh.1,200,000/= au Sh.1,300,000/= hivi ambazo Mheshimiwa Omary Baduwel aliweka pale, imewezesha heka 600 za mpunga zikalimwa mwaka huu na zimezalisha kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachosema lazima tufike sehemu miradi hii ya umwagiliaji iwe na ufanisi fulani. Itatumia fedha za umma, itatumia fedha ambazo Bunge litapitisha hapa lakini tunachotaka sasa tuboreshe usimamizi kwenye miradi ile. Ndiyo maana tumesema kwenye vile vipengele vya adhabu, kuna vipengele vikali, mle ambavyo vinasema ukishakuwa wewe ni kiongozi wa mradi halafu ukafanya vitendo ambavyo kwa makusudi vinahujumu mradi ule, uko *subject* kupigwa faini au hata

kufungwa. Tufike sehemu ambapo sisi Watanzania, tuogope kufanya uharibifu kwenye mambo ambayo yana maslahi kwa sisi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Mheshimiwa Amina Mwidau jana alisema, hizi adhabu inaonekana hazitoshi na Waheshimiwa Wabunge wengine wamezungumzia kwamba hizi adhabu zinaonekana ni ndogondogo kwamba mradi wa umwagiliaji unaingia Sh.600,000, Sh.800,000 mpaka Sh.1,000,000,000. Mtu anafanya uharibifu wa makusudi, zile Sh.1,000,000,000 zitakuwa zimepotea, unampiga faini Sh.2,000,000, hapana! Wamesema tukitaka kuweka uwajibikaji kwa wale wasimamizi wa miradi hii, lazima tuongeze adhabu kali. Niseme tu kwamba na sisi wakati tunapitia michango ya Wabunge, nafikiri tumesema kwamba kulingana na mapendekezo haya ya Wabunge, jambo hili tulifikirie kwa pamoja na tuone namna tunavyokwenda mbele na jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili suala la utwaaji wa maeneo, ni *very specific.* Unapotangaza eneo, unasenma mradi huu ni *irrigated area.* Waziri wa Kilimo analitangaza lile baada ya kushauriana na Waziri wa Ardhi, kwa hiyo, eneo lile linachorwa kwamba ni la *irrigation.*

Sasa kwenye eneo lile, mambo yale ambayo yanaleta hujuma kwa masuala yote ya umwagiliaji, hayaruhusiwi. Siyo kwamba ukitangaza eneo lile ni *irrigated area* maana yake lile eneo sasa kama lilikuwa ni mali ya Mheshimiwa Nassari, basi umemnyang'anya Mheshimiwa Nassari, hapana! *No aspect of that law* inasema hivi lakini, kuna

maeneo ambayo kwa usimamizi bora wa umwagiliaji, kwa mfano, kuna maeneo ambayo vyanzo vya maji viko kilomita mia moja, mia moja hamsini, ukiviharibu kule, huku hatupati maji. Sasa tukasema inabidi uweke utaratibu wa *irrigated area* zile na maeneo yanayoleta maji katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba katika kutengeneza sheria hii, kuna sheria nyingi sana nyingine ambazo zinaingia humu. Kwa hiyo, tunapoangalia mambo ya matumizi bora ya maji, matumizi bora ya maji yako kwenye Sheria ya *Water Resources Management Act,* ambayo ni sheria nyingine ambayo imetengeneza utaratibu kabisa wa namna ambavyo vyanzo vya maji na matumizi ya rasilimali maji vitashughulikiwa. Ziko Sheria za Ardhi na *land management* na kadhalika, hizo ziko kwa kina Mheshimiwa Ole-Medeye na nani, zimepangiwa utaratibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sheria hii au hiyo Sheria ya Utwaaji, hiyo iko kwenye *Land Acquisition Act,* Rais anayo mamlaka ya kutwa ardhi vile anavyoona ina maslahi kwa Jamhuri ya Muungano. Katika jambo hili sisi hatutengenezi jambo jipya, ila tunasema tu kwamba katika uwezo wake Mheshimiwa Rais, wa kutwaa ardhi kwa ajili ya maslahi ya Jamhuri ya Muungano, awe pia ana uwezo wa *consideration* ya *irrigation* kama moja katika yale mambo muhimu ambayo anaweza kutumia kwa ajili ya kutwaa ardhi lakini Mheshimiwa Rais ana upana wake wa mamlaka ya kutwaa ardhi kwa ajili ya maslahi ya Jamhuri ya Muungano.

Waheshimiwa Wabunge, naomba Mheshimiwa Rais atakapopelekewa ushauri wa kutwaa ardhi kutoka kwa Waziri wa Kilimo, Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa Ardhi, Waziri wa Mazingira na Waziri wa Maji, ushauri huu unakuwa umefanyiwa kazi kwa kina sana, siyo ushauri mwepesimwepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na shaka kidogo, labda katika hali hii wananchi kule katika ngazi ya chini hawajazingatiwa, naomba niseme ndiyo pale anapoingia Waziri wa TAMISEMI. Ni matarajio yetu kwamba Waziri wa TAMISEMI itakapofika kwenye kutoa ushauri wa namna hii, kwa namna moja au nyingine atakuwa tayari amepata maoni kutoka kwenye Halmashauri na kwa maana hiyo kutoka kwenye vijiji na maeneo ambako wananchi wanakaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna michango mbalimbali ambayo imekuja kutoka kwa Waheshimwia Wabunge katika sura hiyo, naomba niseme kuna mchango wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Magdalena Sakaya, yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo, kwa hiyo tulikuwa naye na tumefanya kazi chini ya Mheshimiwa Profesa Msolla kwa siku zaidi ya sita (6), tumefanya kazi ya masaa mengine sana. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Profesa Msolla na Kamati nzima ya Kilimo, kwa kazi nzuri sana ambayo tumeifanya kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Magdalena Sakaya alisisitiza jambo akasema, kuna maeneo ambayo

yalitengwa kwa ajili ya kilimo lakini sasa hivi yanachukuliwa na watu, ametoa mfano wa maeneo mbalimbali, mimi ninakubaliana naye. Pamoja na hili, kuna Wabunge wengine wamezungumzia suala la kubadilisha matumizi ya ardhi, mtu anachukua heka 10,000 kwa ajili ya kuendeleza shamba halafu anakwenda kufanyia kitu kingine, anaenda kuiweka *collateral* kwenye benki, hakuna sheria inayoruhusu hilo. Hapo siyo suala ya sheria au upungufu wa sheria, ni suala la usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mheshimiwa Mbunge, nadhani alikuwa Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, alizungumzia kwamba kuna Sheria za *Traffic* lakini watu bado wanagonga magari, *that is human nature,* kuna Sheria za *Traffic* lakini watu wanaendesha wakiwa wamelewa. Hivyo, kwa sababu watu wanaendesha wamelewa *you can not say* tusiweke sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo na sisi tunaweka sheria za usimamizi bora wa *irrigation* ambazo zitaenda sambamba na usimamizi bora wa ardhi ya kilimo. Tunasema lengo ni kutenga maeneo yale ambayo tunaona hata kwa miaka 50, 100 ijayo yatatosha kwa ajili kuendeleza kilimo. Sasa tusibadilishe maeneo yale leo tukaanza kujenga makazi, tukaanza kufanya nini, kwa sababu *demand* ya chakula itakuwepo leo, kesho mpaka siku ya kiama. Kwa hiyo, lazima tuweke *provision* ya mahitaji hayo.

Naomba niseme tu kwamba ushauri wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya ikiwa ni ipamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine waliojielekeza katika hilo, tumeukubali

na tutaufanyia kazi ili kuhakikisha kwamba Muswada huu wa *Irrigation* unakuwa na usimamizi mkali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango mwingine muhimu ulitoka kwa Mheshimiwa Dokta Titus Kamani Jongo, alisema Muswada huu umekuja kwa wakati muafaka na hakuna kitu kibaya kama utumwa wa njaa. Pia alizungumzia uendelevu na usimamizi wa Muwada huu lakini naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani Jongo, wa Kisarawe, aliposema kwamba Muwada huu tusitumbukize ushabiki, masuala haya hayana ushabiki, masuala haya yana *facts* tu, naomba nimshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitambue michango ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mendrad Kigola na Mheshimiwa Modestus Kilufi, waliosema kwamba Muswada huu, hauji kubaini maeneo mapya ya umwagiliaji, umwagiliaji tayari upo Tanzania, tuna skimu zaidi ya 2,500. Muswada huu unakuja kuweka utaratibu kwa skimu zile lakini pia kwa skimu nyingine mpya ambazo zitakuja. Mheshimiwa Kigola alisema wao hawasubiri Muswada huu, wao wanategemea kwamba Muswada huu utakuja kuwaboreshea tu utaratibu wao umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale wenye miradi ya umwagiliaji, wanajua umuhimu wa Muswada huu. Miradi hii ya umwagiliaji, unakuta wakati mwingine ina migogoro mingi baina ya wanachama wake, ina migogoro mingi kuhusu matumizi ya maji, ina migogoro mingi kuhusu ujenzi wa ile miundombinu ya maji. Wakati mwingine mnakuwa na wanachama 30, 10 hawashiriki, hawaangalii namna

bora za kudhibiti mradi, wengine 20 mnahakikisha kwamba maeneo yenu yako sawasawa.

Sasa kwa namna hiyo, ufanisi wa ule mradi unakuwa hauko sawasawa. Kwa hiyo, tunasema kwamba kuna *good practices in irrigations schemes.* Kuna kipengele kipo hapo, kinachosema kabisa hilo. Tunasema hilo linakwenda kwa watu wote. Wadau, wanachama, wote tunawajibika kuwa na tamaduni bora katika usimamizi bora wa miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitambue mchango wa Mheshimiwa Dokta Christina Ishengoma na hasa pale aliposema kwamba na wao kama Kamati imefanya kazi kubwa halafu kuna Mheshimiwa mmoja akamkatalia kwamba huu Muswada si Muswada wa Kamati. Nataka nimwambie tu kwamba katika hatua hii, huu Muswada ni wetu wote sasa maana Kamati imefanyia kazi na sisi na tulicholeta hapa pamoja na *schedule of amendments*, ni mchango mkubwa sana wa Kamati ambao tumeutambua na tumeuweka kwenye mabadiliko hayo ya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejielekeza kwenye hili jambo la *declaration,* hili neno *declaration,* naona limetumika vibaya, *declaration* limetumika kama kutwaa, hapana *declaration* ni kutangaza, kuliwekea taratibu eneo liwe ni eneo la umwagiliaji. Tunasema na wale wanaomwagilia humo ndani wanabaki katika hodhi ya eneo lile, wanabaki nalo lakini tunasema kwamba sasa chini ya sheria hii mtafanya umwagiliaji kwa utaratibu ambao ni endelevu na wenye ufanisi na kadhalika, kwa

maana ya ku-*declare* siyo kwamba umenyang'anywa eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala lile la Mheshimiwa Mnyaa na ameliweka kwenye *schedule of amendment*s, namshukuru sana. Alisema kwamba sheria hii kwa sababu iko upande mmoja wa Muungano, haiko upande mwingine, iseme wazi. Tumepata maelekezo ya kisheria ambayo yanasema kwamba sheria ile inapokuwa haikusema kwamba, *this Act will apply to Tanzania Mainland and Tanzania Zanzibar, assumption automatically* ni kwamba *it will apply only to Tanzania Mainland.*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana na mimi, tulipokuwa wote kwenye Kamati ya Nishati na Madini, haya ndiyo mambo ya Wanasheria, *that is advice* ya kisheria kwamba isiposema maana yake *it applies to one side* lakini tukaulizana, ikisema ina tatizo gani? Nadhani hilo tutalijadili wakati wa vifungu na Mheshimiwa Waziri atakuja kulisemea kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo pia naona nilisemee kidogo. Kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja alisema, Waisrael walikuja wakamwambia kwamba Watanzania hatutumii akili zetu sawasawa kwa sababu vinginevyo tungelisha dunia nzima. Mimi naomba niseme kwamba *that is quite scientifically difficult to believe* kwa sababu ile *land mass* ya Tanzania, *capacity* yake na *acreage* yake *to feed now going to eighty billion individuals, is a beat difficult to comprehend* lakini basi kwa sababu Mheshimiwa Mbunge anasema Waisrael wale

wamemwambia, sijui wanatumia teknolojia gani ya kwamba sisi Tanzania tulishe dunia nzima.

*I would agree* kwamba wenzetu Waisrael wana *practices* nzuri sana za umwagiliaji ambazo tunaweza kujifunza kwao lakini mimi nadhani tuna miradi mingi ya umwagiliaji, kule kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, kuna miradi mingine tumeiona sisi ambayo watu wanamwagilia *the perfect*. Kuna mradi mmoja Malolo kule kwa Mheshimiwa Abdulsalaam nimekwenda kuona, *it is a beautiful one of the* mradi, inakwenda vizuri tu. Kwa hiyo, nasema tusikae tukasema kila kitu tunachofanya Watanzania ni kibaya, tunahitaji watu wengine kuja kutuambia kwamba hatuna akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema Muswada huu unaendana na *obligations* zetu pia kwenye Jumuiya za Kimataifa kama alivyosema Mheshimiwa Jenista Mhagama pale kwenye mikataba tuliyoweka kwenye *SADC* kuhusu kuangalia *food security* na kadhalika. Mradi huu, tusiogope uzalishaji mpana wa chakula kwa sababu masoko ya chakula yanayotuzunguka, yote yanatuangalia sisi. Kuna Mheshimiwa Mbunge alisema jana kwamba tukiwa na *food surplus,* peke yake ni *guarantee* ya *national security.* Hakuna mtu atakayetuchezea wakati anajua sisi ndiyo tumeshika chakula cha eneo zima. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba, katika hilo, upana wa Muswada huu unatambua hayo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kipengele kile kinachosema, tutambue *contribution* ya wakulima wadogo kwenye *irrigation schemes*. Hilo liko kwenye *irrigators*

*organizations* na mikakati waliyoandaliwa wao ili waweze kuwa ni sehemu ya miradi ya umwagiliaji kwa ufanisi bora. Pia sheria inatambua kwamba watakuwa na mikutano ya kila mwaka ya wadau ndani ya skimu zile na inatambulika kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Felister Bura alizungumzia kwamba skimu za umwagiliaji zianzie Dodoma. Naomba nimwambie tu kwamba Dodoma kuna skimu nyingi, kuna skimu moja hapo Bwigiri, kuna skimu Chamwino kule kwa Mzee Chibulunje tulikwenda na skimu hizo zinafanya kazi vizuri na zinaweza kufanya vizuri zaidi zikipata usimamizi bora zaidi. Kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba hapahapa Dodoma, tuna skimu nzuri sana za mfano ambazo ningeomba Waheshimiwa Wabunge waende kuziona na zingine zina matatizo na ndiyo maana tunakuja na sheria hii. Kwa mfano, kuna skimu nyingine zinatumia maji mengi mno kuliko mahitaji yake. Kwa hiyo, ukipata ushauri pale wa kitaalam na ndiyo sheria hii inachosisitiza, pamoja na haya yote utakuwa na *efficient use of water resources.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hamad Rashid aliyezungumzia suala la *analysis* ya gharama za sheria. Hili suala ni muhimu, ni la kisasa kwamba mnapotengeneza sheria lazima muangalie pia na *economic viability* yake ikoje. Hili wenzetu wa India kule na baadhi ya nchi zimeanza kutumia *economic viability* kwenye kufanya *assessment* ya utungaji wa sheria. Tutaliangalia, ni jambo nzuri kwenda kuangalia sheria hii manufaa yake ya kiuchumi lakini pia na gharama zake na kadhalika mpaka iki-t*ake off* ni kiasi gani. Naomba niseme tu kwamba, kwa

kuwa inajielekeza kama nilivyosema kwenye ku-*address* masuala ya usalama wa chakula na lishe, huo ndiyo msingi mkuu wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo limezungumzwa ambalo pia ni muhimu sana, nadhani alilizungumza Mheshimiwa Mangungu na Mheshimiwa Hamad Rashid, walisema unapofanya *application* ya *irrigation* skimu na nini, tuondoe hii hali ya kwamba mtu anafanya *application* halafu anakaa mwaka mmoja, miaka miwili hajapata leseni yake, kama mtu ametimiza vigezo vyote, apewe leseni.

Sasa nasema yale masharti ya kwamba ni muda gani awe ameshapewa leseni, kuziweka kwenye sheria kidogo inakuwa ngumu, ni wepesi zaidi kuziweka kwenye kanuni za Waziri. Mimi na Mheshimiwa Waziri, tumelizungumzia hilo, kuna baadhi ya mambo mengi tu ambayo yameletwa na Waheshimiwa Wabunge ambayo kwa utekelezaji wake bora, ni vizuri zaidi yakaenda kwenye kanuni za Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitambue mchango wa Mheshimiwa Mendrad Kigola na Mheshimiwa Selemani Jafo, mdogo wangu, anasema, sisi kwenye Mkoa wetu wa Pwani, tuna maeneo ya Mto Wami, Rufiji na Ruvu, ambapo maji haya yanamwagika tu yanakwenda baharini. Sasa tukipata utaratibu wa kuyatengenezea skimu za umwagiliaji, maji haya na ukizingatia kwamba Dar es Salaam ndiyo soko kuu, sheria hii inalenga kuangalia namna ya uwekezaji na uwezeshaji wa wananchi ili kuendeleza skimu za umwagiliaji kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niseme kwamba, kama nilivyosema, kuna Waheshimiwa Wabunge wengine walisema kwamba sheria hii pamoja na ubora wake wote lakini isipozingatia masuala ya mbegu na mbolea kwa wakati na wengi wamelizungumzia, pamoja na Mheshimiwa Moza Abeid, itakuwa ni *useless*. Sasa hizo ndiyo *economic viability, economic impact* za sheria hii ambazo tunasema lazima ziendane na sheria zingine ili kuiwezesha kufanya kazi kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala pia Mheshimiwa Mangungu alizungumzia kuhusu *coordination* ya Wizara, kwamba zinaonekana ziko Wizara tatu, nne ambazo inabidi ziwajibike kwa pamoja. Tumekubali, hilo ni jambo muhimu sana na tutalifanyia kazi na kuhakikisha kwamba sheria hii katika utekelezaji wake inazingatia masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ally Keissy alizungumzia suala la kukataa uwekezaji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua dakika mbili za Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie, nitambue tu kwamba kuna masuala haya muhimu yamezungumziwa, Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Agripina, walizungumzia usimamizi wa chombo hiki. Mheshimiwa Riziki Lulida pia alizungumzia usimamizi na Mheshimiwa Yussuf

naye alisema kwamba umwagiliaji huu tunautaka lakini lazima tuweke mipango ya *irrigation* ambayo ni *integrated*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho alichangia Mheshimiwa Ester Bulaya, suala la kwamba pamoja na sheria hii izungumzie *impact* yake kwa vijana. Tunasema, vijana kwa sababu kuna *irrigators groups* pale kwenye *irrigators organization,* matarajio yetu ni kwamba vijana wanaweza wakatenga heka zao kumi, ishirini ndani ya *an irrigated area* na wao wakapata leseni ya kuendeleza mradi wao na pia sasa kwa sheria hii wapate msaada wa kitaalam ili kuwa na uzalishaji uliokuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la adhabu tumelizungumzia na tunadhani tutazungumza wakati wa kupitisha vifungu mbalimbali vya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana wewe, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa michango yao mbalimbali na kwa pamoja nasema, naomba tuunge mkono hoja hii ili tukitoka hapa tukafanye kazi ambayo itakuwa maslahi mapana kwa Watanzania wote bila kujali itikadi zao, wala rangi zao na dini zao kwa sababu sheria hii ni kwa manufaa kwetu sisi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Malima. Sasa

naomba nimwite Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Mhandisi Chiza. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nitumie nafasi hii dakika zangu 45, kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri sana ambayo yote ilikuwa na afya kwa kuchangia uboreshwaji wa Muswada huu wa sheria ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ester Bulaya alisema vizuri sana kwamba kazi yetu ni kutunga sheria. Kwa hiyo, tunapokuwa humu, kazi ni kuboresha, ni kuchangia na mimi nimeyachukua maneno yale kwamba wote waliochangia, wamefanya vizuri kwa sababu imenisaidia pia kujua ni wapi hawaelewi na ni wapi tuweze kusaidiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaweza kabisa kupitia hoja za kila Mbunge na haya makabrasha nimeyaleta hapa kuwaonyesha tu kwamba ni mengi na sitakuwa na uwezo wa kupitia moja baada ya nyingine. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa amejibu baadhi ya hoja na mimi nitajitahidi nisirudierudie. Kwa hiyo, nimeleta haya tu ili muone, wale ambao hatutaweza kuwataja, tutajitahidi tuwaletee majibu ya maandishi ili angalau muweze kuona kwamba yale mliyochangia yamezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, naomba Waheshimiwa Wabunge watambue kwamba tumewagawia kijitabu hiki, kinaitwa 'Asasi za Wakulima

Wamwagiliaji na Kilimo Kwanza'. Kama hamkukipata humu basi kitakuwa kwenye *pigeon hole* kule, naamini hiki mkikisoma kitawasaidieni kwa shughuli hizi za umwagiliaji lakini pia hata kwenye Muswada ule wa Sheria ya Ushirika, kwa sababu kinazungumzia Asasi za Wakulima Wamwagiliaji. Kama kuna Mheshimiwa Mbunge hatakipata basi anipe taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Maji na Mifugo, chini ya uongozi mahiri wa Profesa Peter Msolla. Kazi ilikuwa ni kubwa, wamechambua kwa kina kuanzia Dar es Salaam mpaka hapa na kwa kweli walijitahidi hata kuchukua maoni mengi sana ya *public*. Kwa maana hiyo basi, Muswada ulioko mbele yetu, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, sio wa Chiza wala wa Serikali tu, ni wa Serikali, ni wa Kamati na kwa maana hiyo ni Wabunge, pamoja na *public* ambao waliweza kushiriki kule Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niishukuru Kambi ya Upinzani maana yake lazima na yenyewe iwepo, Waziri Kivuli, leo sitamsema sana kama nilivyofanya *last time* kwa sababu na yeye amesema na kama nilivyosema mimi, kazi yangu hapa ni kutizama amesema nini, kile asichoelewa nimweleweshe na ndiyo kazi ya Muswada huu. Siyo kuja tu kupinganapingana na ninaamini pale ambapo nitamwambia hapa ulikuwa hujaelewa na yeye atanielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jumla, wachangiaji wote walikwenda vizuri, ni sehemu moja tu na si kawaida yangu,

ni sehemu moja kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani mwanangu huyu ndiye kidogo tu alitaka kuniudhi lakini na yeye nimemsamehe bure na mimi kazi yangu ni kufundisha kama mzazi kwa sababu sisi Waha, tena amerudi Mheshimiwa, sisi Waha tunasema hivi na wewe Kiha unakijua, mzazi anachefuka lakini hatapiki.

**MBUNGE FULANI:** Sema Kiha.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mzazi anachefuka lakini hatapiki nimetafsiri kwa Kiswahili.

**MBUNGE FULANI:** Sema Kiha.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Sijui kama mnahitaji. *(Kicheko)*

"*Ngumuvyela sesemwa natanataka". (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake anachefuka hata ukimwudhi, lakini hatapiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekuwa nasema siku zote kwamba jamani wakati mwingine ukiwa mwongo pia usiwe msahaulifu. Ukisema uwongo usiwe msahaulifu baada ya dakika chache ukasema yaleyale uliyosema. Aidha, ukijifunza kupigana, ujifunza na kukimbia maana kuna siku ya kudundwa vilevile. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilitaka Mheshimiwa Mkosamali, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi wala sikuwa nimekwenda kote huko kutizama, nataka

leo tu nitumie nafasi hii kukufundisha kama mtoto wangu. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema mwaka 1986 ukizaliwa, mimi ndiyo *third born* wangu naye anazaliwa na mimi wakati huo tayari nilishakuwa na *masters degree,* kwa hiyo, bila shaka na mimi nina hazina fulani, naelewa mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichotaka kumfundisha Mheshimiwa Mkosamali kwamba katika kuchangia, hebu tujifunze, tufanye kama wapinzani wengine walivyofanya. Mheshimiwa Leticia Nyerere alichangia vizuri sana lakini ni mpinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid alichangia vizuri sana lakini ni mpinzani, Mheshimiwa Asaa alichangia vizuri sana lakini ni mpinzani, Mheshimiwa Amina Mwidau alichangia vizuri sana na wote waliunga mkono na nataka nitambue kabisa kuunga kwao mkono kwamba kumbe walichangia wakiwa wanaelewa kitu wanachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa mwanangu huyu, maana ni mwanangu Mheshimiwa Mkosamali, wewe si sawa na mtoto wangu tu sasa? Kuna methali nyingine ya Kiha inasema hivi, naisema kwa Kiha, *'nguratamba chane ukahena'* yaani ukicheza sana, mwisho upepo unapeperusha nguo zako unabaki uchi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana ukitia madoido sana baadaye unakosea. Maana yake nini? Kuna mahali ulisema eti watu wanafanya umwagiliaji kwa mifereji, huu ni umwagiliaji, bila *pump*? Yaani umwagiliaji kwako wewe, ni *pump* tu? Basi sitaki tena kuanza kufundisha umwagiliaji ni nini, pata nafasi tuzunguke, mifereji ni umwagiliaji, hata *pump* ni umwagiliaji. Sasa ukiangia mambo mengine

kichwakichwa baadaye unaweza ukakosea, ndiyo maana nimesema ukicheza sana mwisho wake utakosea upepo unapeperusha nguo zako. Kwa hiyo, basi tujifunze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema nitumie maneno haya machache angalau mwanangu, Mheshimiwa Mkosamali na yeye ajifunze wakati mwingine. Alifika mahali akasema hata kwake na kwa Chiza ni sawa. Mimi nataka niyasema maneno haya na wenzetu kule nyumbani na wapiga kura wake wakisikia. Kwangu tunazalisha mchele na kwa miradi ya umwagiliaji na kule kwake pia wanazalisha kidogo lakini wanunua mchele hata tunavyozungumza wananisikia, wanunua mchele kwangu na sababu kubwa ni kwamba wao waliitikia mwito wakaanza kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo nataka kukufundisha kidogo mwanangu hapa, yale mambo ya kusema wananchi msichangie miradi, Serikali inafanya nini, ndiyo hayo yanasababisha miradi inabaki nyuma halafu wanashindwa kuzalisha. Ndiyo maana unaona mpaka leo wale watu wa Muhambwe bado wananunua mchele. Ni kwa sababu wakati fulani ulipitiwa kidogo ukawa unawaambia hata kwenye miradi ya maji, waache kuchangia, hapana siyo hivyo! Mimi naamini kwamba ulikuwa umeteleza tu na mimi nasema mzazi anachefuka hatapiki wala sikuhukumu kwa lolote na Mungu akubariki kabisa na wale watakaokupotosha washindwe kwa jina la Yesu. *(Makofi/Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Ameen. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niwatambue wote waliochangia katika Muswada huu, jumla wako wachangiaji 74 waliochangia kwa kuzungumza na kuandika. Waheshimiwa Wabunge 42 wamechangia kwa kauli na Waheshimiwa Wabunge 32 wamechangia kwa maandishi. Waliochangia kwa kauli ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Profes Peter Msolla, Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa David Zakaria Kafulila, Mheshimiwa Joshua Samweli Nassari, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, , Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mheshimiwa Mustapha Akunay, Mheshimiwa Dkt. Christina Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Mundwe Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka. *(Makofi)*

Wengine Mheshimiwa Habib Mnyaa, Mheshimiwa Mchungaji Peter Simon Msigwa, Mheshimiwa Ritta Enesfer Kabati, Mheshimiwa Pauline Phillip Gekul, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga, Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mheshimiwa Rashid Hamad Mohamed, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Luhaga Joel Mpina, Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele,

Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed Mohamed, Mheshimiwa Agripina Zaitun Buyogera, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh na Mheshimiwa Adam Kigoma Malima, Naibu Waziri na Mbunge wa Mkuranga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi wapo 32 nao ni Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye, Naibu Waziri, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mheshimiwa Capt. John Zakaria Chiligati, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura**,** Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele**,** Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembwe, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola na Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Rosweeter Faustine Kasikila, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mheshimiwa AnnaMaryStella John

Mallac na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso**.** Kama kuna niliowasahau basi nitaendelea kuwatambua baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo kwa wachangiaji, naomba niseme jambo hili japokuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amelifafanua lakini naomba na mimi nilisisitize. Muswada huu umeleta hisia nyingi kwa Wabunge na hata kwa walio nje ya Bunge maana yake hizo meseji ambazo mmekuwa mnapata hata mimi nimepata. Wengine wamefikiria maana ya Muswada huu ni kunyang'anya ardhi, kutwaa ardhi na kuwakabidhi wawekezaji.

Nataka niwahakikishie na niwatoa hofu Wabunge na wananchi wote mnaonisikiliza kokote kwamba Muswada haubadilishi chochote katika Sheria za Ardhi zinazotumika wala haulengi kutwaa ardhi yoyote ya mwananchi na kuikabidhi kwa mwekezaji mwingine. Hatukatai wawekezaji lakini nataka niwahakikishie kwamba haitatokea hata siku moja mwekezaji ama kwa sheria hii au sheria nyingine zozote zilizopo akaja katika nchi hii akawa mbadala wa mkulima, hilo halitatokea. Mkulima ataendelea na ardhi yake na pale ambapo mwekezaji atapata ardhi kwa mujibu wa sheria na wananchi wenyewe wakishirikishwa kikamilifu, naye atapata ardhi lakini hatutamfanya mwekezaji kuwa ndiye amekuwa mbadala sasa wa mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, vile vifungu kama kifungu cha 18 ambavyo vinawapa wasiwasi naomba visiwatie hofu kabisa kwa sababu hata ukivisoma kwa

undani, kifungu kama cha 18, kile kifungu kina-*qualify* vifungu vingine vilivyopo tu wala Waziri mwenye dhamana na umwagiliaji hawezi kutwaa ardhi yoyote ile akamkabidhi mtu mwingine na sitofanya hilo, kwanza sina mamlaka hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi yangu ni kutangaza eneo kwamba eneo hili limekuwa la umwagiliaji, maana yake nini? Tumeshuhudia maeneo mengi ardhi inayofaa kwa kilimo ikitumika kwa shughuli ambazo si za kilimo. Hata na ninyi ni mashahidi kule Arusha na sehemu nyingi, unakuta ardhi iliyokuwa ya kilimo hata ardhi ya Wizara ya Kilimo ikifanyiwa utafiti, mahali pengine imetwaliwa na watu, wakaibadilisha kufanya shughuli zingine za makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Waziri wa Ardhi, kama angepata nafasi angeweza kulifafanua hili. Sheria hii haiendi kabisa kubadilisha chochote hapa. Wala msije mkafikiria kwamba kifungu cha 18 sasa kinasema Waziri wa Kilimo sasa atakwenda atachukua eneo halafu akishalichukua anamshauri Waziri wa Ardhi wanakwenda wanamwambia Rais chukua hii ardhi, wakabidhi wawekezaji, wala hatufanyi hivyo. Hata Mheshimiwa Rais mjue ni taasisi na yeye wala hakurupuki hata siku moja, anafanya hivyo kwa mamlaka aliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwambie, utwaaji wa ardhi bado unatawaliwa na Katiba. Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ipo wazi kabisa katika jambo hili. Naomba ninukuu kwa ruksa yako Ibara ya 64(1) inasema, 'mamlaka yote ya kutunga sheria juu ya mambo mengine…' samahani, hili ni

suala lingine. Hili linahusu kifungu cha 17, mtanisamehe, nimechanganya kidogo, hilo la Katiba nitalizungumza baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kifungu cha 17 na 18, nataka nizungumzie ile habari ya kifungu cha 18 kwamba kifungu hiki kinatoa mamlaka kwa Mheshimiwa Rais kutwaa sehemu ya ardhi ambayo pengine itakuwa inatumika kwa madhumuni mengine ili iweze kutumika kwa madhumuni ya kilimo cha umwagiliaji hasa ujenzi wa miundombinu. Utaratibu wa kutwaa ardhi chini ya kifungu hiki, utafanyika kupitia Sheria ya Kutwaa Ardhi, Sura 118 yaani *The Land Acquisition Act.*

Sasa hii ni sheria ambayo ipo ambayo wala hatuizungumzii katika sheria hii wala sheria hii haibadilishi ile Sheria ya *Land Acquisition*, hata tusingeitaja hapa, sheria ile bado ipo. Kwa hiyo, utaratibu wa kutwaa ardhi utafuata misingi ya utwaaji ardhi kufuatana Sheria za Ardhi zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijikita kwenye suala hili la umwagiliaji, nataka nilifafanue kidogo ili lieleweke maana yake naona kwa kweli lilileta mkanganyiko. Tunaposema Waziri wa Kilimo atatangaza eneo, katika kile kifungu cha 17, hatumaanishi kwamba sasa ametangaza ili lichukuliwe. Tunapotangaza eneo kuwa la umwagiliaji maana yake nini? Eneo la umwagiliaji ni pamoja na miundombinu, umejenga tuta kwa maana ya *dam*, linatengeneza bwawa, lakini pia inatengenezwa mifereji na *pump* kama zipo na Mheshimiwa Mkosamali ujue hapo sasa mifereji ni kazi yake hiyo kutoka maji kule kwenye bwawa kupeleka kwa wakulima. Sasa eneo hili kulitangaza kuwa ni la kilimo

cha umwagiliaji maana yake asitokee mtu tena akaja akawadhulumu wakulima wale, akaanza kufanya kazi zingine kama kazi za biashara kujenga hoteli katika eneo la kilimo cha umwagiliaji lakini eneo hilo bado ni la wakulima wadogowadogo walewale.

Kwa hiyo, maana ya Muswada huu kwa kifupi ni kwamba kutaka kuhakikisha wakulima hawaporwi ardhi yao na ardhi yao inalindwa, iweze kuendelea kuzalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo nimeona nilisisitize kwa kweli kwa sababu limeleta hisia ambazo si dhana ya sheria hii. Naomba Mheshimiwa Mpina na Waheshimiwa Wabunge wengine wote mliolichangia mlielewa hivyo kwamba halikuwa na maana yoyote ile ya kutwaa ardhi na kuikabidhi kwa watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ni mfupi lakini naomba niende kwenye masuala ya kijumla kidogo. Tulianza umwagiliaji tukiwa hatuna Sera na Sera ya Umwagiliaji tuliipitisha mwaka 2010 lakini ninyi wote mnaelewa kwamba Sera haina meno. Tulichokifanya sisi ni kuleta Sheria ili itekeleze kwa vitendo Sera ya Umwagiliaji ya mwaka 2010. Kwa hiyo, sasa Muswada huu ambao upo mbele yetu, kazi yake ni kutusaidia kutafsiri yale tuliyosema kwenye Sera ya 2010 ili iweze kutusaidia kuendeleza umwagiliaji. Zipo sababu nyingi. Unapotaka kutekeleza Sera kwa kweli kama huna Sheria, huna meno na wengi mmelizungumzia kwa uzito kabisa kwamba jamani eeh tatizo letu si Sheria na mimi nakubaliana na ninyi lakini sheria lazima zipo na lazima zitungwe. Kwa kuwa Sheria ya Umwagiliaji haikuwepo na

sasa ndiyo inakuja kwa mara ya kwanza, kwa hiyo lazima iwepo.

Ninachokubaliana sasa na ninyi ni kwamba baada ya kuitunga lazima sheria hii sasa iwe na meno na ifanye kazi ili iweze kutafsiri yale yote tuliyojiwekea katika Sera ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema tuwe na muundo wa kitaasisi. Siku za nyuma tulikuwa na vitengo tu vya umwagiliaji, sisi wengine ambao tumekaa katika Wizara ya Kilimo miaka mingi, tulikuwa na Kitengo cha Umwagiliaji, kilianzishwa na wenzetu wa kutoka Sudan, walikuja Wahindi, kikawa kina-*move forward* na *backward,* mara Wizara ya Maji mpaka huko kwenye Wizara ya Ardhi tulikwenda.

Kitengo hiki kwa kweli kilikuwa kinayumbayumba. Baadaye tukaamua kwamba labda tukifanye kuwa Wakala wa Serikali (*National Irrigation Agency)* baada ya kuanzisha ile Sheria *National Executive Agency* ya mwaka 2000. Wakati huo tukaona pia kwamba kwa sababu Wakala wa Serikali ulipewa majukumu ya kufanya shughuli za kibiashara, baadhi ya wadau wakasema, Wakala unaweza usiwahudumie sana wakulima wadogo. Ikaamuliwa kwamba Wakala ule ulikuwa bado muda wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukaamua kwamba ili kuimarisha umwagiliaji, tuanzishe Idara ya Umwagiliaji na Huduma za Ufundi. Nayo tulipoianzisha, tukawa hatuna wataalam wa kutosha. Tukaanzisha kanda saba za umwagiliaji. Kanda ya Kati yenye Mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara, Kanda ya Morogoro, yenye Mikoa ya

Morogoro Pwani na Dar es Salaam, Kanda ya Mbeya yenye Mikoa ya Mbeya, Iringa, Rukwa, Katavi na Njombe, Kanda ya Kilimanjaro yenye Mikoa ya Kilimanjaro, Tanga na Arusha, Kanda ya Mtwara yenye Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma, Kanda ya Tabora yenye Mikoa ya Tabora na Kigoma, Kanda ya Ziwa yenye Mikoa ya Mwanza, Mara, Kagera, Shinyanga, Geita na Simiyu. Hii Mikoa mingine imeongezeka. Ndani ya Mikoa hiyo, kuna Halmashauri na ni nyingi na Waheshimiwa Wabunge wengi mmekuwa mkitoa hisia zenu, nami nazikubali kwamba Kanda kwa kweli kujiteremsha mpaka kufika kwenye Halmashauri, mahali pengine wamekuwa hawaoni, hawapati kile walichokitarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sheria hii imekuja na hoja ya kuanzisha taasisi ya kisheria yenye nguvu, Tume ya Umwagiliaji na haya yalikuwa ni maelekezo pia ya Mheshimiwa Rais baada ya kushauriwa kwamba tuanzishe Tume ya Umwagiliaji, chombo ambacho kitaweza kuwa na meno kisheria, kitaweza kutafuta fedha hata nje ya mfumo wa bajeti ya Serikali, kinaweza pia kuanzisha Mfuko wa Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mkosamali alisema, aah, mnataka kuanzisha kama *TANROADS*, sasa kuna ubaya gani kama Mifuko inaweza ikaanzishwa na wadau wakikubali maana Mifuko haianzishwi tu hivihivi lazima wadau nao wakubali. Wakisema huu Mfuko unafaa na utatusaidia kuchangia kuongeza maana yake ni ku-*leverage financial resources.* Tukasema Tume hii inaweza kutusaidia kwanza kwa kuwa na uwezo wa kisheria, uwezo wa kutafuta fedha pamoja na kuweza kuwa *sued* na ku-*sue,* itakuwa na meno zaidi ya

Idara ya Kiserikali. Kwa hiyo, Tume hii ndiyo maana tukasema inabidi iingie sasa iweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la muhimu zaidi, ni pale ambapo Tume tumeiwezesha ishuke mpaka chini kwenye Halmashauri kwa maana ya kwamba itakuwa na viungo. Tume yenyewe kama Tume haitakuwa ndiyo inayokuwa na Ofisi kwenye Halmashauri za Wilaya na naomba wanaonisikiliza mnielewe. Katika Halmashauri, tutakuwa na Mhandisi wa Umwagiliaji. Mhandisi huyu ataajiriwa na Halmashauri ya Wilaya.

Mamlaka ya udhibiti, mamlaka ya nidhamu, iko chini ya Halmashauri ya Wilaya. Kwa hiyo, Sheria hii na Tume hii haiji kupora kabisa madaraka ya Halmashauri za Wilaya, Madiwani watabaki palepale, mamlaka yao yapo palepale. Kwanza, itakuwa vigumu kwamba Tume imekaa Dar es Salaam iweze kujua yule Mhandisi atafanya kazi gani pale alipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba mnielewe hivyo tunachokifanya ni kwamba Tume kwa sababu itakuwa na mlolongo wa wataalam hawa, tunataka sehemu kubwa, *regulatory function* zake ziweze kwenda kwa Mhandisi yule aliyeko kwenye Halmashauri. Pale Mkoani tumemweka Mhandisi wa Umwagiliaji, naye asaidie katika ile Sekretarieti, yeye atakuwa moja kwa moja chini ya Tume lakini atasaidia kuwa kiungo maana yake Sekretarieti nayo lazima iwe na mtu anaye-*link,* isije ikawa kwamba wanapojadili hawana mtu anayezungumza masuala ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka nilikwenda Igunga, nikakuta kuna matatizo ya pamba. Wakati ule tulipojadili mambo ya pamba, tukajikuta kwamba wana Afisa Kilimo lakini masuala ya pamba alikuwa hawezi kuyafafanua. Yule ambaye anaweza kuyafafanua alikuwa anatoka kwenye Bodi ya Pamba, naye haruhusiwi kuingia kwenye vikao vya Halmashauri.

Mimi nililazimisha tu mwiteni aje. Sasa tunachotafuta hapa ni kuweka kiungo, huyu aweze kuwa anasaidiana na Sekretarieti pale alipo lakini pamoja na kusaidiana na Sekretarieti aweze kuyapeleka yale masuala muhimu ya kitaaluma, kama tuna *technical specifications,* azifikishe moja kwa moja kwa Mhandisi aliyeko chini pale kwenye Halmashauri. Ndiyo maana ukisoma vizuri baadaye mtaona mambo ya miundo, wenzetu wa Utumishi watatusaidia. Yule wa Halmashauri, taarifa zake zote lazima ampe Mhandisi aliyeko Mkoani.

Kwa hiyo, hili maana yake ni kuweka ule mtiririko tu wa masuala ya usimamizi wa kinidhamu na masuala ya kitaalam. Nasisitiza kwamba katika ngazi ya Halmashauri, Ofisi za Umwagiliaji zinazofunguliwa, zitakuwa sehemu ya Halmashauri, Madiwani watakuwa na mamlaka kama kawaida na hakuna atakayeweza kubadilisha mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema Kanuni ziandaliwe. Nakubali kabisa hili limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na mimi mkinikubalia, mkipitisha sheria hii, nitajitahidi hata kabla hazijasainiwa na Mheshimiwa Rais tuanze kuandaa rasimu ya Kanuni ili zitoke mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya usimamizi wa sheria wa vitendo, hili limesemwa kwa nguvu zote na Mheshimiwa Naibu Waziri amelisemea. Kazi yetu kubwa nimewambia wenzangu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na sasa tuna Naibu Katibu Mkuu wawili na Wakurugenzi kwamba sasa lazima tubadilike, tuache *business as usual* tufanye *business un usual* ili tusimamie sheria kwa vitendo na ndiyo kazi tutakayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mkituona tunakuja huko Wilayani, msiseme mbona mnatuingilia katika Halmashauri? Tutakuwa tunakuja kuingilia ili tuweze kufanya kazi ambayo mmetutuma. Mheshimiwa Mkosamali anajua jinsi tunakavyopata taabu tukitaka kujaribu kupanguapangua mambo ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wamezungumzia kuhusu rasilimali watu. Ni kweli tunahitaji kupata rasilimali watu na rasilimali fedha, hili halina mjadala. Tutaiomba Serikali, Mheshimiwa Mgimwa ananisikia, tusitumie muda mrefu kwamba tumeanza Tume sasa tuna miaka mitatu ya kujenga *capacity* haijaanza kazi. Naomba tutajitahidi, Tume hii ianze kazi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya utwaaji ardhi, nimeyazungumza kwa kirefu, sitaki kuyarudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nizungumzie suala la haki ya kutumia maji na mipaka. Hili nalo nataka nilizungumzie kwa sababu nimeona wakati wa uchangiaji kuna watu wamelichanganya. Humu ndani kuna watu

wanasema mbona kuna Ofisi za Mabonde, hii Tume tena itakuwa na kazi gani? Ofisi za Mabonde kwa kutumia Sheria ile ya Rasilimali za Maji, Na. 12 ya mwaka 2009, tuliandika wenyewe nikiwa chini ya Profesa Mwandosya, wanatoa haki ya kutumia maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maji kutolewa kwa ajili ya mradi wa umwagiliaji, sasa kinachotokea katika *scheme* ile ya umwagiliaji, tunaita *on farm works,* hizi shughuli zitakuwa zinafanywa na usimamizi wa Tume, ndiyo maana yake sasa. Pamoja na kwamba umeshapata maji, yako katika mfereji wako lakini asitokee mtu mwingine akasema na mimi nayachukua napeleka huku na yasitumike vibaya. Maana yake tunataka kila tone la maji linalotoka litumike kwa ajili ya kuzalisha mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejiwekea malengo tunataka tuzalishe mahindi ifikapo mwaka 2015, tuongeze tani laki moja zaidi ya hizi tani tunazozipata sasa hivi tani milioni 5.7. Tunataka upatikanaji wa mchele uongezeke kutoka tani milioni 1.1 ya sasa, tuongeze angalau tani 290,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunataka upatikanaji wa sukari uongezeke, kutoka sasa hivi tani 380,000 angalau tuongeze tani zingine 150,000. Sasa tunataka kila tone la maji linalotoka liweze kutumika kwa ajili ya uzalishaji. Kwa hiyo, hapa ndipo tunapotenganisha sasa majukumu ya Tume na hizi mamlaka nyingine, lakini zote kwa pamoja zinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la uwekezaji kwa wageni, naomba tena nilirudie, hata pale ambapo ardhi itapatikana, tena si ardhi ya wananchi ambayo inachukuliwa kuwapa wawekezaji, hata pale ardhi ambapo itapatikana ili mwekezaji apewe awe wa ndani au wa nje, hapewi moja kwa moja, taratibu tulizonazo ni kwamba, ardhi hii inatolewa kupitia *Tanzania Investment Centre* kwa utaratibu wa *derivative right*. Baadaye yule mwekezaji naye ndipo sasa anapewa. Kwa hivyo, ukitazama vizuri ni kwamba bado hata ile ardhi inabaki kuwa ni mali ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, umiliki wa miradi chini ya Halmashauri. Taratibu zetu ziko pale pale chini ya programu ya kuendeleza sekta ya kilimo, tunazo taratibu zetu za *DADP's (Districts Agricultural Development Plans)* zitaandaliwa katika Halmashauri na Mhandisi wa Umwagiliaji sasa atashiriki akiwa na Idara kamili. Kwa hiyo, fedha zote zitaendelea kwa utaratibu ule ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusisitiza hapa ni kwamba, baada ya Tume kupewa meno haya, utaratibu ule ambao Halmashauri nyingi zimeonesha kwa kutumia fedha za umwagiliaji vibaya, ni fedha nyingi sana. Nimemsikia Mheshimiwa Mwanri akipiga kelele kila anapokwenda, miradi iliyojengwa kwa kiwango cha chini, hapa ndipo tunataka sasa Tume isimamie na Tume itakwenda mpaka kwenye Halmashauri kuangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama fedha za umwagiliaji zimetoka lazima zifanye kazi ya kujenga miradi ya umwagiliaji na kama wamejenga chini ya kiwango

tutafuata sheria za kazi, tutafuata sheria za ki-*profession* kwa sababu kama ni Mhandisi amesajiliwa na Bodi ya Wahandisi, kwa hiyo atadhibitiwa pande zote. Atadhibitiwa pia ki-*profession* kwa kuwa ana mamlaka zinazomdhibiti ki-*profession*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunataka sasa tuingie ili tuhakikishe kwamba tunapata *value for money*. Kwa hiyo, umiliki utabaki pale pale, lakini usimamizi tunataka na sisi tuweze kuingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nifafanue kidogo tu kuhusu takwimu wakati nikiwasilisha hotuba yangu hapa. Nilisema tumetumia utaratibu mzuri tu wa kufanya *re-assessment* ya eneo linalomwagiliwa hivi sasa. Sasa naomba wale wanao-*quote* eneo linalomwagiliwa, chukueni hili eneo kama ndilo eneo sahihi na nimelitoa hata kwenye hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufanya *assessment,* eneo linalomwagiliwa hivi sasa ni hekta 454,392 tofauti na lile ambalo mnalolipata kwenye ripoti za zamani na kazi hii imefanywa na wataalam wamepita katika Ofisi zote za Kanda waki-*assess* miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimewapa kazi nyingine na kazi nyingine wanayoifanya ni kuhakikisha kwamba *scheme* zote za umwagiliaji ambazo zipo zifanye kazi sasa. Zinazoweza kuzalisha zizalishe hata mara mbili au mara tatu, kwa sababu lengo letu ni kwamba ifikapo mwaka 2015 asilimia 25 ya chakula cha Watanzania angalau itokane na kilimo cha umwagiliaji. Sasa hili hatutangoja mpaka miradi

mingine iidhinishwe, ni hekta hizi hizi tulizonazo tuhakikishe zinafanya kazi kwa mfumo wa kisheria na utaratibu mzuri ili tuweze kuzalisha. Tunachokifanya hapa ni kuongeza tu ile *cropping intensity.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Kafulila kwamba, eneo tulilonalo ni kubwa na mara nyingi anasema itatuchukua miaka 3,000 kuliendeleza. Hatutasubiri mpaka tulime Tanzania nzima sisi tunachotaka ni kuhakikisha kwamba eneo lile linaloweza kuzalisha lizalishe kwa tija, tuongeze *production,* tuongeze *cropping intensity* katika eneo hilo, hiyo ni *vertical development*. Halafu wakati huo huo tunaendelea kupanua mashamba *horizontal development* vyote vitakwenda sambamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Kafulila kwamba, kweli ukitazama katika maana ya kwamba, lazima tupanue eneo, unaweza ukaona aaha, ukaogopa. Lakini hata ukipanua eneo ukalima Tanzania nzima kama hatutalima vizuri, hatutumii pembejeo, hatuweki maji vizuri, hatusimamii kwa utaratibu, eneo lote tija yake inaweza kuwa ndogo sana. Kwa hiyo, nataka eneo lote hili tulilonalo, kwanza tuanze nalo lizalishe tuongeze *cropping intensity,* tuongeze tija katika uzalishaji, halafu ndio tuendelee kupanua kwa maana ya *horizontal development.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inatambua ushiriki wa sekta binafsi. Sheria yetu tuliona kabisa, moja ya udhaifu tuliokuwa nao, ni sekta binafsi kutokujishirikisha na kilimo.

Sasa Sheria hiyo ukiisoma vizuri utaona tumeruhusu sekta binafsi iweze kushiriki katika kilimo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta binafsi sio tu katika kujenga mifereji, sekta binafsi tunaitazama kwa mtazamo mpana, sekta binafsi katika ku-*design,* ma-*consultant* wetu wa Kitanzania wa-*design*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Leticia alisema mbona mnawaleta *Gem irrigation system* hapa. Kwanza nataka nimhakikishie kwamba hatujaingia mkataba wa fedha ni *memorandum of understanding* tu, lakini wale wanapokuja wanatusaidia ku-*back stop* wataalam wetu na *consultants* wetu ili waweze kushiriki na hao *consultants* sio lazima watoke Serikalini, wengine watatoka sekta binafsi. Kwa hiyo, tunataka sekta binafsi ishiriki katika suala zima katika *value chain* ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ugatuaji wa madaraka kwenda Wilayani nimelizungumza, lakini nimeshangaa katika mjadala mzima kwenye Kamati nilisikia, lakini huku sikusikia kelele za suala la jinsia katika Muswada huu. Kwa hiyo, naamini Muswada umezingatia suala la jinsia, ndiyo maana sikusikia kelele nyingi zikitoka kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nina muda bado, naomba kwa haraka haraka niende kwenye *specifics.* Naomba nijibu hoja za Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa haraka haraka tu, naomba niseme kwamba Kamati tumeshirikiana nao kwa muda mrefu, hoja zote walizotuletea tumezizingatia. Kwa mfano, walisema sheria

isimamiwe kwa umakini kwa lengo la kumlinda mkulima wa kilimo cha umwagiliaji ili anufaike zaidi. Hili tumelizingatia katika maelezo yangu nimesema hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa eneo husika washirikishwe kikamilifu wakati wa kutenga maeneo ya umwagiliaji, hili ni jambo la msingi kabisa na Wabunge wengi mmelichangia. Nasema kwamba, utaratibu wa kutenga na kutangaza maeneo ya umwagiliaji kama ulivyobainishwa katika kifungu cha 17 cha Muswada, utambuaji wa maeneo ya umwagiliaji, yatahusisha sheria nyingine ikiwemo Sheria za Ardhi, Sheria ya Maji, Sheria ya Mazingira na Sheria nyingine zote. Kwa hiyo, ushauri wote ambao tumepewa na Kamati tumeuzingatia kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ishirikiane na Wizara zote zinazohusika, Mikoa na Halmashauri, hayo nimeyaeleza. Serikali iweke utaratibu mzuri ili wakulima wadogo wasiathirike. Ushauri huu umezingatiwa na kwa kweli hatutafanya chochote kile kitakachoathiri wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, naomba nirejee, katika kilimo si suala tu la kulima ni pamoja na masoko na kuuza mazao. Nimesema katika muda wangu huu nikiwa Waziri wa Kilimo, ninachotaka nizingatie ni kuzalisha ziada, kujitosheleza kwa chakula, kuzalisha kwa ziada na kuuza ndani na hata nje ya nchi ili tusiendelee kuwasumbuasumbua wakulima na *road blocks* kwa kuuza mazao, ila wazalishe zaidi wauze ziada tu. Kwa hiyo, tutazingatia yale mahitaji ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi naweza kusema kwamba, yote ambayo Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji walitupatia tumeyazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nimejibu kwa kiwango cha kutosha hoja za Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika mazungumzo yangu na kama nitahitajika pia kutoa ufafanuzi nitajitahidi. Lakini naamini nilikuwa najaribu kuyagusa kwa sababu haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani ndiyo yalinifanya niweke maelezo yale ya utangulizi ili Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Sukum aone kwamba nimeyafafanua. Naamini amenielewa na tulizungumza kwenye chakula akasema ameelewa, naamini ataunga mkono hoja hii.

**WABUNGE FULANI:** Aaaa!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Sasa kwenye chakula hawazungumzi, si tunafafanua hoja tu. Wewe usiwasikilize hao, washindwe wote hao. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zingine tutaendelea kuzizungumza, leo nilikuwa nasikiliza kipindi cha *TBC* Leo, nilisikiliza hoja za Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Kafulilla, nadhani tumezijibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili kama Muswada hautaji kama utakwenda Zanzibar, Mheshimiwa Naibu Waziri amelieleza na ndiyo hilo nililotaka kufafanua mwanzoni pale, nikasema kwanza ni suala la Kikatiba kwamba sheria hii hatuwezi kuzungumza. Neno lile "*National*" wala halibadilishi maana kwamba sasa je, hii

sheria itakuwa tu ni ya Tanzania Bara au la? Sheria hii ngoja nimnukuu ili mpate picha kabisa. Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa pia alilizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninukuu ili nisikosee "Kuhusu suala la sheria ya kutotaja itatumika upande gani wa Muungano hili si tatizo. Zipo sheria nyingi zimetungwa na Bunge hili hazitaji mipaka yake ya kutumika".

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira hayo sheria hii itahesabika kuwa inatumika Tanzania Bara. Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ipo wazi katika jambo hili, inasema hivi:-

Ibara ya 64(1): "Mamlaka yote ya kutunga sheria juu ya mambo mengine yote yahusuyo Tanzania Bara, yatakuwa mikononi mwa Bunge.

(2) Mamlaka yoyote ya kutunga sheria katika Tanzania Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo mambo ya Muungano, yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi.

(3) Endapo sheria yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi inahusu jambo lolote katika Tanzania Zanzibar ambalo liko chini ya Mamlaka ya Bunge, Sheria hiyo itakuwa batili na itatenguka na pia endapo sheria yoyote iliyotungwa na Bunge inayohusu jambo lolote ambalo liko chini ya mamlaka ya Baraza la Wawakilishi, sheria hiyo itakuwa batili na itatenguka.

(4) Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge kuhusu jambo lolote haitatumika Tanzania Zanzibar ila kwa mujibu wa masharti yafuatayo:-

(a) Sheria hiyo iwe imetamka wazi kwamba itatumika Tanzania Bara na vile vile Tanzania Zanzibar, iwe inabadilisha, kurekebisha au kufuta sheria inayotamka Tanzania Zanzibar. Naomba nimalizie tu.

(b) Sheria hiyo iwe inabadilisha au kurekebisha au kufuta sheria iliyokuwa inatumika tangu zamani Tanzania Bara ambayo ilikuwa inatumika pia Tanzania Zanzibar kwa mujibu wa mapatano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1964 au kwa mujibu wa sheria yoyote ambayo ilitamka wazi kwamba, itatumika Tanzania Bara na vilevile Tanzania Zanzibar.

(c) Sheria hiyo iwe inahusu mambo ya Muungano na kila inapotajwa Tanzania katika sheria yoyote ifahamike kuwa sheria hiyo itatumika katika Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa ufafanuzi uliotolewa na masharti ya Ibara hii."

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema mengi sio kuyamaliza, naamini mengine tutaendelea kuyafafanua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Kabla hatujaendelea niwatangazie tu Wabunge wa CCM kwamba, saa 8.00 mchana kutakuwa na kikao pale Ukumbi wa Msekwa.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji wa Mwaka 2013 [*The National Irrigation Bill, 2013*]

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tuketi.

Waheshimiwa Wabunge tukitazama saa yetu, tunayo kama saa moja kupitia kwenye zoezi hili, kwa hiyo, tutapenda kila anayesimama atumie muda kwa bajeti.

Ibara ya 1

**NDG. ANSELM L. MREMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya kwanza ina marekebisho ya Mheshimiwa Engineer Mohamed Habib Juma Mnyaa na Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MWENYEKITI:** Badala ya Mheshimiwa *Engineer* Mnyaa, Mheshimiwa Hamad Rashid!

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. ENG. HABIB JUMA MYAA, MEMBER OF PARLIAMENT FOR MKANYAGENI CONSTITUENCY, AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE NATIONAL IRRIGATION ACT, 2013"**

*[Made under Standing Order 86(9) & (11)]*

A Bill entitled "The National Irrigation" is amended as follows:

**A:** In Clause 1, by deleting the word "National" appearing in the short title of the Bill and wherever it appears in the Bill.
**B:** In Clause 3 by-

(a) Adding the following new paragraph in sub-clause (6)

"(h) a representative nominated from the Ministry responsible for Energy and Minerals;"

(b) Renaming paragraphs (h), and (i) as paragraphs (i) and (j) respectively.

**C:** In Clause 11, by deleting the words "senior public officers" appearing in sub-clause (3), between the words "amongst" and "with", and replacing for it the word "persons".

Dodoma HON. ENG. HABIBU JUMA MNYAA (MP)

29TH August, 2013 **MKANYAGENI CONSTITUENCY**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya Waziri na Mwanasheria Mkuu, nimeridhika na maelezo yaliyotolewa. Ahsante.

**FURTHER SCHEDULE OF AMENDMENTS TO BE MOVED BY HON. LUHAGA J. MPINA, MEMBER OF PARLIAMENT FOR KISESA CONSTITUENCY, AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE NATIONAL IRRIGATION ACT, 2013"**

___________

**[*Made under Standing Order 86(9) & (11)*]**

___________

A Bill entitled "The National Irrigation Act, 2013" is further amended as follows:-

**A:** In clause 17

(a) by adding the words "the Commission or any person shall collaborate with" in sub-clause (5), between the words "rights" and "the";
(b) by deleting the words "shall be entitled to Compensation in accordance with relevant and law" or as may be agreed upon" and replacing for it the words "in the investment in the irrigation development".

**B:** In clause 18, by deleting all words and replacing for them the following new words:-

"there shall not be any displacement of people or dispossession of land as a result of implementation of this Act".

Dodoma HON LUHAGA J. MPINA (MP)
30th August, 2013 **KISESA CONSTITUENCY**

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. LUHAGA J. MPINA, MEMBER OF PARLIAMENT FOR KISESA CONSTITUENCY, AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE NATIONAL IRRIGATION ACT, 2013"**

**[*Made under Standing Order 86(9) & (11)*]**

A Bill entitled "The National Irrigation Act, 2013" is generally amended as follows:-

**A:** In Clause 1, by deleting the word "National" appearing in the short titled of the Bill.

**B:** In the interpretation Clause 2, by providing a proper interpretation of the phrase "Qualified irrigation engineer".

**C:** In Clause 11, by deleting sub-section (3) and replacing for it the following:-

"(3) A person shall not e recommended for appointment as a Regional Irrigation Manager unless he possesses the necessary qualifications as an irrigation engineer."

**D:** In Clause 14, by deleting the words "or any other officer from regional offices or under the local government authorities" appearing in sub-section (1) between the words "engineers" and "to".

**E:** In Clause 16, by-

(a) deleting the word "two" appearing between the words "then" and "million", and replacing for it the word "five";

(b) deleting the words "but not exceeding ten million shillings" appearing between the words "million" and "or"; and

(c) deleting the words "but not exceeding three years" appearing between the words "years" and "or".

**F:** In Clause 17, by deleting the words "or as may be agreed upon" appearing after the word "law".

**G:** In Clause 63 by-

(a) inserting the words "develop and" in sub-section (1)(a), between the words "fail" and "maintain";

(b) inserting the words "and order for compensation of the damage caused" in sub-section (2), after the word "forfeited".

Dodoma, Hon. Luhaga J. Mpina (MP)
28th August, 2013 **KISESA CONSTITUENCY**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana pia na maelezo ambayo yametolewa na Mheshimiwa Waziri na amesema kwamba, neno *National* pale halina athari yoyote na mimi sina pingamizi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Katibu tuendelee.

**NDG. ANSELM L. MREMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya pili ina marekebisho ya Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Luhaga Mpina!

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, neno *Qualified Irrigation Engineer* kama ambavyo limeelezwa katika Ibara ya 14 (1), ningeomba lipewe tafsiri ili kuleta maana yake halisi ili kujua kwamba *Qualified Irrigation Engineer* ni mtu wa sifa za namna gani? Kwa hiyo, ningeomba hili liwekwe kwenye tafsiri kwenye sheria ili lijulikane.

**MWENYEKITI:** Sasa ni vizuri Waheshimiwa Wabunge niwarudishe nyuma kidogo ile 5.1, ile *clause* ya kwanza kwa vile haina mgogoro wowote inaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. CHRISTOPHER K. CHIZA, THE MINISTER FOR AGRICULTURE, FOOD SECURITY AND CO-OOPERATIVES AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE NATIONAL IRRIGATION ACT, 2013"**

---

*Made under S.O. 86(10) (b)*

---

A Bill entitled "The National Irrigation Act, 2013" is amended generally as follows-

**A:** In Clause 2, by-

(a) deleting an article "a" appearing between the words "Commission" and "established" in the definition of the word "Commission" and substituting for it the word "as";

(b) deleting the definition of the term "canal" and substituting for it the following:-

"canal" means an open channel allowing free or controlled flow of water and may include underground channel";

(c) deleting the definition of the term "channel" and substituting for it the following:-

"channel" means any ditch, aqueduct, trench, conduct, tunnel, sluice, or flume allowing free or controlled flow of water for irrigation";

(d) deleting the words "practice of causing water to be removed" appearing in the definition of the term "drainage" and substituting for them the words "removal of water";

(e) adding, in the definition of the term "member" the words "and including the Chairman" immediately after the word "Commission";

(f) deleting the words "sub-oil drain" appearing in the second line in the definition of the term "drainage works" and substituting for them the words "sub-soil drainage";

(g) adding the words "responsible for land" immediately after the word "Minister" appearing in the third line in the definition of the term "irrigation area;

(h) deleting "Cap. 366" appearing in the marginal note in the definition of the term "Irrigation Inspector";

(i) deleting the word "operational" appearing in the third line in the definition of the term "irrigation service fee" and substituting for it the word "operations";

(j) deleting definition of the term "irrigators' organization" and substituting for it the following:-

"irrigators' organization" means a group of farmers formed and registered under this Act or any other written law, and approved by the Commission pursuant to section 30 of this Act to-

(a) accommodate joint interests and activities of all farmers on an irrigation scheme; and

(b) ensure increased crop production and productivity through optimal management of land, irrigation water and operation and maintenance of their scheme.";

**B:** In Clause 3, by deleting-

(a) the word "do" appearing in sub-clause (3)(d) and substituting for it the word "doing";

(b) the provision of sub- clause (8) and substituting for it the following:-

"(8) In exercising powers under subsection (6), the nominating authority shall-

(a)

nsure that the nominated person has adequate knowledge and competence in his respective profession;

(b) nominate a principal officer; and

(c) take into account gender balance."

**C:** In Clause 5 (2), by deleting-

(a) article "the" appearing between the words "in" and "national" in the first line of paragraph (b);

(b) the words "carryout studies" appearing between the words "plan" and "design" in the first line of paragraph (f), and substituting for them the words "carry out studies";

(c) the word "the" appearing between the words "in" and "irrigation investment" in paragraph (g), and inserting immediately after the word "support" the word "the";

(d) the words "capacity of the irrigator" appearing in the first line of paragraph (k) and substituting for them the words "capacity of irrigators";

(e) the word "facility" appearing in the second line of paragraph (m) and substituting for it the word "facilities";

(f) the words "overseeing collaborations" appearing in the second line of paragraph (n) and substituting for them the words "to oversee collaboration";

**D:** In Clause 6, by deleting sub-clause (2) and substituting for it the following-

"(2) The size, functions, terms and conditions of such committees shall be as may be determined by the Commission."

**E:** In Clause 7, by deleting sub-clause (1) and substituting for it the following new sub-clause:

"(1) The common seal of the Commission shall not be affixed to any instrument except in the presence of the Chairman or the Director General, or in their absence, by an authorized officer of the Commission and two members of the Board.";

**F:** In Clause 8, by deleting-

(a) in sub-clause (1), the words "who possess high level of" and substituting for them the word "with";

(b) sub-clause (3) and substituting for it the following:

"(3) For the proper discharge of functions under this Act, the Director General may assign any function provided herein to any authorized officer.";

(c) the word "function" appearing in the first line of sub-clause (4) and substituting for it the word "functions";

**G:** In Clause 9, by deleting the word "efficient" appearing in the fourth line and substituting for it the word "efficiently";

**H:** In Clause 10, by deleting the word "services" appearing in the third line of sub-clause (3) and substituting for it the word "service";

**I:** In Clause 11, by-

(a) deleting the words "Regional Irrigation Managers" appearing in sub-clause (1) and wherever they appear in the Bill and substituting for them the words "Regional Irrigation Engineers";

(b)
eleting the word “irrigation” appearing between the words “of” and “potential” in paragraph (b) of sub-clause (2);

(c) deleting the word “formulation” appearing in paragraph (f) of sub-clause (2) and substituting for it the word “formation”;

(d) deleting the words “rain water” appearing in paragraph (i) of sub-clause (2) and substituting for them the words “surface water”;

(d) adding the following new paragraphs immediately after paragraph (p) of sub-clause (2):-

“(q) to coordinate activities of the Commission and District Authorities on the enforcement of this Act;

(r) facilitate promotion, development, fostering and upholding of local government authorities towards realization of their goals and targets pertaining to irrigation development;

(s) advise the Director General on the implementation of this Act;

(t) facilitate the designation of the District Irrigation Offices in their areas to foster irrigation development and management; and

(u) perform such other functions as may be entrusted to them by the Commission for the better implementation of this Act.";

**J:** By deleting provisions of clause 12 and renumbering clauses 13 to 77 as clauses 12 to 76 respectively;

**K:** In Clause 12 as renumbered, by-

(a) deleting the words "Irrigators' Association" appearing in paragraph (g) of sub-clause (4) and substituting for them the words "Irrigators' Organizations";

(b) adding immediately after sub-clause (5) the following new sub-clauses:

"(6) In performing functions under this Act, the District Irrigation Engineer shall, when dealing with all technical issues relating to irrigation, be accountable to the Commission.

(7) Every Local Government Authority shall facilitate establishment and operation of the District Irrigation Departments and ensure that all allocated resources are effectively utilized so as to achieve objectives of this Act.";

**L:** In Clause 13 as renumbered, by deleting sub-clause (2) and substituting for it the following:

"(2) Any person appointed or designated as Inspector under subsection (1), shall be given a certificate, identity card or a document as showing proof of his

appointment or designation which shall be produced in the exercise of his powers under this Act.”;

**M:** In Clause 14 as renumbered, by-

(a) deleting sub-clause (3) and substituting for it the following new sub-clause:-

“(3) An Irrigation Inspector may, if he has reasonable grounds that any of the provisions of this Act or regulations or orders made under this Act have been violated, seize any property or material which is connected to such violation or issue a stop order against any action to which the violation was committed.”;

(b) adding immediately after sub-clause (4), the following new sub-clause:

“(5) The Minister shall determine the appeal within twenty one days from the date of receipt of such appeal.”;

**N:** In Clause 20 as renumbered, by-

(a) designating clause 20 as renumbered as clause 20(1);

(b) deleting sub-clause (2) and substituting for it the following:-

“(2) Any person other than the Commission who wishes to construct irrigation works in any irrigation area shall first apply for the approval of the Director General or any authorized officer acting on his behalf pursuant to the procedures

prescribed in the regulations made under this Act.”;

(c) deleting the word “and” appearing at the end of paragraph (f) of sub clause (3) and adding immediately after paragraph (f) the following new paragraph:-

“(g) detailed feasibility study report; and”;

(d) r enaming paragraph (g) as paragraph (h);

**O:** In Clause 28 (2) as renumbered, by deleting-

(a) the words “for the management of irrigation scheme” appearing in paragraph (a);

(b) the words “ for effective monitoring and management of irrigation schemes” appearing in paragraph (c);

(c) the words “for the proper management of irrigation schemes” appearing in paragraph (d);

(d) the words “necessary for the betterment of irrigation scheme management” appearing in paragraph (o);

**P:** In Clause 29 a renumbered, by deleting sub-clause (1) and substituting for it the following:-

“29.-(1) The Commission shall, in collaboration with the local government authorities, facilitate establishment of the irrigators’ organizations with due consideration of layout of a particular irrigation scheme.”;

**Q:** In Clause 31 as renumbered, by deleting the word "disputes" appearing in paragraph (i) and substituting for it the word "dispute.";

**R:** In Clause 34 as renumbered, by inserting the word "have" between the words "shall" and "regard" appearing in sub-clause (2);

**S:** In Clause 35 as renumbered, by deleting sub-clause (1) and substituting for it the following:

"35.-(1) In order to minimize water and land conflicts on irrigation schemes, the Commission shall collaborate with the local government authorities, basin water boards and respective irrigators using water from the same source and establish a mechanism for amicable settlement of disputes within the schemes through involvement of relevant government institutions or systems.";

**T:** In Clause 38 (2) as renumbered, by deleting the figure "1" appearing between the words "subsection" and "the Commission" in the first line and substituting for it the figure "(1)";

**U:** In Clause 39(1) as renumbered, by deleting the word "and" appearing between the words "prescribe" and "irrigation" in the third line;

**V:** In Clause 40 as renumbered, by deleting-

(a) the word "as" appearing at the beginning of paragraphs (a) and (b) of sub-clause (1);

(b) the word "he" appearing in the fourth line of sub-clause (2) and substituting for it the words "the Irrigation Inspector";

**W:** In Clause 41 as renumbered, by deleting the words "rats or other vermin" wherever they appear in that clause and substituting for them the word "pests";

**X:** In Clause 45 as renumbered, by deleting-

(a) paragraph (a) of sub-clause (1) and substituting for it the following:

"(a) occupy or encroach an irrigation area for purposes other than irrigated agriculture.";

(b) the word "to" appearing between the words "not" and "block" in paragraph (c) of sub-clause (2);

**Y:** In Clause 46 as renumbered, by deleting sub-clause (4) and substituting for it the following:

"(4) Any person who is aggrieved by orders of an inspector under sub-section (3) may, within fourteen days from the date of receipt of the order, appeal to the Minister.

(5) The Minister shall determine the appeal within twenty one days from the date of receipt of such appeal.";

**Z:** In Clause 50 as renumbered, by deleting sub-clause (2) and substituting for it the following:

"(2) Any person who pollutes or causes to be polluted any irrigation works commits an offence and

upon conviction, shall be liable to a fine of not less than one million shillings or to imprisonment for a term of not less than six months or to both.";

**AA:** In Clause 52 as renumbered, by -

(a) adding the words "sources of" between the words "The" and "Irrigation" appearing in the opening words of sub-clause (2);

(b) adding a new paragraph (c) immediately after paragraph (b) as follows:

"(c) funds accrued from disposal of obsolete plants and equipments";

(c) renaming paragraphs (c) to (f) as paragraphs (d) to (g) respectively;

**BB:** By deleting clause 54 as renumbered and renumbering clauses 55 to 76 as re-numbered as clauses 54 to 75 respectively;

**CC:** In Clause 54 as renumbered, by deleting sub –clause (4);

**DD:** In Clause 67 as renumbered, by deleting the words "stakeholders meeting" appearing in the marginal note and substituting for them the words "stakeholders forum";

**EE:** In Clause 74 as renumbered, by deleting-

(a) paragraph (g) of sub-clause (2) and substituting for it the following:

"(g) provide for the formation, functions, conduct and procedures of irrigators' organizations;";

(b) the word "prescribe" appearing in the second line of paragraph (q);

**FF:** In the Schedule-

(a) by deleting the words 'their number" appearing in paragraph 1 and substituting for them the words "themselves";

(b) in paragraph 2 by inserting the word "for" between the words "excuse" and "three" appearing in the fourth line;

(c) in paragraph 3, by-

(i) deleting sub paragraph (1) and substituting for it the following:

"The Commission shall meet at least three times in a year.";

(ii) inserting the words "in his absence" between the words "or" and "the" appearing in the second line of sub-paragraph (2);

(d) in paragraph 5 by deleting the word "rot" between the words "shall" and "have" appearing in the third line and substituting for it the word "not";

(e) by deleting paragraph 6 and substituting for it the following:

"(6) A member who has any interest, direct or indirect in any matter coming before the Commission or Sub-Committee shall, as soon as

is reasonably practicable, disclose the nature of that interest to the meeting and shall not thereafter take part in any decision on that matter nor, except with the consent of a majority of the members present at that meeting, take part in any deliberations relating to that matter."

Dodoma,
**CKC**
28th August, 2013
**MAFC**

**MWENYEKITI:** Tunakwenda *clause* ya pili, Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi kuhusiana na alicho-*raise* Mheshimiwa Mpina?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, neno hilo limetumika mara moja tu katika Muswada mzima. Maana ya neno *Qualified Irrigation Engineer,* ukisoma katika Muswada lilikuwa linataka kuzungumzia *Irrigation Inspector*. Kweli lilikuwa lina-*qualify*mtu ku-*qualify* kuwa *Inspector* wa *Irrigation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo ni kwamba, naomba nimwombe Mheshimiwa Mpina tu alielewe kwamba lilikuwa linataka kutoa ni sifa gani za Mhandisi wa Umwagiliaji atakaye-*qualify* kuwa *Irrigation Inspector*. Kwa maana hiyo ina maana kwamba basi tutakapokuwa tunatunga kanuni si kila Mhandisi wa Umwagiliaji atakuwa *Irrigation Inspector*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaweka taratibu ili labda kuwe na mafunzo au maelekezo maalum ili mtu fulani aweze ku-*qualify,* sio kuwa *Irrigation Engineer,* kuwa *Irrigation Inspector.* Yeye ni *Irrigation Engineer* lakini sasa a-*qualify to become an Irrigation Inspector*. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mpina alielewe hivyo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kama ndiyo hivyo, kwa sababu katika hizi tafsiri za *engineers* hawa, kwenye Sheria hapa namwona yule *Inspector Engineer,* lakini kama ndiyo hivyo ingetafsiriwa, kwenye Sheria sijaona kama imetafsiriwa kuwa *Irrigation Engineer* ni mtu wa aina gani, basi naridhika na hoja yangu kuiondoa, lakini kama hiyo haijatafsiriwa basi ni lazima ijulikane kuwa, unapozungumza *Irrigation Engineer* anatakiwa kuwa na *qualifications* za namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mwisho wa siku, hii *proffesion* inaweza kuwa *compromised,* mwisho wake ikawa kwamba, mtu yeyote akawa–*defined* kuwa yeye ni *Irrigation Engineer*. Kwa mfano, unapozungumza Mhasibu, inajulikana ni mtu wa namna gani, ukizungumza *Economist* inakuwa *defined* ni mtu wa namna gani, sasa na hapa kwenye *Irrigation Engineer* kama huku kwenye Sheria haijawa *defined* basi *Irrigation Engineer* iwe *defined* na tuache ile *qualified Irrigation Engineer.*

**NAIBU WAZIRI, KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako, hapa kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, tulipokuwa tunazungumzia

hili suala la *qualified Irrigation Engineer* hata kwenye *Irrigation Engineering* yenyewe, *in general assumption* ni kwamba, ukitumia neno *Irrigation* na ukitumia *Engineer* linajitosheleza katika tafsiri yake na hatulitumii nje ya uelewa mwingine wowote zaidi ya huo, *that, you are an Engineer* lakini *you are qualified as an Irrigation Engineer* kwa maana kuwa wewe ni *Engineer* katika fani ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa upande wa Mwanasheria Mkuu kama kuna ziada. Suala hili tumelijadili sana kwenye Kamati, lakini hatukuona ulazima wa kuliweka pale kwa maana ya tafsiri maalum, haina tafsiri maalum nje ya kuwa *Irrigation Engineer*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatoa tafsiri ya maneno ambayo yanaleta ukakasi, nafikiri Mheshimiwa Mpina ana maana kama vile kwenye neno Profesa ni nani, unaweza kusikia Profesa Maji Marefu, kwenye Sheria tunaposema *Irrigation Engineer* inaeleweka kuwa ni *Engineer* aliye *qualify* kuwa *Engineer*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 3

**NDG. ANSELM L. MREMA – KATIBU MEZANI:** Kifungu hiki kina marekebisho ya Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa *Engineer* Mohamed Habib Juma Mnyaa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamad Rashid kuhusu hilo!

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, hii amendment ambayo tumependekeza, itapatikana kwenye *Water Resource Management Act,* lakini nashauri, ni vizuri iingizwe katika Sheria hii. Kwa hiyo, ningependa Mheshimiwa Waziri azingatie maombi yetu.

**NAIBU WAZIRI, KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa mabadiliko haya ni kwamba, Mheshimiwa Mnyaa alikuwa anataka *incorporation* ya matumizi ya maji kwenye masuala ya Nishati na Madini, yaingie hapa, lakini lake linasema kuwa baadaye kuna fikra kuwa labda hata matumizi ya maji ya *domestic consumption* yaingie humu tukasema hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo matumizi ya maji kwa upana wake na maelekezo yake *specific* yanatokana kwenye *Water Resources Management Act* ndiyo imeeleza vizuri zaidi kwa hiyo, tunasema tulikuwa tunachelea kui- *commit* Sheria hii kwenye maeneo mengine ambayo yana tafsiri pana zaidi na yanaweza kutumika.

Kwa hiyo, tukasema kuwa, kwa sababu kule kwenye *Water Resources Management Act* imejieleza vizuri na sisi mahitaji yetu kwenye *Irrigation* yana mipaka Fulani, yale mahitaji ya ziada yanatafsiriwa vizuri zaidi kwenye ile Sheria nyingine.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10

**NDG. ANSELM L. MREMA – KATIBU MEZANI:** Ibara zote za hapo juu zina marekebisho ya Mheshimiwa Waziri tu.

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 11

**NDG. ANSELM L. MREMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii ina marekebisho ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Mohamed Habib Juma Mnyaa na Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed!

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imejadiliwa sana kwenye Kamati na Waziri alisema hana pingamizi nalo, sasa atueleze ni kwa nini anakataa badiliko hili.

**NAIBU WAZIRI, KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa lililokuwa linazungumziwa ni

Ibara ya 11(3) inayozungumzia uteuzi wa hawa *Reginal Irrigation Managers* waweze kutoka kwenye sehemu yoyote. Kwa hiyo, tukasema kuwa kwa mwanzo huu misingi ya *Human Resource base* tuliyonayo nyingi kwenye masuala ya *Irrigation* inatokana na *Senior Public Officers,* lakini wawe na *relevant qualifications*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kamati tulikubaliana ili uteuzi huu usiwe kwa mtu yeyote, unajisikia kuwa huyu ni ndugu yangu mtoto wa mjomba, nimpe u- *Regional Irrigation* hapana!

Tumesema kwanza wawe na *relevant qualifications,* lakini kwa sababu miradi yenyewe *base* yao kubwa iko kwenye Public Serivice, wawe watoke miongoni mwa *Senior Public Officers* lakini *with relevant qualifications* hata kwenye *Public Service* wasitoke kokote tu.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri.

**MHE. LUHAGA. J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hoja ambayo inafanana sana na ya Mheshimiwa *Engineer* Mnyaa, lakini hatuna sababu yoyote ile ya msingi ya kung'ang'ana kwamba hawa *Regional Irrigation Officers* watokane na *Senior Public Officer;* kuna vijana wengi waliosoma sasa hivi hawako kwenye *field* wanasubiri ajira, tunao wataalam wengi ambao leo wako katika *private sector* wanafanya kazi nzuri tu kuliko hata watu ambao tunao Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kutunga Sheria za ubaguzi, nadhani siyo kuwatendea haki Watanzania ambao wako *competent* na wanayo nafasi ya kulitumikia Taifa lao, lazima Sheria ifungue mlango, hawa watu wa-*compete,* tupate mtu kwa uwezo wake siyo kwa uteuzi, kwa sababu hata huu uteuzi uta- *base* tu, kama ni suala la kupendelea liko vile vile, mtu atakayeteua hapa naye ni binadamu atapendelea vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tu–*base* kwenye *competence* za watu, tu-*base* kwenye uwezo wa watu, itisha *interview,* wa-*asses* watu hao uwezo wao wa kuchanganua mambo na namna ya kukusaidia wewe Mheshimiwa Waziri, kwa nini ujifungie kwa Sheria? Fungua Sheria, waruhusu watu waingie, upate mtu mzuri, kwani lengo hapa ni kupata mtu mzuri na siyo mtu atoke wapi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na dhana ya kuwapata watu wenye uwezo kwenye kazi hizi na tunaanza na kifungu cha 3(2) kinachosema kuwa: "*The commission shall be an independent Department of the Government under the Ministry responsible for Irrigation*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa masharti ya ajira ya watu hawa, ni masharti yale ya ajira katika kazi za Utumishi wa Umma na naomba kueleza wazi, inawezekana wengine hawafahamu kwamba, hakuna kinachomzuia mtu kuteuliwa kutoka nje, kwa sababu atakapokuja ndani atakuwa ni *Public Officer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala hili la kugombea, katika utaratibu wa kuteua watu wa aina hii kuna mchujo na kila mtu anafahamu, mlioko Serikalini na ambao mmewahi kuwa Serikalini, katika uteuzi halipelekwi jina moja tu, hata mimi hapa halikupelekwa jina moja, nilikuwa na wagombea wenzangu. Ndivyo ilivyo katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshawishi Mheshimiwa Mpina, katika hili alilolisema kwamba, kwa sababu mapendekezo yake yanasomeka: "*A person shall not be recommended for appointment as a Regional Irrigation Manager unless he possesses the necessary qualifications as an Irrigation Engineer.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukisoma hapo na mapendekezo yaliyoko kwenye Sheria kuwa *a Regional Irrigation Officer shall be appointed from amongst senior Public Officers with relevant qualifications, experience, skills and competence in irrigation development.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma haya utaona kwamba, sifa hizi ni nzito kuliko hizi ambazo zinaelekea kwenye *qualifications* peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu *qualifications* peke yake ni kwamba, mtu amemaliza shule leo ana *qualification, is an Engineer,* lakini hana *experience, skills and not competent* kwenye *field* hiyo, kwa hiyo ninafikiri vile zilivyo kwenye Muswada ni kubwa zaidi, lakini *issue* ya kusema kuwa, tufungue mlango hata *private sector* waingie, ni *issue* nzuri, lakini tukumbuke kuwa tayari

tumeshabana pale kuwa, *this is the independent Department of the Government under Ministry responsible for Irrigation*. Kwa hiyo, nashauri tukubaliane kwamba, kifungu kilivyo, kibaki kama kilivyo.

**MWENYEKITI:** Sasa nimefika mahali pa kuhoji *unless* Mheshimiwa Mpina kama unakubaliana na Serikali kama hukubaliani nataka kuhoji.

**MHE. LUHAGA. J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na hoja ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Basi naomba kuwahoji Waheshimiwa Wabunge mtuongoze, hoja iliyoko mezani ni ile ya mabadiliko yaliyoletwa na Mheshimiwa Mpina.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Marekebisho ya Mheshimiwa Luhaga Mpina yalikataliwa na Bunge)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 12

**NDG. ANSELM L. MREMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 12 kinafutwa na Mheshimiwa Waziri na kufanyiwa *renumbering* kutoka kifungu cha 13 – 77 kuwa kifungu cha 12 - 76.

**MWENYEKITI:** Mabadiliko hayo yanaafikiwa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

Ibara ya 12

**NDG. ANSELM L. MREMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 12 ina marekebisho.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 13

**NDG. ANSELM L. MREMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 13 ina marekebisho ya Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina marekebisho yako katika Ibara ya 13 yanahusu nini?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawaje upigaji wa kura sijui matokeo yake kama ndiyo yanakuwa halali kwa utaratibu huo, lakini niendelee kwa nafasi uliyonipa sasa hivi. Marekebisho yangu yanahusu...

**MWENYEKITI:** Moja ya makosa makubwa ni kutokuwa na imani na Kiti Mheshimiwa Mpina, endelea!

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa na mashaka ni lazima useme, kuliko kunyamaza wakati una mashaka na kile kilichoamuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, marekebisho yangu ya pili ni kuhusu huu uteuzi wa *Irrigation Inspector* na Sheria imesema vizuri sana pale katika Ibara ya 14(1): "*The Commission shall, upon the recommendation of the Director General and by the notice published in the Gazette, appoint or designed the qualified Irrigation Engineer"* sasa maneno yanayofuata pale "*or any other officer from Regional Offices or under the Local Government Authorities*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiweka Sheria ya namna hii, unataka kuweka Mkaguzi wa kuwakagua Wahandisi wa Umwagiliaji, halafu ukasema *any person*, sasa *any person* mwenye *qualifications* zipi? Pia ukasema kuwa Afisa yeyote atoke Mkoani au Wilayani, nadhani pale utakuwa ume-*water down* kabisa Sheria yenyewe, ni bora hata ingebaki kuwa huyu ni *qualified Irrigation Engineer* ndiyo huyu unayempa mamlaka ya kwenda kufanya ukaguzi wa kuwakagua Wahandisi wenzie na siyo mtu mwingine yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachwa uchochoro huu, tutateuliwa watu wa ajabu wa kwenda kuwakagua Wahandisi ambao hawana *professional* ya Kihandisi yenyewe, wataingilia *professional* za watu na tutasababisha mgogoro mkubwa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunatunga Sheria? Kwa hiyo, hapakuwepo hata sababu ya kuandika hapa *qualified Irrigation Engineer,* kwa maelezo haya yaliyofuatia baadaye, kuwa ni *any person*. Kwa hiyo, ingawa naona kura ya Waziri inashinda mara kwa mara ukisema ndiyo na hapana, lakini hebu angalia *essence* ya kitu chenyewe, *or any person,* tutakuja kuchaguliwa watu wa ajabu kusimamia shughuli muhimu. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuepuka *ambiguity,* tunaweza kukubaliana na Mheshimiwa Mpina, lakini Kanuni za tafsiri ya maneno ya Kisheria, yana maana kwamba, ukimtaja Sheikh, halafu ukawataja na wale wengine wadogo.

**WABUNGE FULANI:** *(Hawakusikika)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Utamwondoa Sheikh Mkuu au ukimtaja *Sister* ukamtaja na Bruda, ukamtaja na Padri unamwondoa Askofu, ndiyo Kanuni ya tafsiri. Maneno yalivyo hayana ukakasi, lakini kwa sababu ya kuepuka hiyo *ambiguity,* naomba tuongeze maneno, baada ya *any other* tusiondoe hayo maneno. Tuseme *any other qualified Officer from Regional Offices or under the Local Government Authorities.* Nafikiri hii itakuwa ime-*cover concern* ya Mheshimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Hapo sawa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 14

**NDG. ANSELM L. MREMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii ina marekebisho ya Mheshimiwa Waziri.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 15

**NDG. ANSELM L. MREMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii ina marekebisho ya Mheshimiwa Luhaga Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hiyo inazungumzia juu ya mtu asiye na taaluma ya Ukaguzi wa Umwagiliaji kuingilia shughuli ya ukaguzi, lakini pale nimesema kuwa adhabu iliyotolewa ya *fine* ya milioni mbili ni ndogo sana, nikasema kuwa hii adhabu isiwe chini ya milioni tano, lakini yale maneno tena *but not exceeding ten million*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno yanaiharibu Sheria yenyewe, kwa sababu unapoweka kikomo hicho, wakati huo wewe hujui katika zoezi la yeye kuingilia shughuli ya ukaguzi na siyo Mkaguzi na hana *mandate* hiyo, hujui *damage* ambayo ataifanya kwa utapeli wake huo. Sasa unaposema *not exceeding ten million* maana yake ni kwamba unaifunga Mahakama, ishindwe kuangalia upana wa hasara ambazo zitasababishwa na huyu mtu ambaye ameingilia shughuli ambayo siyo ya kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri na kulishawishi Bunge lako likubali kuwa *not exceeding five million,* lakini pia ifungue, ile *ten million* iache, Mahakama itaamua kulingana na hasara ambayo huyu ataisababisha wakati anatekeleza ule utapeli wake.

**MBUNGE FULANI:** Iwe *not less than five million*.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Ndiyo, iwe *not less than five million* halafu yale maneno *but not exceeding ten million shillings* tunayaondoa, Mahakama itaona kulingana na ukubwa wa kosa, kulingana na hasara iliyojitokeza.

**MWENYEKITI:** Hebu kwa kifupi sana rudia tena unachokipendekeza hapo, ni nini?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokipendekeza iwe hivi: "*Any person not being qualified as Irrigation Inspector, who purports to act as Irrigation Inspector commits an offence and upon conviction shall be liable to a fine not less than five million...",* inaendelea, lakini maneno yale *but not exceeding ten million* yanaondoka na ile *two* inaondoka.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na hilo, isipokuwa naomba tufahamu tunachofanya, adhabu hii inayotolewa hapa siyo *compensation* kwa mtu aliyeathirika na vitendo vya huyu mtu ambaye siyo *qualified Inspector;* kama anataka

kupata *compensation* ya kutosha, ni lazima huyu mtu aliyeathirika aende Mahakamani kudai fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri niliweke hili sawasawa ili kusudi tufahamu tunafanya nini kwa sababu sisi tunatunga sheria na utungaji wa sheria ni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, hii adhabu ya mtu mmoja ni adhabu ya Kaizari, yaani mtu anayefaidika na fedha zinazotozwa hapa ni Serikali, kwamba zinakwenda Hazina, lakini wale ambao wana *scheme* zile kama wamepata athari nyingine ni lazima waende Mahakamani kudai *compensation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, nafikiri kwamba ile *qualification* ya *not exceeding ten million* inaweka *cap* kwamba katika kutoa adhabu basi Mahakama itoe kati ya milioni tano na milioni kumi, lakini kama mnaondoa yale maneno mimi sina tatizo, ila katika kutunga sheria tusiwe na hasira.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatunga sheria hapa zenye kuleta nidhamu kwa Watumishi wa Umma, wakati huo huo tena tunawakinga hawa Watumishi wa Umma na tunataka kuielekeza Mahakama. Kwa nini tunataka kuielekeza mahakama, sisi tu-*set* kwamba kulingana na adhabu hii Mahakama itatumia busara yake sasa, kutoka pale kwenye faini ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendesha kesi ambazo hata wakati mwingine tunajikuta, hili ni kosa kubwa la mtu kujifanya Mkaguzi akaingilia mamlaka zetu, huwezi ukajua

alifanya hivyo kwa ku-*intend* kitu gani. Kwa hiyo, tunapoweka adhabu kali tunawashawishi hawa watu kuacha kufanya makosa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hili kosa ni miongoni mwa makosa makubwa mno, kosa la watu kujifanya Wakaguzi kwa sababu si kwamba ni mtumishi tu amejifanya kuwa mkaguzi, ni mtu kutoka nje ameamua kufanya kazi hiyo kwa nia yake yeye mwenyewe anayoijua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili ni kosa kubwa mno ambalo hatuwezi tukali-*entertain* mpaka tunamwekea na *cap* kwamba eti isizidi milioni kumi. Kwa nini tunasema hivyo? Anaweza kutozwa hata zaidi ya hapo kulingana na makosa hayo ili mtu mwingine anayefikiria hivyo na anayetarajia kufanya hivyo, asifanye kabisa, sasa kwa nini tunamwekea kinga?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kabla hamjafika mbali, yapo mambo ni ya kubishania, yapo mambo unapata *professional advice*. Tunachokipata hapa ni ushauri wa kitalaam wa uzoefu na kadhalika. Ni vizuri kuweka *minimum* na *maximum,* ndiyo ushauri ambao tunaupata hapa.

Ushauri wa Mheshimiwa Mpina wa kusema acha tu, Mahakama ni binadamu kwamba Hakimu wa Mtwara ataamua anavyojua, Hakimu wa Kilimanjaro ataamua anavyojua, wa Bukoba hivyo hivyo, sasa sijui, labda Mwanasheria Mkuu fafanua vizuri zaidi.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu una *core* mbili na nilishakubali kwamba yale maneno yanaweza kutoka, nilichokuwa nasema ni angalizo tu. Kwa hiyo, ukiondoa yale maneno *but not exceeding ten million shillings,* ume-*enhance* ile *two million* kuwa *five*, *is just ok*, halafu yanayobaki yanaendelea sawasawa, sina ugomvi na hilo.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo kwa maana ya kwamba yanasomekaje sasa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inasomeka: "*Any person not being qualified as a Irrigation inspector, who purports to act as Irrigation Inspector commits an offence and upon conviction shall be liable to a fine not less than five million or to imprisonment for term of less not than two years, but not exceeding three years or to both such fine and imprisonment*.

**MWENYEKITI:** Kinachoonekana wanaongea lugha moja.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 16

**NDG. ANSELM L. MREMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 16 ina marekebisho ya Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mheshimiwa Selemani Jafo.

**MWENYEKITI:** Ibara ya 16 tuanze na Mheshimiwa Jafo.

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. SELEMANI SAID JAFO, MEMBER OF PARLIAMENT FOR KISARAWE CONSTITUENCY, AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE NATIONAL IRRIGATION ACT, 2013"**

***[Made under Standing Order 86(9) & (11)]***

A Bill entitled "The National Irrigation Act, 2013" is amended in Clause 16 as renumbered, by deleting words "the holder of such land shall be entitled to compensation in accordance with the relevant land law or as may be agreed upon" appearing in sub-clause (5) and substituting for them the following new words:

"the holder or holders of such land shall be entitled to be shareholder or shareholders to any project which shall be developed in such land as may be agreed upon".

Dodoma HON. SELEMANI SAID JAFO (MP)
30th August, 2013 **KISARAWE CONSTITUENCY**

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kifungu hicho kinaelekeza kwamba, pale ambapo eneo limekuwa *declared* kiasi kwamba hapa naweza nikasema ndiyo roho ya Muswada huu tunaokwenda kuujadili mchana huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, eneo likiwa *declared,* wale watu ambao wanaathirika pale watakuwa *liable* kupata *compensation*. Lakini hali halisi ilivyo ni kwamba, maeneo haya ambayo wananchi wanalima hivi sasa, ndiyo maeneo ambayo wao wameyarithi na ni kwa ajili ya uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kwamba, baada ya kupata *compensation,* pendekezo langu kubwa ni kwamba, wale watakaokutwa katika eneo lile, wawe ni *shareholder* wa hiyo *project* itakayoendelea hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapai ndiyo tutakuwa tunaleta maana nzima ya *irrigation* kwa ajili ya kumkomboa Mtanzania. *Otherwise* tukiacha kwa mujibu wa Serikali ilivyoleta hapa ina maana kwamba tunakwenda kuwatengenezea ulaji watu. Tukimpata mtu ambaye ni mwehu, amepewa madaraka hayo kama Kamishna, kitakachotokea ni kwamba, atakuja kufanya maamuzi ambayo yatakuja kuwaathiri watu wengi sana katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikasema kwamba *shareholder,* katika kitu ambacho nimesema tuna *delete*, nimesema kwamba *delete the word the owner of such land, shall be entitled to compensation in accordance with relevant law, land law or as may be agreed upon*. Nikasema iwe *substitute to the holder or shareholder of such land, shall be entitled to be shareholder or shareholders to any project which shall be developed in such land as may be agreed upon.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana hata wale watu watakaokuwa katika eneo lile wawe ni miongoni mwa ambao ni wanufaika wa hiyo *project* ya *irrigation*, kuliko kwamba tumechukua hiyo ardhi, wananchi wanaitegemea ardhi ile, wameondolewa, anakuja mtu anawekeza, maana yake atakuwa siyo *part* ya hiyo *project*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wabunge wenzangu wote waniunge mkono katika hili kwa ajili ya kulinda maslahi ya Watanzania tunaowawakilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina hapo hapo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri ana-*wind up,* pale alipokuwa akizungumza kwamba, hii sheria haijawanyang'anya wananchi ardhi, alikuwa hasomi Ibara ya 17(5), ukiisoma Ibara ya 17(5) ukasoma na Ibara ya 4(1), ukasoma na Ibara ya 17(1) na ukasoma na Ibara ya 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 17(5) inasema: "*Where any declaration referred to in sub-section* (1) pale ambapo Waziri imempa *mandate* ya kufanya *declaration* ya *irrigation area, affects the existing land rights, the holder of such land shall be entitled to compensation in accordance with the relevant land law or as may be agreed upon.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifungu hiki moja kwa moja kwa maana ya kwamba kuna *lines* mbili hapa, kuna *line* kwamba *declaration* inaweza isi-*affect land rights*, lakini *line* ya pili *declaration* inaweza ika-*affect land rights*. Sasa *when it affects land rights* hawa wananchi tumewa-*protect* namna gani kuhusu ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hicho ambacho Waziri alikuwa hakizungumzi, anasema tu kwamba, hii sheria haijachukua ardhi ya mtu, lakini ukisoma hapa ni kwamba, wameshachukua ardhi ya mtu na wamelipa fidia kwa mujibu wa kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kifungu hiki kiwe sawa, naomba sasa kisomeke ifuatavyo:

"*Where any declaration referred to in subsection one affects the existing land rights,* yaongezeke maneno yafuatayo: *the commission or any person shall collaborate with the shareholder of such land*, nafuta yale maneno mengine yote pale, *shall be entitled to compensation in accordance with the law of land*, yale yote unayafuta mpaka pale kwenye neno *as may be agreed*, yote unayafuta na una-*replace* na neno *in investment in irrigation development*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kifungu hicho kinasomeka chote kwa pamoja kwamba: "*Where any declaration referred to in sub section (1), affects the existing land rights the Commissioner or any person shall collaborate*

*with the holder of such land in investment in irrigation development.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale sasa utakuwa moja kwa moja umewashirikisha wananchi wenye ardhi kwa kumlazimisha mtu yeyote yule atakayekuja kwenye ardhi yao, kushirikiana na wao katika kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji na siyo kuiacha kama ilivyokuwa imeachwa hapa.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nilitumia muda mrefu kidogo pale kwamba, nadhani bado kuna dhana ambayo haijaeleweka hapa. Unajua hata ilivyo sasa hivi, eneo lolote ambalo kwa mujibu wa sheria linaweza likachukuliwa kwa ajili ya manufaa mapana ya umma, linaweza likachukuliwa, lakini linapochukuliwa ni kwa ajili ya wale watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukija kwenye kutangaza eneo la umwagiliaji, naomba hapa ndiyo ni-*define* vizuri, eneo tulilolisema kama la umwagiliaji ni pamoja na *headwork's* (miundombinu). Kwa mfano, tunataka kuanzisha mradi mkubwa wa umwagiliaji, tunajenga bwawa, tuta, tuta lile litakuwa na bwawa, halafu kutakuwa na mifereji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yote haya hatuyafanyi kwamba, sasa tunamnyang'anya yule mtu, hii *development* inafanywa kwa ajili ya hao watu, wakulima wadogo wale wale. Kwa maana hiyo miundombinu yenyewe hiyo ni ya kwao isipokuwa sasa huwezi ukasema

kama mfereji unatakiwa upite hapa, nimpe mfano mdogo tu, kuna wakati unaweza kusema mfereji upite hapa, huo mfereji unafukua makaburi ya watu na mimi nimekuwa *Irrigation Engineer* wa miaka mingi, unakuta kwamba watu wale wanashirikishwa, wanasema mfereji lazima upite hapa kwa sababu ya manufaa mapana, lakini hebu tuchinje ng'ombe, mbuzi na kadhalika ili hii mifupa ifukuliwe tena iwekwe mahali pengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama kwa mfano, mtu alikuwa na nyumba, alikuwa na mali nyingine ambazo zina thamani kubwa lakini kwa manufaa ya wale watu ambao watafaidi mradi huo wa umwagiliaji, ndiyo watapata *compensation* kulingana na hicho alichopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilivyokaa hivi, sidhani kama inatofautiana na sheria zingine zozote, ndiyo maana nimesema: "*Where any declaration referred to in subsection (1), the existing land rights.* Zipo Sheria za Ardhi, siyo kwamba *we re-inventing the rule* au sheria nyingine mpya.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri mimi na Waziri siyo Wanasheria, lakini asome vizuri sana Ibara ya 17 na Ibara ya 17(5) ninayoizungumza. Aliposema tu *where any declaration affects*, hapa wananchi umewataifisha ardhi yao, sisi kama Bunge tunasema, hii ardhi ya wananchi tunaukaribisha umwagiliaji kwa nia njema kabisa uje, lakini wakati huo huo tukiwalinda wananchi wetu wasipokonywe ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa anapozungumza kuna suala la *compensation* tu, inapo-*affects land rights*

kuna suala la *compensation* na sisi tunataka tumboreshee zaidi Muswada wake kwamba utaje moja kwa moja. Kwa sababu unapo-*declare land,* mimi ni Mhasibu na maana ya sheria hii Waziri anapo-*declare land,* hakuna uwekezaji wowote, nadhani hapo ndiyo hakuna madhara kwa huyu mwananchi anayeishi kwenye ardhi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini anapo-*declare land* kwamba hii ni kwa ajili ya *irrigation,* akapata wawekezaji, kwenye Ibara ya 4(1) ameshasema ni nani anayewekeza, amesema anayewekeza ni Tume. Kwa hiyo moja kwa moja inapofika sasa Mwekezaji amepatikana kwa ajili ya eneo hilo, ndipo hapo mahali wananchi watakapoikosa haki yao, kwa sababu watakuja wawekezaji katika eneo hilo, mwananchi atalazimika sasa alipwe hizi *compensation* tunazozizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wananchi hawa tukianza kuwafanyia *compensation* watakwenda kuishi wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *compensation* leo ya hekari moja utaambiwa na Serikali shilingi milioni moja. Ukilipwa milioni moja katika maisha yako umeikosa ile ardhi. Naweza nikawa na mapato makubwa kutokana na ardhi yangu ambayo napata laki mbili kwa mwaka, lakini nitapata mimi mpaka na vizazi vyangu vinavyokuja katika ardhi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuondoe hiyo *notion* ya *compensation* katika suala la ardhi, isipokuwa wananchi wetu waishi kwenye ardhi yao, wakikutwa na umwagiliaji

wajipongeze kwamba kumbe nilikuwa naishi pazuri, nilikuwa namiliki ardhi yenye rutuba, ambayo sasa napata wawekezaji, tuwekeze nao pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma haya marekebisho niliyoyafanya, ndiyo yanakifanya kitu hicho cha kumhakikishia huyu mwananchi anamiliki ardhi yake kama kawaida, lakini atakapoingia kwenye ubia, ndiyo hapo *transit of ownership* itakapokwenda lakini itakwenda kwa *terms* za makubaliano ya kiuwekezaji.

**MWENYEKITI:** Nadhani tayari tumeshapata picha yako. Mheshimiwa Halima Mdee, halafu Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kifupi sana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mtoa hoja, kwa sababu uzoefu unatuonesha kwamba, eneo lolote ambalo lipo *prime* ambalo wanamiliki wazalendo, Watanzania, wazawa pasipo kujali rangi zao, anapokuja mwekezaji, Mswahili, ama Mhindi wa Kitanzania ama Mchina wa Kitanzania anaondolewa yule mwekezaji anawekwa na inalipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapotunga sheria hizi sasa, ni lazima tutengeneze utaratibu wa kulinda wazawa, sheria zinapokuwa haziko wazi, zina *loophole* tafsiri yake ni kwamba *loophole* hizo huwa zinatumika kuwanyanyasa wazawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nina-*recommend* kwa Serikali kwa sababu hatutarajii na nafikiria kabisa kwamba, isije ikawa hii Sheria ya Umwagiliaji imeletwa kwa

sababu ya ule utaratibu wa *SAGCOT* ambao utaratibu wa *SAGCOT* unamwangalia mkulima mdogo pembezoni mwa mkulima mkubwa. Sasa tusije tukawa tunatunga sheria hapa kumbe tunatungia Wachina na Wazungu na Waarabu wanaokuja kuchukua maeneo yetu *prime*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza wazo ambalo amelitoa Mheshimiwa Mpina la kulinda watu wetu ni muhimu. Lakini zaidi hata ukiangalia hiki kipengele cha tano, nasoma kile cha Kiswahili kinasema: "Iwapo azimio lolote linalotajwa katika kifungu kidogo cha (1), litaathiri haki za umilikaji ardhi, mmiliki wa ardhi hiyo anastahili fidia kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi, ama kadri ya makubaliano yatakavyokuwa yamefikiwa".

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu, licha ya kwamba napinga hilo suala la fidia kwa sababu litakimbiza watu, ama kadri ya makubaliano yatakavyokuwa yamefikiwa na yenyewe ni kichochoro cha wizi. Kwa hiyo, napendekeza na naunga mkono kabisa, mapendekezo ya Mheshimiwa Mpina na Serikali iangalie kwa maslahi ya Watanzania na siyo Wawekezaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista Mhagama, halafu Mheshimiwa Sendeka.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba naunga mkono kabisa mapendekezo ya Mheshimiwa Mpina ambayo yameongezewa uzito wa kutosha na mapendekezo yaliyosemwa na Mheshimiwa Jafo, Wabunge hawa wote

wawili wa Chama cha Mapinduzi. Pia namshukuru Mheshimiwa Halima ameunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, umwagiliaji huo utakuwa ni kwa ajili ya wananchi katika maeneo hayo hayo. Nakwenda Ibara ya 28, nimpeleke Ibara ya 27 kwa sasa, nimpeleke mbele ili nimwambie ni kwa nini tunajenga hii hoja ya umiliki wa Watanzania katika maeneo hayo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisoma ile ya Kiswahili Ibara ya 27 ambacho ni Ibara ya 28 kwa Muswada, kinataja makundi hayo ya wamwagiliaji watakaokwenda kukabidhiwa ardhi ya umwagiliaji baada ya *declaration* ya Mheshimiwa Waziri katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma makundi hayo ni yapi; ni mkulima binafsi, Vyama vya Wamwagiliaji, Vyama vya Wamwagiliaji inaweza kuwa ni wale wananchi pale, lakini kutakuja pia makampuni, ama taasisi za umma, mashirika ya dini, ama asasi zisizo za kiserikali au kikundi chochote kitakachotambuliwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hebu tuseme kwa mfano, labda leo kampuni ndiyo inaenda kumiliki ule umwagiliaji katika kijiji fulani ambako tayari lile eneo limeshachukuliwa na kuwa *declared* kwamba ni eneo la umwagiliaji, wale wazawa kama kutokuwa *shareholders* watafaidikaje sasa na ule mradi unaokwenda pale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Mpina ya kuwalinda wazawa wa Tanzania, kuwa na hisa katika mradi wa kwenye eneo lao, ni hoja ya msingi sana kwa manufaa ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi sana Mheshimiwa Ole-Sendeka na Mheshimiwa Ester mtakuwa wa mwisho. Kwa kifupi sana!

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kutamka kwamba naunga mkono pendekezo la Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Jafo kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huhitaji kusoma Muswada huu wote kupoteza muda mrefu kujua maudhui yenye dhamira ovu yaliyoko kwenye Muswada huu. Unahitaji kwenda kwenye kifungu cha (4) kifungu cha 17 na cha 18. Nami nataka niwaambieni, Kifungu cha (4) kinatoa mamlaka kwa Tume kuweza kuwekeza kwa ubia na mtu yeyote katika eneo.

Kifungu cha 17 kinatangaza eneo la umwagiliaji kwamba, Waziri mwenye dhamana na masuala ya ardhi anaweza kushauriana na Waziri na kwa amri itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali kutangaza kwamba eneo lolote lililoainishwa kwenye amri hiyo kuwa ni eneo la umwagiliaji kwa madhumuni ya Sheria hii.

Sasa akishatangaza, kifungu kidogo cha tano cha aya hiyo, inakuwa kama alivyosema Mheshimiwa Mdee pale; "iwapo azimio lolote linalotajwa katika kifungu kidogo cha kwanza litaathiri haki za umiliki wa ardhi, mmiliki wa ardhi hiyo atastahili fidia kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi, ama kadri makubaliano yatakavyokuwa yamefikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukienda kifungu kinachofuata, upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, utakuta kwamba Mawaziri hawa bila kushirikisha Serikali za Mitaa kwa maana ya Mkutano Mkuu wa Vijiji vinavyohusika, wanamshauri juu kwa juu Rais atoe ardhi ya wananchi katika bonde lolote, wao wawekeze na mwekezaji kwa mujibu wa kifungu cha (4) baadaye waitekeleze hisa za Serikali wamwachie huyo mwekezaji. *Room* hiyo ipo kwenye kifungu cha (4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiacha hicho, kuna habari ya kutoa fidia. Ukishatoa fidia, maana yake ardhi hiyo siyo yako tena. Nami nataka niwaambieni na niwaombe makada wenzangu walioko, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, nina imani kubwa na nyinyi; kuna agenda imejificha kwenye vifungu hivi na agenda hii ni kuwapeleka Watanzania kwenye utumwa, maana ardhi hii itachukuliwa na watapewa wageni na Serikali itajiingiza kwa mgongo kidogo na baadaye inaachia. Hivyo ndivyo kifungu cha (4) kinavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pendekezo la Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Jafo ninaliunga mkono kwa asilimia 100. Serikali iseme hapa, inabadilisha? Kama

Serikali haisemi, ondoa Muswada huu, Serikali ikarekebishe, uje upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili likiridhia Muswada huu kama ulivyo, maana yake Bunge hili limetumika kama kichaka cha kuwafanya Watanzania kuwa wakimbizi kwenye ardhi yao. Vifungu hivi vinakwenda kinyume na Sheria ya Ardhi ya Vijiji na Sheria mama ya Ardhi. Kwa hiyo, wala haitambui hata Mikutano Mikuu ya Vijiji. Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI hana mamlaka na ardhi. Mwenye ardhi ni Mkutano Mkuu wa Kijiji na yale mabonde yako chini yao, na pale kuna Watanzania wanaishi. Ukiwaondoa wafugaji kwenye bonde hilo, ukalitangaza, halafu umlete mwekezaji kwa mlango wa nyuma, hii ni dhambi ya mauti. Msikubaliane na hilo Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya, karibu tafadhali.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kusisitiza yale ambayo yameshaongelewa na wachangiaji waliopita.

Kwanza, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Jafo. Napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri, alivyokuwa akijibu, anasema, hakuna ukakasi wowote. Ukakasi upo na ndiyo maana hata yeye anasita kukubaliana na mapendekezo ya Wabunge hawa moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu leo hii likubali kufanya mambo mawili. Jambo la kwanza, kulinda

ardhi ya Watanzania au kuuza ardhi ya Watanzania kwa wageni na kurudisha ukoloni mamboleo katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *trend* ya kwenda ku-*invest* kukaribisha wageni halafu kuwaondoa wazawa kwenda katika maeneo mengine bila kunufaika na mradi ambao unakwenda kwenye eneo husika, Bunge hili leo linasema hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshindwa kunufaika katika rasilimali nyingine. Tegemeo kubwa la Watanzania ni ardhi, na tegemeo kubwa ni hii *project* tunayoipitisha ya kilimo cha umwagiliaji, ambacho kitamnufaisha Mtanzania, mdogo mdogo na hakitaweza kufanya hivyo kwa kuridhia Sheria hii kupita bila kufanyiwa marekebisho ambayo yameletwa na Wabunge wenzetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunachokisema hapa ni kulinda mali za Watanzania. Ni kulinda ardhi ya Watanzania ambayo Mheshimiwa Mugabe naye alikataa! Tusiingizwe changa la macho kukubali tu eti ni makubaliano ya nchi za *SADC.* Hapa ni lazima tukatae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na Mheshimiwa Mpina na

Mheshimiwa Jafo, lakini naomba kufanya marekebisho ya mapendekezo yao kama ifuatavyo:- *(Makofi)*

Kwenye kifungu kidogo cha (5) ambacho kilikuwa zamani kifungu cha 17 sasa ni cha 16, kifungu cha (5) ukurasa wa 21, nilikuwa nasema naomba Waheshimiwa Wabunge, sauti imesikika: "*where any declaration referred to in Sub-Section (1), ya 16 (1) affects the existing land rights the holder of such land shall be entitled to compensation in accordance with the relevant land law or as may be agreed upon." Provided,* haya ni maneno naongeza na nachukua maneno yote ya Mheshimiwa Jafo. '*Provided'* hilo ni neno langu, maneno yote mengine yanabaki ni ya Mheshimiwa Jafo.

*"Provided that the holder or holders of such land shall be entitled to be shareholder or shareholders to any project which shall be developed in such land as may be agreed upon."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia. Kwanza, nifafanue furaha yangu niliyonayo leo kwamba Bunge sasa limekuwa ni *debating chamber,* yaani mahali ambapo watu wanatumia akili zao barabara. *(Makofi)*

Kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Halima Mdee, maneno yake yale mazuri sana alivyounga mkono wenzetu hawa. Sasa nasema hivi: "*provided that the holder or holders of such land shall be entitled to be shareholder or shareholders to any project which shall be developed in such land as may be agreed upon*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Waheshimiwa Wabunge, naomba mniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa Mpina umesimama. Kwa kifupi sana tafadhali. Naona mnaongea lugha moja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kabisa hatujaongea lugha moja, kwa sababu hatutaki hata kuwaruhusu wananchi wetu ku-*negotiate* na *investor* kwa ajili ya kuuza ardhi yao. Kwa hiyo, ndiyo maana mapendekezo yetu haya yanataka kuwaondoa kabisa wao kwenye ku-*negotiate* suala *compensation* wala nini. Kwa hiyo, kwa jinsi alivyorekebisha kwa marekebisho yake yale, bado yanaruhusu *negotiation* na wananchi wetu bado hawajawa na uwezo sana. Ardhi yao itanunuliwa tu mtu akija na pesa. Kwa hiyo, tunataka tufunge huo mlango wa kuuza ardhi kwa namna yoyote ile kwa mtu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafahamu kwamba hili suala ni la usimamizi wa Sheria. Kwa sababu, kwa wale waliosoma Sheria, *native* hawezi kuuza ardhi, bila *consent* ya *Commissioner for Lands. That is the law*. Labda Mheshimiwa Waziri ameeleza maudhui ya Muswada kwamba tunalenga wakulima wakubwa na wa kati. Wale wadogo, Serikali itafanya kazi ya kutengeneza miundombinu. Nafikiri ndivyo nilivyoelewa. Kwa hiyo, wakubwa na wa kati na miundombinu hiyo ni kwa sababu ya maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiwanyima ku-*negotiate* kwa msingi kwamba hawana uwezo, mimi sifahamu. Nyinyi ndio mnaotunga Sheria, lakini nilikuwa nashauri kwamba tuiache hiyo kwa sababu wanaweza ku-*negotiate* kupitia Halmashauri zao.

Mheshimiwa Ole-Sendeka nafikiri amesema vizuri. Nyinyi Waheshimiwa Wabunge wote ni Madiwani na miradi hii inatekelezeka kwenye maeneo yenu, kwa nini msiwasaidie hao wakulima? Itakuwa ni vigumu sana kuwanyima hawa Watanzania ku-*negotiate* haki zao. Kwa sababu sidhani kama wataendelea kuwa mbumbumbu kama tunavyowafikiria sisi na wengine sasa wanaanza kutumia hata Wanasheria.

Mheshimiwa Mdee, niunge mkono, unaweza kupata kazi kule kwenye... *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa kifupi sana tafadhali.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Mimi namwelewa sana *AG,* lakini ninachotaka kumwambia *AG,* bado kuna ukakasi. Hata yeye anaposema unaona kabisa na yeye anaona ule ukakasi bado upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunafikiri suala la *compensation* ni la msingi, mimi nafikiri tunapofika pale, "*where any declaration referred to in Sub-Section (1), affect the existing land rights, the holder of such land shall be entitled*," tuanze mu-*entitle* huyo kuwa *shareholder* ama

akitaka kuwa *compensated.* Labda tukiweka hivyo nitamwelewa *AG* na huo ukakasi utakuwa haupo. Lakini kuiweka hii ya kwake kama ilivyo, halafu huku chini sasa ndiyo aje na *provided*, Mheshimiwa *AG* ukakasi bado upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa *AG* atuelewe, na kama alivyotupongeza leo, tuna-*debate* Bungeni kwa maslahi ya Watanzania. Kama tuna-*debate* kwa pamoja kwa maslahi ya Watanzania, *AG please,* tuanze kuwaweka Watanzania kuwa *shareholders* kwanza kwenye ardhi zao, halafu kama kutatokea na mazingira ya kuwa-*compensate.*

Kwa hiyo, mimi nadhani hapa tukiweka hayo yote mawili, lakini tukianza, wanaweza kuamua, umesema wata-*negotiate.* Waki-*negotiate* kuwa *compensated is okay.* Lakini waanze kuwa *shareholders* halafu *after negotiation* wakiamua kuwa *compensated, is okay*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yote tukiyaweka hapo kwa utaratibu huo mzuri ni sawa. Lakini hiyo ya kuweka ya kwako *AG,* halafu ndiyo ije hii ya Mheshimiwa Mpina ama ya Mheshimiwa Jafo, hapana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyoona muda wetu hauko upande wetu, sasa Kanuni zinataka turudi kwenye Bunge tumwombe Mheshimiwa Waziri wa Nchi, tupate muda wa kushughulikia jambo hili mpaka tuelewane. Kwa hiyo, Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Kanuni ya Bunge itenguliwe kwa mujibu wa kifungu cha 28(2) ambacho kinaruhusu kwamba Spika akiona inafaa muda utaongezwa ili kumaliza shughuli iliyopo mbele yetu. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kwa hiyo, tutarudi kwenye utaratibu wa Kamati ya Bunge Zima halafu mpaka tumalize shughuli yetu na haitatuchukua muda mrefu sana.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri unataka kusema kitu? Tafadhali!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema tu kwamba ndiyo maana tuko humu ndani ya Bunge na ndiyo maana tukaleta Muswada ili tupate ushauri na michango ya watu. Hatuko kwa ajili ya kushindana tu kwamba nani atafanya

hivi. Lakini pia nilitaka niseme kwamba Muswada huu haukuletwa *specific* kwa ajili ya *SAGCOT.* Huu umeanza kutungwa hata kabla *SAGCOT* haijaanza kufikiriwa. Lakini ilikuwa tu inafikiriwa fikiriwa. Kubwa zaidi ni kwamba baada ya kutafakari, Waheshimiwa Wabunge ambao ndio Wawakilishi wa hawa wakulima, Serikali inakubaliana kabisa na hoja ya mabadiliko yaliyoletwa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasoma nyakati, kwamba Waheshimiwa Wabunge wanakubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Mhagama. *(Makofi)*

Kama ndivyo, kile kifungu cha (5) unajua inategemea unaiweka wapi. Ukiiweka kwenye *provisal* au ukiiweka katikati, lakini kwa sababu ya *compromise,* tuiweke katikati na itasomeka kama ifuatavyo:-

"*Where any declaration referred to in Sub-Section (1) affects the existing land rights, the holder of such land shall be entitled, if he wishes ('he'* hapa ina-*incorporate* pia *she) to be a shareholder or to be compensated in accordance with relevant land law or as may be agreed upon." (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, kwa kifupi sana.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo imekaa vizuri, lakini kuna maneno tu ambayo yatakuja

kutuletea ufisadi mkubwa tena mwingine upande wa Serikali. Kwa hiyo, "*or may be agreed upon"* hiyo tuiondoe. Kwa sababu hii itakuwa ni uchochoro mkubwa wa watu kusema tu kwamba tulishauriana tukakubaliana. Kwa hiyo, hii tuiondoe na baada ya hapo itakuwa imekaa sawa sawa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mungu Baba Mwenyezi! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua hili ni suala la nipe nikupe. Sasa ile nipe nikupe ndiyo hii ya *agreed upon,* kwamba wewe kama unakuwa *compensated,* unakuwa *compensated* kiasi gani? *Subject to negotiation!* Kama unataka kuwa *shareholder* huwezi kusema kwa vile unachukua hii, basi mimi nakuwa *shareholder.* Ni lazima tukubaliane kwamba, unaweka kiasi gani? Au *land value* yako ni kiasi gani? *That is the point* ya *negotiation.* Kwa hiyo, ni *agreed upon. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri haina shida sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafo.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa usikivu wa Serikali kwa hoja tulizozitoa hapa. Tunafanya hivi siyo kwa sababu ya ubishi, hapana; tunafanya hivi kwa maslahi ya Watanzania. Kwa hiyo, mimi nashukuru sana kwa hayo ambayo yalielekezwa

hapa. Mimi kwa upande wangu nimeridhika zaidi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamad Rashid wa mwisho kabisa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na pendekezo la Mwanasheria Mkuu, isipokuwa wakati mwingine katika biashara, mambo yote mawili yanaweza kuwezekana. Inawezekana mtu akawa *shareholder* na akawa *compensated something.* Kwa mfano, kama *land* ina *value 100 million,* akasema, basi mimi nakubali kuwa *shareholder* kwa *50%* ya hiyo *100 million,* na *50%* unipe mwenyewe *cash.* Kwa hiyo, *you will either be a shareholder or both.*

**NAIBU SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hiyo iko kwenye *line* hiyo hiyo, ila namna tu ya kuiweka vizuri.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *"shall be entitled if he so wishes to be a shareholder or be compensated or both."* Sawa. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 17

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilivyokiona kile Kifungu cha 18, ni kwamba hakikutakiwa sana kuwepo hapa kwa sababu haya ni madaraka ambayo Mheshimiwa Rais anayo ambayo amepewa na

hiyo Sheria ya *Land Aquisation Act,* yapo tayari; lakini nataka yale maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wameyasema hapa Bungeni, basi yaonekane kabisa kwenye Sheria.

Kwa hiyo, ndiyo nasema, unaweza ukaiondoa tu hiyo 18 yote halafu uka-*replace* haya maneno ukasema, "*There shall be no any displacement of people or disposition of the land as the result of implementation of this Act.*"

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

**MWENASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la Sera kwa ujumla, na Sera ni mamlaka ya Rais kwenye utekelezaji wa Sheria za Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachozungumzwa hapa, naangalia maneno yaliyotumika *very carefuly,* kwa sababu nafikiri na sisi kifungu hiki tumekikalia kuhakikisha kwamba watu hawawi *displaced.* Cha kwanza, wanasema, *Where it is necessary for the better achievement of objectives of this Act, the Minister may... (Minister* anayezungumzwa hapa ni *Minister responsible for irrigation) upon consultation with the Minister responsible for land* (Waziri wa Ardhi, kwa sababu, ndiye mwenye mamlaka ya masuala ya ardhi) *and the Minister responsible for Local Government* (kwa sababu ndiye mwenye maeneo yale).

Mheshimiwa Mwenyekiti, unasema hawa *Local Government* hawana mamlaka ya ardhi kule, lakini ile ardhi kule iko kwenye maeneo ya *Local Government.* Sasa hawa watatu wakifanya *consultation,* watamu-*advise President*

kutumia mamlaka ya Sheria aliyonayo kwenye *acquisition of land,* kutwaa ardhi kwa sababu ya *irrigation?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa *obligation* ya Rais kama *grund norm* ni kuhakikisha kwamba, watu hawatakuwa na *displacement.* Ndiyo *obligation* ya kwanza ya Rais, kwa mujibu wa Katiba. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba, kifungu hicho cha 17 kilichokuwa cha 18, kibakie kama kilivyo kwa sababu kina umuhimu sana. Hiki ndiyo kinaunga mnyororo wa mamlaka ya ugawaji wa ardhi nchini na kusimamia ardhi. Kwa sababu Mheshimiwa Rais anayo mamlaka ya kutwaa ardhi, lakini hawezi kutwaa ardhi, kwa mujibu sasa wa maamuzi yaliyofanywa na Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Hawezi kutwaa ardhi bila sababu za msingi. *That is an obligation.*

Kwa hiyo, hii ya kusema kwamba *there shall not be displacement, I do not think,* hata bila kusema kwamba, *there will be a President* ambaye atafanya hivi; na kwa mujibu wa Katiba tuliyonayo na ile inayokuja, hata kwenye Rasimu umeona, halafu awe salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kama kifungu kilivyo ni sawasawa, na mapendekezo ya Mheshimiwa Mpina ni mazuri, lakini yasiwe kwenye Sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina halafu Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatunga Sheria, hatuangalii kwamba Rais wa sasa ni nani na wa baadaye ni nani. Hatuwezi kujua baadaye

tunaweza kuwa na Rais wa aina gani. Lakini hiki Kifungu cha 18 kilivyo, tukikiweka hivyo, kinaweza kutumika kabisa kukimaliza kile kifungu, hapa kinasomeka cha 18. Kinaweza kutumika kabisa kukifanya hiki kifungu tulichokifanyia marekebisho kikawa hakina nguvu yoyote tena. Kama kitaendelea kubaki hivi kilivyo kifungu hiki cha 18, kitatumika tu kama uchochoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bora, kama alivyosema Mwanasheria Mkuu, anajua kwamba madaraka ya Rais, anaweza akatwaa ardhi wakati wowote anapoona inafaa. Kwa hiyo, hatuna hata sababu ya kuiingiza hapa, isipokuwa kama ndivyo hivyo, kama haya ya kwangu kama alivyosema kwamba, hata Rais tusipomu-*instruct,* hili ni la kwake, basi la kwangu hili tuliondoe, mimi nakubali haya mapendekezo yangu, lakini na hiki kifungu tukifute kabisa kisiwepo hapa. Kwa sababu, ukiendelea kukiweka hiki hapa, yaani hata hiki kifungu cha 17 (5) kitakuwa kimefifishwa na hakitakuwa na nguvu tena. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER N. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kutoa angalizo nikimuunga mkono Mheshimiwa Mpina, lakini kwa kiasi pia kama *Arttoney General* atakubaliana na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiacha Kifungu cha 18 kama kilivyo, na kwa kutambua kwamba ardhi inayozungumzwa hapa, kwamba, Rais anaweza kushauriwa aitwae inaweza kuangukia kwenye ardhi ya Vijiji. Wakati huo Waziri wa *TAMISEMI,* Waziri wa Ardhi, Waziri anayehusika na Umwagiliaji, wote wako Dar es Salaam na Dodoma; ardhi inayozungumziwa inaweza kuwa Kagera,

inaweza kuwa Simanjiro, lakini unajua ardhi hiyo inaangukia kwenye ardhi ya Vijiji. Hapa hujafanya *consultation* na wenye ardhi ile ambayo ni Mikutano Mikuu ya Vijiji. Kwa hiyo, bado unaweka mwanya wa watu kufanya maamuzi ambayo siyo shirikishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nia ya ku-*consult* Mawaziri hawa ni kuweka ushirikishwaji, bado dhamira ile ile itambue kwamba kuna ardhi ya Vijiji, ukiacha ardhi nyingine, ambayo iko chini ya mamlaka ya Mikutano Mikuu ya Vijiji. Wanaojua kwamba ardhi ile inatumika kwa shughuli gani, hasa ukizingatia kwamba mabonde mengine yanatumika pia kwa ufugaji na ardhi hii imeweka pembeni shughuli za ufugaji, haijatambua kwa kiasi stahiki; na ufugaji wa kisasa unahitaji umwagiliaji wa nyasi ili uweze kupata nyasi za uhakika kwa mwaka mzima; hii Sheria iko kimya, sijui italetwa lini sheria itakayotambua hayo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachosema, kifungu hiki ni lazima ama kirekebishwe kama *Arttoney General* atakubaliana na sisi au kiondolewe kwa kadiri ya mapendekezo ya Mheshimiwa Mpina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mpina. Ikibaki hivi, bado itakuwa siyo shirikishi na ardhi ya wananchi itachukuliwa bila kuwashirikisha wao. Vinginevyo kuwepo na *consultation* pale ambapo inaangukia kwenye ardhi ya Vijiji, basi mamlaka nyingine, *Local Authorities,* kwa maana ya Mikutano Mikuu ya Vijiji iwe *consulted.*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nadhani yale maelezo ya Mheshimiwa Ole-Sendeka, hapa yapo *included,* lakini kwa sababu Mheshimiwa Ole-Sendeka amesema jambo ambalo tunaliona; amesema kwamba, Mawaziri mnaweza mkakaa huko *and then* haya maamuzi yenu yasiwe *reflected* kule chini kwa sababu, utaratibu wa maelezo yale kuwafikieni ninyi huku juu umechakachuliwa hapa katikati. Sasa *I can understand that and I can agree that.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema tu ni kwamba, ukiiangalia pale mwanzoni inasema hivi: *"Where it is necessary for the better achievement of objectives of this Act."* Sawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa najaribu kufikiria, mimi nilijaribu tu kurekebisha mawazo yangu kidogo, kwa mfano unapotengeneza bwawa la kuhifadhia maji, lazima utengeneze ile *dam,* unajenga ule ukuta. Ukishatengeneza ule ukuta, lengo lako ni kuweka ule ukuta ili kuhifadhi yale maji ujenge *reservoir,* hifadhi ya maji, *depending on how much water you want to do; and this is a standard practise* ya ujenzi wa *dam* zote duniani. Kwamba, utakapoweka ukuta ule, wanasema uta-*inundate,* utafukia maeneo yaliyokuwa makavu; yatakuwa maeneo sasa ambayo yako chini ya maji.

Sasa *in that case,* unapofanya *inondantion,* maana yake ni kwamba, mmekubaliana kwamba wale watu watakaokuwa kwenye yale maeneo ambayo yatafukiwa, yatakuwa chini ya maji watahamia maeneo mengine. *This*

*has happened* kwa *projects* zote, *dams* zote *everywhere you go.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nataka kusema kwamba, ile ya *displacement,* kwenye *technical assessment* ya baadhi ya hii miradi *it is not workable.* Lakini hii ya Mheshimiwa Ole-Sendeka is *very workable.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ukienda na, *the Minister may upon consultation with the Minister responsible for Land, Minister Responsible for Local Government,* sasa iseme kwamba, hii *consultation* pia iwe imehakikisha kwamba, pana *consultation with the affected persons of the land being acquired, na kadhalika.* Kwa maana kwamba, kule chini unapopeleka kwa Mheshimiwa Rais, unasema Mheshimiwa Rais, mimi Waziri wa Kilimo na Waziri wa Ardhi, kwa pamoja kwa kuwashirikisha wananchi kile Kijiji cha pale Sengerema, kwa pamoja tunasema kwamba, tumeafikiana kwa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo sasa, unachosema ni kwamba, *responsibility* ya *consultation* ile ya Mawaziri hawa, ni lazima warudi kule kwa wananchi. Wananchi wakisema *we have not been consulted,* ina maana kwamba, unamzuia hata Mheshimiwa Rais kuridhia jambo hili kwa sababu wao hawakushirikishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane kwamba, pamoja na pale kwenye *consultation process,* ionekane wazi kwamba *the General Assemblies of the Villages involved of the persons involved has also been consulted.* Sasa hii tukiiweka

hapa, basi mimi nadhani tutakuwa tumefikia sehemu nzuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, nafikiri uko vizuri sasa kwamba lile jambo la *displacement* litoke kwa sababu nyingi tu ambazo zimeelezwa. Mojawapo ni kwamba, unapojenga miundombinu mikubwa ya umwagiliaji, ikabidi uwe na bwawa kwa mfano, chukulia Mtera; kabla ya bwawa walikuwa wamejaa watu ml, wafugaji, wakulima, na kadhalika. Lakini lilipowekwa bwawa, maji yamejaa yametengeneza ziwa.

Kwa hiyo, lazima watu wengine *naturally* wawe *displaced.* Sasa ukiweka kwenye Sheria kwamba, *there shall be no displacement* wakati ni lazima pawe na *displacement* ya maji au mambo mengine, itakuwa taabu kidogo. Ndicho wanachojaribu kukiweka hapa. Wanasema sasa tu-*accomodate* ile ya kwamba, uhusishaji uhusishe na Kijiji pia.

Mheshimiwa Mpina, nilikuona ulisimama kwanza kabla ya wengine.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwekwa hivyo itakuwa vizuri. Lakini sasa hebu waiweke tuione itakaaje kisheria? Halafu baada ya hapo, mimi sina tatizo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza haya maneno ukiyaweka yatakuwa *surplus.* Yaani itakuwa ni ziada, *of course* ni ziada ambayo siyo mbaya, kwa sababu, mtu mwenye mamlaka ya ardhi,

iwe ardhi ya Kijiji, ardhi ya wapi, ni Waziri mwenye mamlaka ya ardhi. Katika kufanya haya ambayo yanasemwa hapa, huyu Waziri lazima awashirikishe wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa nini Waziri wa *Local Government* amewekwa hapa? Kwa sababu, ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na *consultation* na watu wanaokaa vijijini. Kwa hiyo, yale maneno tunaweza kuyaweka, lakini yatakuwa *surplus.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ndivyo, afadhali kukiondoa kile kifungu, na mamlaka hayo ni *residual powers* za *President* kwenye Sheria nyingine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Umwagiliaji!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe sasa mfano halisi, yaani *what is on the ground now,* kinachoendelea. Sisi tunajenga bwawa sehemu moja inaitwa Kasuga.

Kilichotokea ni kwamba, wakati tumepanga kwamba sasa bwawa litakuwa hapa, ilichukua muda kwa sababu ilibidi Mkuu wa Wilaya na wengine wote waende kule kwanza, Wanakijiji cha Kasuga wakae wakubaliane na wale ambao watakuwa *affected* na *inundation* ya *reservoir,* halafu Kijiji chenyewe kikasema sasa sisi tutawapa maeneo mengine. Maana walikuwa wanalima, walikuwa wanachunga, wengine wana nyumba. Lakini *among themselves* wakasema sasa ninyi kama Kijiji kwa maslahi

mapana, sisi watu wachache familia tano, sita, lazima tupishe ujenzi wa bwawa hili. *Payback position* yetu ni ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *Village Council* ikaamua kwamba tutawatafutia eneo lingine ndani ya Kijiji ili wapishe. Tukai-*accomodate* na bwawa limejengwa.

Mheshimiwa mwenyekiti, sasa nilichotaka kusema ni kwamba, pengine nimwombe Mwanasheria Mkuu kwamba, hayo maneno kama hayataharibu maana, lakini yataongeza *value* ya watu kuelewa tukiya-*accomodate* itakuwa vizuri. Lakini suala la *displacement;* ametumia neno *displacement,* hilo haliepukiki. Huwezi ukafanya *reservoir* watu wakaja wakafukiwa na maji kwamba, wao wasiondolewe. Hilo haliwezekani.

**NAIBU SPIKA:** Uzuri tuko kwenye makubalino. Labda kwa dakika chache sana Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani Waziri amerahisisha mambo. Waweke kwa sababu, uzoefu unaonesha hizo *consultations* ambazo Mwanasheria Mkuu wa Serikali anazizungumza huwa hazifanyiki na Wizara, huwa hazifanyiki na *TIC* ama chombo kingine chochote ambacho kimepewa mamlaka ya kuchukua ardhi.

Mheshimiwa mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba, ili watu ambao wameshaathirika sasa, wasiendelee kuathirika, kwa sababu, Sheria ambazo zipo sasa zinazotumika kuchukua ardhi haziwatendei haki, hii hapa ieleze kwa sababu, haitaathiri chochote, sana sana itafanya watu wajue aah

haa, kumbe kwa kila ardhi ambayo inatakiwa kuchukuliwa lazima tuwe *consulted!* Ni makosa kutolea mfano bwawa kwa sababu, hapa hawazungumzi ardhi ya bwawa, wanazungumza ardhi kwa ujumla. Sasa bwawa ni mfano mdogo. Watu wanaweza wakatumia hii pale inapobidi; na pale inapobidi inaweza ikawa kwa kitu kingine na siyo lazima bwawa.

Kwa hiyo, *consultation* ni muhimu na uzuri tuna wananchi waelewa, pakiwa na uwazi. Vifichoficho ndiyo vinafanya wananchi wanakuwa na hofu. Sheria ni kwa ajili ya watu wetu. Kwa hiyo, kama watu wetu ni vilaza, tuweke Sheria hiyo hiyo katika mfumo huo huo wasioelewa wajue kwamba, tunakwenda kwenye mlengo huu.

**MWENYEKITI:** Tunarudi kwa Mwanasheria natumaini!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kukubali siyo hoja, kukubali ni maneno. Nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge na naomba kuweka maneno haya yafuatayo: Kutakuwa na vifungu viwili pale, Kifungu cha 17 (1) kama kilivyo na Kifungu cha 17 (2), kama ifuatavyo:- Sasa sijui Wataalamu wangu hapo mnisikilize na Waheshimiwa Wabunge, mtupe muda sasa kwenda kukiandika vizuri:-

*"There shall be evidence of consultations with affected persons or Village Councils of affected areas submitted to the President with the advise of the Ministers."*

**MWENYEKITI:** Bado, Mheshimiwa Sendeka?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimshauri Mwanasheria Mkuu, kama ataona haiendi kinyume; pale inaposema *Village Councils,* ambapo ardhi ya vijiji iwe ni *Village Assemblies,* kwa sababu kwa mujibu wa taratibu wa ardhi ya vijiji, sasa wanatoa *consent* ni *Village Assemblies* na siyo *Village Councils.*

Mheshimlwa Mwenyekiti, ni *General Assembly*, Mkutano Mkuu wa Kijiji.

**MWENYEKITI:** Ni sawa mnaongea lugha moja, ni vizuri. Ahsante sana. Sasa tunahoji kifungu hicho pamoja na mabadiliko yake na kifungu kipya.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ni *record,* tunaomba ruhusa ya Bunge kwamba tukiandike vizuri kwa maudhui haya haya.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Ibara ya 18

Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 21

Ibara ya 22

Ibara ya 23

Ibara ya 24

Ibara ya 25

Ibara ya 26

Ibara ya 27

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

Ibara ya 29

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 30

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya*

*Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 32

Ibara ya 33

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34

**A SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. MURTAZA ALLY MANGUNGU, MEMBER OF PARLIAMENT FOR KILWA CONSTITUENCY, AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE NATIONAL IRRIGATION ACT, 2013"**

***[Made under Standing Order 86(9) & (11)]***

A Bill entitled "The National Irrigation Act, 2013" is amended in Clause 34 as renumbered, by deleting the words "Village Council" appearing in sub-clause (1), between the words "the" and "authenticate" and substituting for them the following new words "General Village Assembly."

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kama *amendment* inavyoonyesha hapo kwamba kifungu kimetoa mamlaka kwa *Village Councils* na mapendekezo ambayo nimeyaleta, mamlaka haya yarudi kwenye *General Village Assembly,* kwa sababu kesi nyingi zinazotokea Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji wakishakaa, wanampa eneo mwekezaji, wananchi hawana habari, matokeo yake wanakuja kuambiwa eneo hili ameshapewa mwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima tuweke ukomo, wananchi washirikishwe kwa maana ya Mikutano hii ifanyike ili kuondoa ile dhana ya watu ku-*forge* ile mihutasari ya vijiji na ardhi kupewa watu ambao wananchi hawana habari nao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo lakini naomba nifahamu, kwa sababu kwenye marekebisho yaliyowasilishwa mbele yako, maneno yanayotumika ni *General Village Assembly* ambavyo mimi nafahamu ni Mkutano Mkuu wa Kijiji wa Mwaka. Sasa kama ni *Village Assembly,* sina tatizo, lakini kama ni *General Village Assembly, we need to debate that.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mangungu!

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ya lugha mara zote inakuwa ni pana sana. Lakini maana iliyomaanishwa hapa ni Mkutano Mkuu wa Vijiji, aidha uwe wa mwaka, au uwe wa mwanzo wa mwaka au ukiitishwa kwa dharura na zaidi Mkutano ule wa mwaka.

Maana ya dharura ni kwamba utaweka mfumo ambao wale wanaoonekana wakija watatoa hoja za kupinga wasipewe taarifa. Lakini ule Mkutano Mkuu ambao ni wa lazima inajumuisha watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima tuweke mfumo ambao utakuwa ni shirikishi. Nadhani hata vifungu vingine hivi vyote ambavyo Waheshimiwa Wabunge wame-*move amendments* ni kutokana na tatizo ambalo tumekuwa nalo. Wananchi hawashirikishwi katika mipango ya uwekezaji au wananchi kutokushirikishwa katika utolewaji wa ardhi kwa wawekezaji au kwa mtu mwingine yeyote.

**MWENYEKITI:** Nafikiri tunaongea lugha ile ile. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili linafanana na lile ambalo tumekwishalimaliza, kwamba suala lisimalizwe na Serikali ya Kijiji, kwa maana ya wale Wajumbe 25. Wahusishwe Mkutano Mkuu wa Wanakijiji wote.

Kwa hiyo, hoja anayoitoa, ndiko tulikotoka, ndiko tulikokubaliana. Sasa hapa labda tafsiri tu, maana wengine wanatanguliza *General Village Assembly,* wengine *Village General Assembly,* lakini hapa tuna maana ya Mkutano unaohusisha wanakijiji wote.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 35

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 36

Ibara ya 37

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38

Ibara ya 39

Ibara ya 40

Ibara ya 41

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 42

Ibara ya 43

Ibara ya 44

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 45

Ibara ya 46

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 47

Ibara ya 48

Ibara ya 49

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 50

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 51

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 52

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 53

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

**NDG. ANSELM L. MREMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 54 kimefutwa na kufanyiwa *renumbering* na sasa kifungu hicho kinasomeka kuanzia 54 – 75.

Ibara ya 54

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 55

Ibara ya 56

Ibara ya 57

Ibara ya 58

Ibara ya 59

Ibara ya 60

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 61

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 61 kina marekebisho yangu nadhani Katibu amepitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 61 nimesoma Sheria hii, hakuna mahali ambapo inawadhibiti wale watu ambao tumeshafanya jitihada zote mpaka tumewaachia ardhi sasa wa-*invest,* lakini baadaye wasifanye kazi hiyo. Sasa nikasema kwamba kifungu cha 61(a) kikifanyiwa marekebisho *wilfully damaged or fails to,* unaongeza maneno pale "*develop and maintain irrigation system or irrigation works,"* inakuwa imewa-*cover* wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pendekezo lingine la pili ni katika hiyo 61(2) ambapo inasema imeonyesha zile *penalties,* pale kwenye's' imeonyesha *penalties one, two* sasa ile two inayofuata: "*The Court may in addition to any penalty imposed under this Act, order any article in respect of which such offence has been committed or which has been used for the commission of such offence to be forfeited."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutaifisha tu kile chombo kilichotumika kwa sababu tunataka tuwakinge pia hawa watu ambao wanakwenda kuanzisha miradi hii, kutaifisha tu kile chombo kilichotumika kufanyia uharibifu haitoshi, tungeongeza na mapendekezo yangu pale niliyoweka kwamba sasa umeshataifisha kile chombo kilichotumika aidha ilikuwa ni panga au shoka au greda au nini, lakini Mahakama inaweza; unaongeza maneno yafuatayo: "*and order for compensation for the damaged caused.*" Kwa hiyo, ile itakuwa imewakinga vizuri sana watu wetu pale inapotokea wamefanyiwa uharibifu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sina matatizo sana na maneno ya Mheshimiwa Mpina isipokuwa labda sasa *formulation* ya kisheria ya Kiingereza. Lakini maneno yenyewe ukiyasikiliza, mimi naona kama yana mantiki. Sasa *formulation* ili yakae vizuri, pengine Mwanasheria atusaidie.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yaliyofanywa kwenye kifungu hiki kama kilivyorekebishwa, kwa sababu kwa sasa kinasomeka kama ifuatavyo:-

"*Any person who* (a) ambako ndiko Mheshimiwa Mpina anafanya marekebisho *wilfully damages or fails to maintain irrigation systems or irrigation works.*" Hiyo ndiyo sentensi ambayo inakwenda kwenye adhabu. Sasa Mheshimiwa anasema tuweke maneno "*develop*" kati ya maneno "*fail*" na "*maintain.*" Sasa kati ya maneno "*fail*" na "*maintain*" kuna neno "*to*". Ukiweka yale maneno sasa inasomeka kama ifuatavyo:-

"*Any person who wilfully damages or fails to develop"* (nafikiri) *and maintain irrigation system or irrigation works".* Sasa huwezi kumpa mtu adhabu yule ambaye ana-*fail* ku-*develop. You cannot do that unless* huyo mtu kama ame-*fail* ku-*develop,* unachofanya, unachukua tu. Una-*revert back,* huwezi kumpa adhabu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpina kwenye hilo, nafikiri ukubaliane na sisi.

Kwenye hili la pili la adhabu ya *compensation of damages caused,* kimsingi mimi nakubaliana naye, ingawa *compensation* ambayo *Court* inaweza kutoa hapa, ni lazima iwe kwenye misingi ya *proof of damage* na *quantum of damage.* Kwa hiyo, nakubaliana na hiyo kwamba yale maneno aliyoweka kwenye *sub section* ya pili yaingizwe kama alivyosema, lakini hii ya kwanza naona kuna matatizo kidogo ya *construction.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina!

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Nakubali.

**MWENYEKITI:** Umeafiki! Ahsante. Naona wameafikiana.

**SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilikuwa tu naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa *AG* kuhusu *61(i) and (ii).* Ukiangalia utaona kwamba, "*if it is an individual, to a fine of not less than one*

*million shillings and not exceeding five million,"* hicho pamoja na kile kingine.

Nilikuwa naomba kujua, kwa nini tunaweka *clause* hiyo kwamba isizidi milioni tano? Je, kama kosa ni kubwa, hatuwezi kuachia tu pale, *not less than one million,* halafu kama kutakuwa na ziada, kama adhabu itakuwa kubwa zaidi, *then* inaweza kuwa milioni kumi au zaidi? Kwa nini tunasema *not exceeding five million? Same* na ile inayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba ufafanuzi kutoka kwa *AG.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ufafanuzi!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshafanya maamuzi huko nyuma ya kutoweka *maximum.* Kwa msingi wa maamuzi yale, siyo kwa shingo upande, lakini kwa mantiki ya yale yale maamuzi, basi tungeondoa ile *cap* ya *ten million*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 62

Ibara ya 63

Ibara ya 64

Ibara ya 65

Ibara ya 66

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 67

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 68

Ibara ya 69

Ibara ya 70

Ibara ya 71

Ibara ya 72

Ibara ya 73

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 74

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge*

*Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 75

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Taarifa.

***Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji wa Mwaka 2013 (The National Irrigation Bill, 2013)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ibara kwa ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji wa mwaka 2013, yaani *The National Irrigation Bill* 2013 kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa taratibu zetu na Kanuni za Bunge za mchakato wa Sheria, hapa tulipofikia kwa majukumu yetu sisi ndiyo mahali pake. Muswada huu sasa utapelekwa mbele ya mamlaka ya Mheshimiwa Rais; ukipata baraka, basi utakuwa ni sheria kamili mbele ya safari.

Nitumie tu fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika - Mheshimiwa Chiza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Malima, uongozi wote wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mheshimiwa Profesa Msolla, wamefanya kazi kubwa sana, wadau mbalimbali ambao wameshiriki katika kuupitia Muswada huu; lakini vile vile pongezi kwa nyinyi Waheshimiwa Wabunge wote kwa umoja wenu. Naomba mjipongeze kwa jinsi ambavyo mmeupitia kweli kweli Muswada huu. Kwa kweli wananchi hawana budi kujivunia Bunge letu Tukufu kwa jinsi linavyofanya kazi. Mmefanya kazi mpaka nje ya muda wa kawaida, nawapongezeni sana, nasema ahsanteni sana. Tuendelee kushirikiana namna hiyo. *(Makofi)*

Pia tumejifunza baadhi ya mambo, kama hili jambo la ardhi ambalo sasa hivi linazidi kuwa *very sensitive* kwa wananchi wetu, ni jambo ambalo sasa lipo karibu sana na mioyo, hata Serikali watakapokuwa wanaleta kitu chochote ambacho kinahusu masuala ya ardhi, watakuwa makini sana kwa huko tunakoelekea. Maana tumeshaumwa na nyoka, sasa tukiona unyasi tu tunaruka.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo linawahusu Waheshimiwa Wabunge wa Kamati za *LAAC, PAC* na Bajeti, wale ambao watakwenda kuhudhuria Mkutano wa *SADC-PAC* kule Arusha kwamba wale wote mlioteuliwa mtaondoka Mjini Dodoma kuelekea Arusha siku ya tarehe 01 Septemba, Jumapili kwa usafiri wa ndege. Muda wa kuwasili uwanja wa ndege Dodoma ni saa 4.00 asubuhi. Hivyo, Wajumbe wote mnaombwa kuzingatia muda. Wale Wajumbe wa *LAAC, PAC* na Kamati ya Bajeti wanaokwenda Arusha kwenye *SADC-PAC* Jumapili saa 4.00 bila kuchelewa hapa kwenye uwanja wetu wa ndege Dodoma mnaombwa kufika pale.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 8.40 mchana Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu, Tarehe 2 Oktoba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*